BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2016 - 2020

1.	Mhe.	Zubeir Ali Maulid	-	SPIKA
2.	Mhe.	Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
3.	Mhe.	Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4.	Mhe.	Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
5.	Mhe.	Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
6.	Mhe.	Issa Haji Ussi Gavu	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
7.	Mhe.	Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
8.	Mhe.	Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
9.	Mhe.	Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais
10.	Mhe.	Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
11.	Mhe.	Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki
12.	Mhe.	Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
13.	Mhe.	Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais
14.	Mhe.	Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais
15.	Mhe.	Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani

16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais**
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe. Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe. Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe. Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe. Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**
29.	**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe. Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe. Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe. Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**

34.	**Mhe.**	**Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe.**	**Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
36.	**Mhe.**	**Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
37.	**Mhe.**	**Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
38.	**Mhe.**	**Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
39.	**Mhe.**	**Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
40.	**Mhe.**	**Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
41.	**Mhe.**	**Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
42.	**Mhe.**	**Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
43.	**Mhe.**	**Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
44.	**Mhe.**	**Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
45.	**Mhe.**	**Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
46.	**Mhe.**	**Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
47.	**Mhe.**	**Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
48.	**Mhe.**	**Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**
49.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
50.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
51.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
52.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
53.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
54.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
55.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
56.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
57.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
58.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
59.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
61.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
62.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
63.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
64.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
66.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
67.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
68.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
69.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
70.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
71.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
72.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
73.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
74.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
75.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
77.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
78.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
80.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
81.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
82.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
83.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**

85.	**Mhe. Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
86.	**Mhe. Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
	Ndg. Raya Issa Msellem	**-**	**Katibu**

Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 04 Juni, 2018

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, katika kikao cha tarehe 28 Mei, 2018, Mhe. Maryam Thani Juma na Mhe. Omar Seif Abeid waliuliza maswali ya nyongeza kwa Wizara ya Afya, yaliyotokana na swali la msingi Nam. 48 na Mhe. Waziri aliahidi kujibu maswali hayo kwa maandishi. Sasa, namuomba Mhe. Waziri wa Afya asome majibu ya maswali ya nyongeza yaliyoulizwa na Wajumbe hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe.shimiwa Maryam Thani Juma kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kazi za michoro na mambo mengine niliyoyataja zilighariimiwa na Wizara ya Afya na jumla ya shilingi 26,000/- zilitumika kwa kazi hiyo. Aidha, wizara imepanga kutumia jumla ya shilingi bilioni moja kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa nyumba hizo kwa mwaka wa fedha huu tulionao 2017/2018.

Mhe. Spika, napenda kumjibu swali lake Mhe. Omar Seif Abeid alitaka kujua kiasi cha fedha zilizogharimu katika kuwalipia kodi ya nyumba za wafanyakazi wanaofanyakazi Hospitali ya Mkoani.

Jumla ya shilingi milioni 75,600,000/- zilitumika kwa ajili ya kulipia kodi ya nyumba za madaktari na wafanyakazi wa Hospitali ya Abdalla Mzee, kwa hatua za awali. Ahsante Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny. Waziri wa Afya): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Masoud Abrahaman Masoud (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Hati Mezani Kuhusu Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka 2018/2019. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 66

Kujiunga kwa SMT katika Jumuiya ya *OIC*

Mhe. Simai Mohamed Said – Aliuliza:

Kwa kuwa Jamhuri ya Muungano sasa imejikita katika Diplomasia ya Kiuchumi (*Economic Diplomacy).*

Je, SMZ imefikiria kuishauri SMT kujiunga na Jumuiya za Kimataifa zenye maslahi ya kiuchumi kama vile *OIC* ambayo tayari wanatambulika na Umoja wa Kimataifa na kuwa wanakiti chao pia katika umoja huo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Simai Mohamed Said swali lake Nam. 66 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Pamoja na kwamba Umoja wa Mataifa (*UN*) inaitambua rasmi *OIC*, zamani ikiitwa (*Organization of Islamic Conference*) siku hizi inaitwa *Organization of Islamic Cooperation* na kuipa fursa ya kuwa mwalikwa wa kudumu katika baadhi ya vikao vyake, bado SMZ haioni kama muda huu ni wakati muwafaka kwa kuishauri SMT kuhusiana na suala la kujiunga na Jumuiya hio. Wakati muwafaka ukiwadia SMZ haitosita kufanya hivyo.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Spika, japo kuwa swali langu lilikuwa ukiangalia lina mistari 6 na majibu ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi yana mistari minane *any way* wacha nitauliza swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Waziri, katika majibu yake mstari wa mwisho anasema kwamba wakati wa muafaka ukiwadia SMZ haitosita kufanya hivyo. Sasa mimi niulize ni miaka mingapi sasa hivi ishapita tangu swali hili la *OIC* lilianza kujadiliwa ndani ya Jamhuri ya Muunguno wa Tanzania pamoja na SMZ na tutakumbuka tu kwa majibu hao. Sasa ni muda gani tunaohitaji jamani angalau wananchi wakapata kufahamu ili SMZ ataweza kuishairi SMT katika kuangalia.

(b) Lakini halkadhalika tumeona mara nyingi kwamba nchi yetu sasa hivi tuna Balozi hapa tulitajiwa juzi tuna balozi 41 na tumeona sasa karibuni kwamba Jamahuri ya Muungano wa Tanzania imefungua ubalozi rasmi sasa katika nchi ya State of Israel na pia juzi imesherehekewa kwa nguvu nyingi sasa niulize ni kipi kimekuja mwanzo Zanzibar kutaka kujiunga *OIC* au Israel na kwa nini muda mrefu tukapata kujuwa rasmi majibu kama je tunaweza kujiunga twende kwa ajili tupate kufaham. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Simai Mohamed Said maswali yake mawili (a) na (b) ya nyongeza kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, Mhe. Simai Mohamed Said anataka kujuwa kwa muda gani tokea lilipoanza hili jambo na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nini imechukuwa muda mrefu, jambo hili kwa mara ya kwanza lilitokeza nchini kwetu mwaka 1993 ndipo ilipokwenda *motion* makusudi na baadae likatolewa na sababu ya kutolewa ni kwamba jambo hili ni jambo la Kikatiba, ukisoma Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 77 Kifungu cha 4 ibara ndogo ya tatu ukaenda kwenye nyongeza ya pili ya mambo ya Muungano jambo hili ni la pili.

Kwa hiyo, hoja ya wakati ule bado ipo na wakati muafaka maana yake kwamba taratibu, sheria, na kanuni zitakaporuhusu ndio itakuwa muafaka wakati kwa hapa hatupimi kwa miaka tunapima kwa mujibu wa taratibu, miongozo na kanuni zitakaporuhusu hatutosita Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kushauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika jambo hili.

(b) Mhe. Spika, alitaka kujuwa kwa nini Serikali ya Jamhuri imefungua ubalozi katika nchi ya Israel ni *policy* ya nchi kwamba tunakwenda katika *diplomacy economy* na kama yalivyo maagizo na maelekezo ya taifa lolote duniani mnapoanzisha urafiki mnaangalia maslahi kwa wakati ule na *future*. Kwa hiyo, imani ni kwamba Tanzania na Israel zimekuwa na uhusiano kwa muda mrefu tumekuwa tukisaidiana nao muda mrefu, wamekuwa wakitusaidia mambo mengi, tumekuwa tukiwasaidia mambo mengi kama ilivyo desturi ya nchi mnapofungua balozi hizo. Imani yangu na wao nchi ya Israel itafungua ubalozi wao nchini tutaendelea kuimarisha mahusiano yetu yaliopo kwa faida ya wananchi wanchi zote mbili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, name nimuulize swali dogo sana la nyongeza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Kwa kuwa, suala la *OIC* limezingatiwa katika rasim ya Katiba Mpya ni lini mchakato huo utakamilishwa ili wazanzibar waweze kunufaika na *OIC* na ulisema vile vile hapa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano vile vile masuala ya mafuta na gesi imo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ili kupitisha hili ipate kuondolewa.

Mhe. Spika: Vipi Mhe. Waziri umemfahamu hebu Mhe. Jaku liulize tena kwa taratibu kidogo

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuwa swali la msingi linahusu *OIC* na limezingatiwa katika rasimu ya Katiba Mpya, ni lini mchakato huu wa Katiba utakamilishwa ili wazanzibar waweze kunufaika na *OIC* na vile vile alinukuu Kanuni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nataka kumwambia tu likapita hili na suala la mafuta na gesi litaondoshwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub maswali yake (a) na (b) ya nyongeza kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, katika Rasimu ya Katiba inayopendekezwa halikutajwa suala la *OIC* imetajwa fursa ya Zanzibar kuweza kujiunga na Jumuia ambazo hazitokuwa na ulazima wa *sovereign state* kuweza kuwa mwanachama kwa hiyo imani yangu kwamba mchakato wa katiba hatuwa iliyobakia kwenda kupiga kura itakapopigwa kura jambo hili litakwamka kama *OIC* mahitaji yake yatakuwa ni *sovereign state* bado Zanzibar hatutokuwa na fursa ya kuweza kujiunga.

(b) Mhe. Spika, *OIC* na suala la mafuta kikatiba, bado kwenye katiba ipo lakini sheria imeweza kutoa fursa kwa upande wa Zanzibar na upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maana kwamba Tanzania Bara kuwa na sheria tofauti zinazosimamia suala la utafutaji na uendelezaji wa masuala ya mafuta. Kwa hiyo, sheria zinaruhusu upande wa Zanzibar tuna sheria yetu na upande wa Serikali ya Jamhuri wana sheria yao iliyotungwa mwaka 2015.

Nam. 80

Uchakavu wa Kituo cha Afya cha Kitogani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Kituo cha Afya cha Kitogani kimekuwapo pale muda mrefu mpaka sasa kimechakaa na wananchi wa Kitogani wanakitumia kupata huduma za afya.

Je, lini Kituo cha Afya cha Kitogani kitafanyiwa ukarabati.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 80 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba nikiri na nikubaliane kabisa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba Kituo cha Afya cha Kitogani ni kituo kikongwe ambacho kwa sasa kimechakaa na kwamba kinahitaji kufanyiwa matengenezo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ya Wilaya ya Kusini imepanga kukifanyia matengenezo makubwa kituo hicho yakiwemo, kuezeka, kuweka dari pamoja na rangi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nitakuwa mtovu wa adabu wa mwisho kama sikumpongeza kwa dhati Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ leo, nikupongezi kwa dhati Mhe. Naibu Waziri na nanafikiri

katika kuuliza maswali yangu tokea kuteuliwa leo lilikidhi kunijibu swali hili la msingi nikupongeze kwa dhati na huu ndio uungwana. *(Makofi).*

Hapa Mhe. Spika, hatumtii mtu adabu tunauliza maswali ya wananchi leo kakiri na nimpongeze tena na ndio uugwana uliounyesha kwa kujibu swali la msingi.

Mhe. Spika, naomba kumuuliza swali moja tu dogo la nyongeza, unajuwa akeshakujibu mtu ukweli utakuwa hata mdomo keshakuziba huwezi kuuliza swali jengine kwa ukweli.

Mhe. Naibu Waziri, kwa vile kituo ni cha muda mrefu kimetengenezwa nafiriki 1860 au 80 na *population* ya watu imekuwa, kituo kile kimejengwa miaka utakubaliana nami ukarabati huu hautokidhi hivi na patahitajika kujengwa kikuko kikubwa *atleast* kuliwahi kutokea kipindu pindu mara 2 na zikawekwa kambi pale *population* ya watu wa Kitogani imekuwa, Jazani imekuwa na Muungoni imekuwa ni kuombe tu pamoja na majibu yako ...

Mhe. Spika: swali Mhe. Jaku Hashim Ayoub

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: je, ni lini utakubaliana na mawazo yangu kwenda kukiangalia mimi na wewe mguu kwa mguu uone ukweli ulivyo wa suala hili wa kituo kile.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, naomba nitoe maelezo mafupi kwamba, Mhe. Jaku Hashim Ayoub nakubaliana na pongezi ambazo umezitowa lakini vile vile Mhe. Mjumbe nimuombe tu kwamba pale na sisi ambapo tunampa majibu yale ambayo yeye anahofu nayo naomba akubaliane na sisi kama vile ambavyo kwa kweli yale unayoyasema ya kweli na sisi tunakubalian naye.

Mhe. Spika, ukweli ni kwamba Kituo cha Kitogani kama nilivyotangulia kusema kwamba kimechakaa na haja kama alivyosema Mhe. Mwakilishi kwamba kutokana na ongezeko la watu kule ambao wanahudumiwa na hizo kambi ni kweli zishawahi kufanyika kwa ajili ya masuala ya kipindupindu naomba nikubaliane na hilo. Lakini, nimwambie Mhe. Mjumbe kwamba tuwache kwanza tufanye matengenezo hayo ili kusudi kuweza kuhami na baadae tutaangalia kwa namna gani hiyo haja lazima tukubaliane ipo na mimi Mhe. Spika, naomba nimueleze Mhe. Jaku kwamba mimi tayari nimeshafika na nimeshatembelea na ndio mana nikakiri kuweza kuyasema hayo ambayo nimeweza kuyasema.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Spika, kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa majibu yake mazuri na kikuri kwamba Kituo hicho cha Kitogani ni kituo kikongwe na kinahitaji matengenezo lakini mbali na kituo cha Kitogani kuna kituo kikongwe zaidi ambacho kipo katika jimbo la Kikwajuni maeneo ya Rahaleo. Je. Nimuulize Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ anakijuwa kituo hicho na kama hakijui ni lini atafanya ziara ili kwenda kuangalia changamoto katika kituo hicho cha Afya cha Rahaleo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, naomba nikubaliane kwamba kituo cha afya ambacho kiliopo eneo la Rahaleo Jimbo la Kikwajuni, mimi binafsi sijawahi kufika. Lakini vile vile kwamba ni lini ambapo tunaweza tukakubaliana kwenda kutembele nimpongeze sana Mhe. Mwakilishi kwa namna ambavyo tumekuwa tukishirikiana kwa miradi mbali mbali ambayo mimi binafsi huwa ananitaka niende tunaenda. Kwa hiyo, na hili kwa upande wangu kwa sababu ni jambo ambalo nishalizoea naomba na niwajibu wangu basi kwa maana hiyo nimwambie kwamba wizara iko tayari kwenda katika jimbo hilo ili kuona kituo cha afya hicho na vyengine ambavyo tayari vimegatuliwa.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa ruhusa yako naomba kuuliza maswali mawili mafupi ya nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri ambayo yanakidhi haja na majibu ambayo mwenye hili swali kakiri kwamba kafikia kiwango ambacho kinakubalika katika Baraza letu swali langu lipo hapa.

(a) Mhe. Spika, wananchi wetu wanaendelea kujenga vituo kwa ajili ya kuwaondolea usumbufu wananchi katika maeneo mbali mbali moja wapo langu mimi Jimbo la Kijitoupele. Kituo cha Afya kipya kipo Magirisi (Taveta). Je, Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwanza hili analijuwa kama kituo hicho kipo na atatembelea lini.

(b) Mhe. Spika, ili wananchi waondokane na mawazo tofauti kuna hospitali zetu kuu na kuna vituo vya afya ugatuzi unaelekea wapi, ili wananchi waelewe kuondoka na usumbufu wa maombi ya mambo yao mbali mbali.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, itakumbukwa kwamba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ alipokuwa akiwasilisha hotuba ya bajeti moja katika jambo ambalo alilitolea ufafanuzi alieleza bayana kwa namna ambavyo ugatuzi umefanyika ni kwamba ni mpango mkakati ambao umepagwa kiwizara kwamba tuvitembelee vituo vyote ambavyo vimegatuliwa ili kusudi na sisi kuweza kuvijuwa na namna gani ambavyo yale mahitahi ambayo yanahitajika tuweze kuvifanyia matengezo au kufanya marekebisho. Kwa hiyo, kituo cha Magirisi Mhe. niseme nakisikia lakini mimi sijawahi kukitembele kituo hicho, na kuwa ni jambo ambalo tumesema baada ya kumaliza kwa bajeti hii, basi tutafanya kuvitembelea vituo vyote vya Unguja na Pemba, ili kubaini mapungufu na mahitaji mbali mbali, ili kuwaongezea ufanisi zaidi wananchi.

Vile vile, kuhusiana na vituo vipi ambavyo tumegatua. Mhe. Spika ni kwamba kwa mujibu ambavyo tumeelezea mara nyingi ni kwamba vituo ambavyo vimegatuliwa ni lile daraja na kwanza na daraja la pili, kwa maana kwamba zile hospitali za wilaya pamoja na za mkoa zile zitabakia katika usimamizi wa wizara husika, lakini sambamba na hayo kuna mambo baadhi yao tumegatuliwa katika vituo hivyo hivyo, lakini kuna baadhi ya mambo yatabakia wizara husika. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante Mhe. Spika kwa kuniona pamoja na majibu mazuri sana kwa ruhusa yako na majibu yenye afya naomba kumuliza Mhe. Waziri hili lifuatalo.

Katika miaka minane nyumba Tunguu ilijengwa nyumba ya daktari karibu na kituo cha afya Kusini, je nyumba ile imejengwa na mfadhili anaitambua nyumba ile iko na kwa muda huu nyumba inatumika kwa madhumuni ya afya au mengineyo, nyumba hiyo iko kona kuelekea njia ya Makunduchi kupitia njia ya Ndijani. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, naomba nitoe majibu ya ziada kwa Mhe. Mwakilishi Ahmada Yahya Mwakilishi mahiri sana, ambaye ni mdau mkubwa ni muhusika mkubwa katika taasisi yetu hii, katika kutusaidia mambo mengi.

Lakini naomba nirejee Mhe. Spika, ni kwamba tumesema kwamba tuna mpango ule wa serikali ambao serikali za mitaa, vituo hivi ambavyo tumegatua, tumevigatua lakini bado hatujafanya ziara ya kuvitambua, tulivyovitambua ni vichache mno kwa maana hiyo inawezekana hiyo nyumba ipo na inawezekana kama ni yakwetu, lakini pia inawezekana ni kwa mazingira mengine. Kwa hivyo, naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba nalo hilo tutalifanyia kazi, tutafika ili kuona na kulibaini hilo jengo ili tujue nani muhusika au nani mmiliki wa jengo hilo. Ahsante.

Nam. 82

Ukosefu wa Kituo cha Daladala Mjini

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Wananchi wengi wanaosafiri kupitia Bandari ya Malindi Zanzibar wamekuwa wakisumbuka wanapotoka au kwenda Bandarini hapo kutokana na umbali wa masafa na kukosekana kituo cha daladala cha karibu.

Je, hatua gani zitachukuliwa kusogeza huduma za usafiri wa daladala hasa ukizingatia wapo wazee, watoto na akinamama ambao wanasumbuka kutokana na umbali huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashimi Ayoub Mwakilishi makini, mahiri swali lake Nam. 82 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, uwekaji wa vituo vya daladala upo kwa mujibu wa Sheria *"Road Decree 1925 cap. 134"* pamoja na Marekebisho yake Nam. 17/2013 chini ya Wizara dhamana ya Usafirishaji. Hata hivyo, Mhe. Spika ni vyema iyeleweke kwamba uamuzi wa kuweka vituo vya daladala unafanywa kwa kuzingatia vigezo maalum ikiwemo masafa, ukubwa wa barabara husika kwa ajili ya kujenga *"bus bay"* na kadhalika.

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ itaendelea kushirikiana na Wizara husika pamoja na taasisi nyengine kuona namna bora ya kulishughulikia jambo hili ili kuwaondoshea wananchi wetu usumbufu kama malengo ya serikali yalivyo. Mhe. Spika, pamoja na hayo, kwa hivi sasa Bodi ya Usalama Barabarani inakamilisha kazi ya kufanya mapitio ya suala zima la vituo vya daladala na hatimae kuishauri wizara husika. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, duniani kote mji au miji kunakuwa na kituo kikuu cha usafiri, ambacho kinaunganisha usafiri wa kuingia na kutoka maeneo tofauti, Zanzibar kituo chetu kikuu kipo wapi ili wananchi wapate kujua kituo chao kikuu kiko wapi. Hilo la kwanza.

Pili je, mmetumia kigezo gani cha kuondosha kituo Darajani na badala yake pale pale Darajani umefanya maegesho ya magari, kuwapa wananchi usumbufu na serikali hii iliahidi ndani kituo cha Kijangwani kitajengwa hivi karibuni huu mwaka wa pili au mipango miji iko *ICU* mpaka muda huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, naomba nitumie fursa hii pia, kumpongeza tena Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa namna ambavyo anajitoa katika kusimia au kutetea maslahi ya wananchi wetu. Kwa kweli, serikali imeliona jambo hii na nisema kwamba, kutaka kujua kwamba kituo cha kituo kikuu cha huduma za daladara katika mji wa Zanzibar ni kwamba tukumbuke kwamba kwa sasa hivi tunaelekeza nguvu zetu katika eneo lile la Kijangwani kama ambavyo mipango ya serikali imeshaanza kuonekana pale.

Lakini ni kweli ni kwamba kituo kile bado kikuu ambacho tunasema kwamba hichi ni kituo kikuu bado hakijakuwepo kama vile ambavyo tumesema, lakini hatimae kwa kuwa jambo hili linashirikisha taasisi nyingi naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba kituo kikuu, kitapatikana pale ambao kwa kweli tumeshafikia maamuzi na imeonesha kwamba kuna matayarisho ambavyo yameshafikiwa katika hatua ya mwisho katika kufanikisha jambo hilo.

Lakini kwa nini Darajani kwamba kituo kile tumekiondosha, Mhe. Spika ni kweli kituo cha Daladala tumekiondosha kutokana na haja ambayo sasa hivi, imekuwapo na mpango mkuu wa serikali kulijenga, kuliboresha eneo lile la Darajani, ambalo hatimae ninakuja kutoa taswira nzuri na ambayo yenye mafanikio makubwa, kulikoni hicho ambacho labda tulikitaka kiweko katika maeno yale pale. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Mwakilishi kwa hili atuvumilie na aendele kuvuta subira na tuwelishe wananchi wavute subira, serikali haikusudii kuwatesa wananchi na baada yake kuna mipango ambayo itaweza kuleta mafanikio zaidi.

Lakini Mhe. Spika, kuhusu kituo cha Kijangwani kwamba kimekaa muda mrefu. Waheshimiwa Wajumbe, naomba tukubaliane kwamba juhudi za serikali zimeshafanyika, hatua haikuweko pale tumepita hatua kwa hatua tuliweza kuondoa wafanyabiashara waliokuwepo pale ni moja katika *process* yao, kati ya hatua lakini vile vile, tukajaanzisha pale tukaweka katika hali ambayo muonekano unaonekana sasa hivi, lakini hatima baada ya hapo ile kazi ya mwisho itaweza kufanyika ikiwemo na ujenzi huo bado kama unavyoonekana kwamba hatujakamisha na tunaendelea.

Mhe. Spika, naomba tuvute subira kidogo zimalizike hizi mvua tuweze kufanya kazi ambayo yenye ufanisi zaidi.

Nam. 56

Ucheleweshwaji wa Uingizwaji wa *OC* kwa Baadhi ya Taasisi za Serikali

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza:

Zanzibar ni miongoni mwa nchi za kupigiwa mfano katika Bara letu la Afrika kwa hatua zilizofikiwa katika ukusanyaji wa mapato kupitia vianzio vyake vya ndani.

(a) Je, ni kitu gani kinachopelekea baadhi ya taasisi za serikali kukosa *OC* kwa baadhi ya miezi.

(b) Je, kudumu kwa tatizo hilo kwa muda mrefu sasa hatuoni tunapelekea kudhorotesha kazi zilizopangwa kutotekelezwa kupitia bajeti husika.

(c) Kwa nini bajeti inayopitishwa na Baraza la Wawakilishi kwa baadhi ya taasisi za serikali huwa hazipatikani kama zinavyoombwa na idara au taasisi husika.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali Nam. 56 Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa naomba kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Kwa utaratibu, serikali inatumia mfumo wa fedha taslimu kwa maana *(cash budget system)* katika matumizi. Kwa mfumo huu, matumizi ya kila mwezi hupangwa kwa kutegemea matarajio ya mapato ya mwezi husika, mahitaji muhimu ya serikali na maombi ya kila wizara au taasisi kwa kulingana na bajeti yake kwa maana ya *cash flow* jumla ya mahitaji ya fedha hulinganishwa na matarajio ya mapato na matumizi mengine ya laziman na mgao wa fedha kwa matumizi na kikasma huzingatia mambo yote hayo kila mwezi.

Baada ya maelezo hayo ya jumla naomba kujibu swali lenye vipengele (a)(b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kimsingi Wizara na taasisi zote za serikali zinazopokea fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina hupata fedha za *OC* kila mwezi baada ya mazingatio nilliyokwisha eleza katika maelezo ya awali.

(b) Hakuna tatizo lililodumu la kukosekana *OC* ya mwezi hivyo hatuna tatizo la kuzorotesha kazi zilizopangwa.

(c) Kwa kweli, kama nilivyoeleza awali utoaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti iliyoainishwa hutegemea mambo mengi yakiwemo kiasi halisi cha mapato kinachokusanywa na mahitaji muhimu ya serikali.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza pamoja na majibu ya mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Je, ni utaratibu gani unaotumika wa kuingiziwa fedha taasisi ambazo hakulipanga jambo la kutekeleza lakini likatokezea ni muhimu kwa utekelezaji.

(b) Je, kwani tunapofikia mwisho wa mwaka kuna taasisi zinaripotiwa kwamba hazijapatiwa fedha asilimia 100 na huku anatwambia hakuna ukosefu wa bajeti kwa baadhi ya miezi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika,

(a) Iwapo wizara au taasisi haina fedha katika bajeti yake na limetokea jambo la muhimu kuna mambo mawili yanafanyika, ama taasisi hiyo inahaulisha vifungu vyake na uwezo huo anao waziri, baada ya kumuandikia Waziri wa Fedha na Mipango na kupata idhini yake kunatokea na uhaulishaji wa fedha kutoka fungu moja kwenda fungu jengine. Lakini kama tatizo hilo ni kubwa na linahitaji mazingatio maalum tunaweza ukafanyika uhaulishaji kutoka fungu la wizara moja kwenda fungu la wizara yengine, lakini pia ikiwa haya ipo na bado tumo ndani ya *ceiling* ya bajeti basi uwezo wa kutumia Mfuko Mkuu wa Serikali pia upo. Lakini alimradi shughuli za serikali haziwezi kukwama kutokana na ukosefu wa fedha.

(b) Aliuliza kwamba zipo taasisi mpaka mwisho wa mwaka zinakuwa hazikupata fedha, upatikanaji wa fedha ni wa asilimia *zero* kama nimesikia vizuri. Nadhani katika miaka mitatu hii, hali hiyo haijawahi kutokea na hata kukitizama kwa bajeti za wizara ambazo zimeshapita nyingi zao katika kipindi cha miezi tisa basi wamepata fedha asimilia kuanzia 70 – 80 – 90 zipo, na yapo maeneo machache sana ambayo yana asilimia 56 – 57. Lakini niseme tu, kwamba bajeti yetu ni *cash budget* tunachokusanya ndicho tunacho gawana baada ya kutoa matumizi ya lazima.

Lakini kwa ujumla hali ya upatikanaji wa fedha kwa taasisi za serikali hivi sasa umeimarika zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Saidi: Ahsante sana Mhe. Spika, nilikuwa na swali dogo la nyongeza, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa.

Mhe. Spika, katika mfumo ambao tunautumia sasa hivi baina ya serikali zetu na halmashauri ni kupeleka ugatuzi au *devolution of power* katika halmashauri zetu, sasa ni kweli kuna halmashauri bado nyengine uwezo wake wa kifedha bado ni haupo, kuna tafautiana na maeneo tofauti hasa kwa upande wa Pemba pamoja na Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja.

Je, ni utaratibu upi ambao serikali kuu au unatumia katika kusaidia katika masuala ya *OC* na maeneo mengine ya kifedha wanawasaidia halmashauri hizi, ambazo bado zina changamoto katika ukusanyaji wa mapato, lakini katika mfumo mzima wa matumizi na mapato ni wanatumia mfumo upi wa serikali kuu wa kuweza kuzisaidia hizi halmashauri ahsante sana.

Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, kwanza huu ni mwaka wa kwanza wa ugatuzi na ni maeneo matatu ambayo yamegatulia afya ya msingi, elimu ya msingi lakini pia na huduma za ugaani katika sekta hii, kwa kiutaratibu kwamba fedha zote zile zilizokuwa katika mawizara zimetolewa na kupelekwa kwenye Halmashauri na Mabaraza ya Mji kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za ugatuzi.

Lakini, nisema tu kwamba ipo Kamati Maalum imeundwa kuangalia uwezo wa kila halmashauri uwezo wake wa mapato yake ya ndani kila Halmashauri, na baada ya hapo serikali itakuwa na mazingatio maalum, na tunaita *equalization formular*, ili kuhakikisha kwamba kila Halmashauri au Baraza linapata uwezo wa kuendesha shughuli zake. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika na swali langu mimi dogo tu, na kama litakataliwa unilinde kwa Kanuni ya 38 Mhe. Spika.

Mhe. Waziri swali la msingi katika ukusanyaji wa mapato kupitia chanzo vyake vya ndani ni swali la msingi aliloulizia Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, hivi karibuni tu Mhe. Waziri tumesikia kauli kutoka Bungeni kuna pesa Zanzibar katika mgao wake, sijui 203.9 milioni je, pesa hizi kweli zipo na kama zimekuja Zanzibar utupe kauli na kama litakuwa gumu hili swali naomba unijibu wa maandishi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, swali hili tayari ameshalizungumza, na nilikwisha litolea majibu katika mkutano huu. Lakini nataka kumuhakikishia Mhe. Mjumbe akikosa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, atakuta kwamba shughuli za Bunge zinazohusu masuala ya Bunge hazipaswi kujadiliwa katika Baraza la Wawakilishi.

Na hili suala hili ambalo analizungumza linatokana na ripoti ya *CAG* ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ni suala ambalo lilizungumzwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nisingepaswa kupata majibu yake katika Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Nam. 224

Uimarishaji wa Hoteli za Chake, Mkoani na Wete

Mhe. Ali Suleiman Ali – Aliuliza:

Katika kukuza utalii nchini, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, Rais wa Kwanza wa Zanzibar alijenga Hoteli katika Kisiwa cha Pemba katika maeneo ya Mkoani, Chake Chake na Wete, ili kuimarisha uchumi nchini.

(a) Je, hoteli hizo bado zipo chini ya mikono ya serikali au zimekodishwa.

(b) Je, wizara ina mpango gani wa kuliokoa jengo la hoteli ya Mkoani ambalo lipo katika hali mbaya hivi sasa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kujibu swali lake Nam. 224 la Mhe. Ali Suleiman Ali kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa serikali ilijenga hoteli katika Miji ya Mkoani, Chake – Chake na Wete.

(a) Hoteli zote tatu bado zinamilikiwa na serikali. Kwa sasa, jengo la Hoteli ya Wete limekabidhiwa Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*) na linatarajiwa kubadilishwa matumizi na kutolewa huduma za kibenki. Jengo la Hoteli ya Chake - Chake limekodishwa kwa kampuni ya *National Marketing Ltd* na jengo la Mkoani serikali imeamua kuipatia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*).

Mhe. Spika, baada ya kupatiwa na serikali, *ZSSF* inaendelea na tathmini ya jengo hilo na inatarajia kulifanyia matengenezo makubwa. *ZSSF* inatarajia kutumia jengo hilo kwa shughuli za hoteli katika Wilaya ya Mkoani.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa ruhusa yako naomba kumuuliza swali la nyongeza.

Kwanza kabisa nimpongeze kwa dhati kabisa au naipongeza serikali kwa kuhakikisha kwamba rasilimali majengo yetu, yale ya Wete, Chake Chake na Mkoani yako salama na yanaendelea kutoa huduma au yanatarajiwa kutowa huduma kubwa kwa jamii yetu.

Pamoja na mpango mzuri huo, nataka kumuliza Mhe. Waziri majengo haya tumefaidika na kumbukumbu ya historia ya nchi yetu. Je, kwa majengo mengine yoyote ya serikali kama hayo, mfano jengo la Benki ambalo liko Mkwajuni na jengo la Makunduchi yamehifanyiwa salama na yako mikono ya serikali au yamekodishwa na taasisi gani.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, kwanza hivi sasa ni dhamira ya serikali kuhakikisha *asset* zote za serikali zinalindwa, zinatengenezwa, zinatunzwa hiyo ndio dhamira ya serikali *asset* zote, iwe majengo iwe mashamba iwe vyombo vya kufanyia kazi hiyo ndio dhamira ya serikali, na kama ilivyofanyika kwa majengo haya yaliyokuwa yakitumiwa kama hoteli, Chake Chake, Mkoani na Wete kwa *asset* nyengine za serikali zitachukua hatua kama hizo. *(Makofi)*

Pale itakapoona kuna haja ya jengo kukodishwa, litakodishwa lalini kwa maslahi ya serikali na kwakufuata taratibu za kisheria na pale itakapoonekana kwamba jengo hilo litafaa kutumika, kwa shughuli nyengine yoyote ile ya kiserikali basi serikali haitosita kufanya hivyo. Na hii si kwa majengo hayo, lakini kuna majengo kwa mfano ya ilichokuwa Kiwanda cha Sigara Maruhubi, majengo yale sasa yamebadilishwa yamepewa hadhi ya kutosha na yanatumika kwa taasisi nyengine. Kwa hivyo, na hayo yatafanyika kwa majengo hayo aliyoyataja ya Makunduchi na Mkwajuni.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kwa kuweza kuuliza suala la nyongeza dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, katika majibu yako umesema kwamba serikali ina nia njema ni kweli hilo kwa kuyadhibiti yale majengo pamoja na mashamba, lakini kuna tetezi kwamba kuna mashamba baadhi ya mengine yamemilikiwa na watu binafsi. Je, wizara au serikali ina mpango gani wa kuyarudisha mashamba yale kwenye mkono wa serikali na kuyatoa kwenye mikono ya watu binafsi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, kwanza sina hakika shamba lipi analizungumzia Mhe. Mwakilishi ambalo linamilikiwa na mtu binafsi. Lakini niseme tu dhamira ya serikali na tayari imeshaonesha kwa sababu kumefanyika tathmini ya kina kabisa ya kujuwa mashamba yote ya serikali Unguja na Pemba na utaratibu unafanywa kwa kuhakikisha kwamba hao walionayo mashamba hayo wanayamiliki kihalali kwa njia zinazotakiwa kwa mujibu wa sheria. Sasa kama lipo ambalo limeshauliwa Mhe. Suleiman Makame Ali analijuwa atupe tu taarifa nalo litafanyiwa kazi kwa maana ya kwamba kuhakikishiwa huyu anaelimiki basi analimiki kwa mujibu wa sheria na utaratibu wa nchi.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, na nakushkuru kwa kuniona kwanza nimpongeze Mhe. Waziri na majibu mazuri aliyoyatoa.

Mhe. Spika, pamoja na suala mama na majibu aliyoyatoa ya kuhusiana na majengo ya serikali ambayo yalikuwa yakitumika kama mahoteli kwa upande wa Chake chake, Wete na maeneo mengine kwa upande wa Pemba, lakini halikadhalika kwa upande wa Unguja kuna Hoteli ambayo ni ya Bwawani ambayo serikali ilipanga katika kuboresha mradi mkubwa wa kuendeleza eneo lile na hadi hivi sasa kwamba eneo la Bwawani limekuwa ni kichaka la kujificha mashetani pamoja na wizi ambao unaendelea hadi watu wamekuwa wakipita sasa hivi wanakuwa wanaogopa na usiku unakuwa unasikia masauti ambayo hayajuilikani.

Sasa, niulize ni nini kauli ya serikali hasa baada ya kutoa ahadi nyingi kwamba pataendelezwa ajira zitapatikana mji utakuwa na hadhi mpya, patapendeza, maduka, biashara lakini bado hali ilivyo sasa hivi ni bora ilivyokuwa ya zamani, sasa ni nini kauli ya serikali juu ya suala la Hoteli ya Bwawani.

Lakini halikadhalika tuna visiwa katika maeneo ya Unguja na Pemba ambayo pia vinamvuto sasa tunajua kwamba kwa mfano kisiwa cha *Prison Island* kimekuwa kimetumika kama eneo hilo hilo la kitalii wakiwa chini ya *Zanzibar Tourist Cooperation* ambayo kimetumika kama wazamani kampuni ya *Furaha Hotels*.

Sasa kwa nini serikali isifikirie kubadilisha matumizi ya umiliki wa kile kiwa cha *Prison Island* hasa katika mapato yanayopatikana hayaendani na hadhi ya ile kisiwa chenyewe cha *Prison Island* au Changuu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, kwanza nimhakikishie kwamba Hoteli ya Bwawani haijatelekezwa bado serikali iko katika mazingitio ya kuhakikisha kwamba kazi iliyokusudiwa kufanywa katika hoteli ile inafanyika, kwa hivyo hilo suala la kuchelewa ni suala

jengine, lakini suala la dhamira ya serikali ya kuendeleza jengo la Bwawani iko pale pale na itafanyika *Ishaallah* Mwenyezi Mungu akipenda wala hilo lisiwe na mashaka kwa Mhe. Mwakilishi, serikali inajua kuna kazi inafanyika na mara baada ya kukamilika kazi hiyo basi shughuli za ujenzi zitaanza kama ilivyokusudiwa pale mwanzo pasiwe na wasiwasi, hizo sauti anazozisikia sijui anakwenda kufanya nini wakati wa usiku. Lakini kwa kawaida naamini kabisa dhamira ya serikali ni nzuri katika kuhakikisha jengo lile linatekelezwa kama lilivyodhamiriwa pale mwanzo.

Suala la *Prison Island*, tumesikia wazo lake. Kwa hiyo, naomba niseme tu kwamba serikali inathamini *asset* zake na kuna utaratibu maalum hivi sasa wa kuziorodhesha *asset* zote na Wizara ya Fedha na Mipango ndio inayoratibu masuala haya, kuorodhesha *asset* zake na kuweka matumizi na mpango bora wa matumizi wa *asset*.

Nam. 46

Changamoto Zinazoukabili Mfumo wa Elimu ya Maandalizi na Msingi

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:

Kwa kuwa, lengo la serikali yetu ni kutoa elimu bora na sio bora, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kupitia wataalamu wake ina wajibu wa kuupitia mfumo wa elimu uliopo hivi sasa kwa wanafunzi wa maandalizi na msingi unataka mwanafunzi wa maandalizi amalize akiwa na umri wa miaka 6, jambo ambalo mtoto huyu hutoka hapo akiwa hajui kitu kutokana na umri wake.

(a) Je, ni lini serikali itafanya upya mageuzi ya mfumo wa elimu ya maandalizi na msingi ambayo tunaendelea nao hivi sasa.

(b) Je, faida au hasara gani iliyopatikana kutokana na kutumia mfumo huu ambapo wazazi na walimu wanaona kwamba mfumo huu ni kikwazo kikubwa.

(c) Je, Wizara ya Elimu ilifanya utafiti kabla ya kuanza kwa mfumo huu katika nchi nyengine zikiwemo Tanzania Bara na Kenya ambao waliujaribu na baadae waliacha kuutumia kwa maslahi mapana ya kielimu kwa nchi zao.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam 46 lenye vifungu (a), (b) na (c). Kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kutokana na Sera ya Elimu ya mwaka 2006, imeanzisha mfumo wa elimu ambapo wanafunzi huaanza kusoma elimu ya maandalizi wakiwa na umri wa miaka minne kwa muda wa miaka miwili na kuanza elimu ya msingi kwa miaka sita kuanzia umri wa miaka 6 hadi 12 na elimu ya sekondari ya miaka minne kuanzia umri wa miaka 12 hadi miaka 16. Mfumo huo wa elimu umetokana na maoni ya wadau mbali mbali

na kupata uzoefu kutoka nchi nyengine. Faida na hasara ya mfumo wowote wa elimu hueleweka baada ya kufanyiwa tathmini.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Wizara imeunda kamati ya kufanya mapitio Sera ya Elimu ya Mwaka 2006, ambayo mfumo wa elimu ni mojawapo wa kipengele kimoja katika sera hiyo. Hivyo, wizara itafanya mabadiliko ya sera hiyo kulingana na maoni sahihi yatakayotolewa na wadau mbali mbali katika mikutano ya kukusanya maoni ya wadau inayoendelea kwa Unguja na Pemba.

(b) Mfumo huu una faida ya kumuwezesha mwanafunzi kumaliza muda wa elimu ya lazima kabla ya kuathiriwa na changamoto za ujana. Mfumo huu utawawezesha watoto wengi wa kike kukamilisha elimu ya lazima kabla ya kuingia katika ndoa za mapema. Hii itapelekea vile vile, mtoto kumaliza elimu ya juu katika umri mzuri wa kuweza kulitumikia taifa lake kwa muda mrefu kama nchi za wenzetu zilivyo ambapo wengi wanahitimu masomo ya shahada ya kwanza katika umri wa miaka kati ya 18 hadi 21. Hata hivyo, lengo la serikali ni kuwaendeleza vijana wake katika fani nyengine za ufundi kwa ambao wataishia elimu ya lazima, fani hizo ni pamoja na ushoni, umeme, upishi na useremala ambazo zitawasaidia kwenye soko ajira watakapohitimu.

(c) Wizara, ilifanya utafiti katika nchi mbali mbali ambazo zimebadilisha mifumo yao ya elimu. Baadhi ya nchi hizo ni pamoja na Ghana, Mauritus na Seychelles. Pia, hivi karibuni nchi za Kenya, Rwanda na Tanzania Bara nazo pia zimebadilisha mifumo yake ya elimu ambayo itawawezesha wanafunzi kuanza elimu ya msingi katika umri mdogo kuliko ilivyokuwa zamani ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri ambayo nashukuru kwa kukiri kwamba ameiona kwamba iko changamoto, lakini kwa kuwa izo nchi anaozozitaja kwanza tunatafauti nao kimaumbile hata ya watoto wetu na bado Tanzania Bara mpaka sasa hivi hawako na huwo mfumo wetu kama huo tulionao sie wa 4,6, 2,2 na wao wanawao na mwisho wa siku tunawafanya mtihani watoto wetu wa taifa kwa pamoja kwa Tanzania. Je, ni lini sera hiyo au watafiti hao wa hiyo sera watakamilisha ili waweze kuishauri vizuri wizara na wizara nayo iweze kwa maslahi mapana ya vijana wetu waweze kubadilisha mfumo huo wa elimu, ili uendeane na uhalisia wa vizazi vyetu au hawa watoto wetu tulionao kwa hivi sasa. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, ni kwamba juzi tu Ijumaa Kamati hii iloteuliwa ilimaliza kazi yake ya kuandaa ripoti ya awali, ripoti hiyo baadae italetwa kujadiliwa katika katika wadau wengine wa ngazi ya wizara, kisha baadae itakuja katika ngazi ya Wawakilishi na baadae itakwenda ngazi ya juu mpaka hatimae itapokuwa itakapokubalika na serikali.

Kwa hivyo, tunaweza kusema kwamba wakati wadau wote watakapomalizika ndio ripoti itapatikana, lakini ripoti sio lazima iwe kama unavyosema inawezekana wadau wakaona kwamba

mfumo uliopo sasa unafaa uwendelee utaendelea na ikiwa ripoti itaonesha kunahitaji mabadiliko yatafanywa ahsante sana.

Nam. 30

Kuchelewa Kutolea Vibali vya Ujenzi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Utaratibu wa utoaji vibali vya jenzi kutoka *DCU* hasa kwa wawekezaji umekuwa mgumu, unachelewa na urasimu kinyume na ilivyokuwa hapo awali, wakati vibali hivyo vinaratibiwa na *ZIPA* vilikuwa vikipatikana bila kuchelewa, mpaka hivi sasa karibu vibali saba vya miradi ya ujenzi ya wawekezaji havijatolewa.

(a) Je, kuna tatizo gani linalopelekea vibali vya ujenzi kucheleweshwa na *DCU* hasa kwenye miradi ya uwekezaji.

(b) Ule utaratibu wa kuweka kituo kimoja *(One Stop Center)* kupunguza urasimu umekwamia wapi katika upatikanaji wa vibali vya ujenzi.

(c) Kwa nini vibali hivyo vinacheleweshwa hatuoni kuwa tunawavunja moyo wawekezaji.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 30 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Kwanza, kwa uelewa wa Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati, Kamisheni ya Ardhi na Kitengo cha *DCU* hakuna utaratibu mgumu wa utoaji wa vibali. Taarifa kwamba hapo awali utaratibu ulikuwa mzuri na sasa ni mbaya si sahihi, vile vile. Suala la utoaji vibali linakwenda vizuri zaidi sasa kuliko hapo awali. Kwa kiasi kikubwa, *DCU* imefanikiwa kuweka utaratibu mzuri zaidi na ambao umeondosha changamoto nyingi zilizokuwepo. Ni ukweli kuwa kama taasisi mpya *DCU* bado inazo changamoto za utendaji, ufuatiliaji na usimamizi. Haya yanajulikana na yanafanyiwa kazi.

Aidha, wizara inataka kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kuwa katika mashindano ya kibiashara (*doing business*), suala la utoaji vibali ni kitu muhimu ni kiashiria kikubwa. Aidha, suala la utoaji vibali haliishii tu katika kutoa karatasi ya kibali, kunatakiwa kuwepo na ufuatiliaji wa kujua aliepewa kibali anatekeleza masharti ya kibali hicho. Haya yote yanafanywa vizuri zaidi katika mfumo wa sasa wa *DCU*, kuliko hapo awali.

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Hakuna tatizo la vibali kuchelewa. Vibali vyote vinatolewa ndani ya siku 14 kama utaratibu unavyoeleza.

(b) Suala la *One Stop Centre* ni la *ZIPA*, wao ndio wanaojua limefikia wapi. Wizara, inaelewa kuwa hivi sasa Kamisheni ya Ardhi na *DCU* zinaye mwakilishi wake ndani ya ofisi za *ZIPA* ambae anapatikana wakati wote.

(c) Zaidi, wizara inaelewa kuwa hadi hivi sasa hakuna ombi lolote la *ZIPA* ambalo liko ndani ya mikono ya *DCU*. Tunamuomba Mhe. Mjumbe kama anayo taarifa ya maombi ya vibali ambayo yako *DCU* na hayajapatiwa jawabu awasiliane na wizara sisi tutahakikisha kuwa suala hilo tunalitatua haraka.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa sana rafiki yangu Mhe. Naibu Waziri nilikuwa naomba sana ajaribu kufata nyayo za Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kabla ya kujibu swali afatilie mimi sifanyi kitu cha kubahatisha. Kwa kweli, majibu yake naomba uniruhusu Mhe. Spika, katika kitengo cha *DCU* hakuna utaratibu mgumu wa utoaji wa vibali taarifa ni kwamba hapo awali utaratibu ulikuwa mzuri na sasa ni mbaya si sahihi, umerekebishwa kama jana au juzi *ZIPA* wenyewe walikuwa wanakilio hichi kuna vibali karibu sita au vinane vimechukuwa mwaka mmoja na nusu leo unakuja kujibu kitu gani Mhe. Waziri hii Ramadhani. Lakini baada ya maelezo haya naomba niulize swali la nyongeza.

(a) Je, upo tayari kupokea watu wanaokabiliwa na matatizo hayo ya wawekezaji ambao wameamua kuekeza miradi wakiwa wanamatatizo ya vibali na lizi mpaka muda huu ninavyokwambia ni mtihani hazitoki.

(b) Je, ni lini Zanzibar itakuwa na kituo cha *One Stope Centre*, ili kuondowa matatizo haya na ukiona muwekezaji hawezi kuwa na *lease* hawezi kuekeza kuna ripoti ya *AIA* kwanza halafu apimiwe ardhi huoni ni uzembe wa watendaji wako huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, lakini kwanza naomba afahamu ninaposema kwamba *DCU* ndani ya siku 14, inatakiwa kibali ni sahihi lakini ina maana ya kwamba zile taratibu nyengine zote uwe tayari umekamilisha iwapo hujakamilisha zile taratibu nyengine kama michoro, na *plan* na mambo mengine ambao yanatakina kisheria inawezekana likachelewa na hivyo utaona ni zaidi ya siku 14.

a) Ni lini na nipo tayari kukutana na hao watu ambao anadai wamecheleweshwa. Kwa heshima naomba nimwambie niko tayari wakati wowote aje nao kwa ajili ya kuonana na hao watu.

b) Kama vile ambavyo nimesema suala la *One Stop Center* lipo Wizara ya Fedha na Mipango na imani yangu ni kwamba linaendelea vizuri lakini sisi kama Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati tunae mtu wa kudumu pale kwa sasa kwa ajili ya kurahisisha hiyo huduma ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Mhe. Naibu Waziri, naomba nitoe ufafanuzi kwenye suala hili la *One Stop Centre* ni kwamba

suala la *One Stop Centre* tayari serikali imesahafanya maamuzi na tayari hivi sasa maofisa wa zile sekta wote wameshawekwa chini ya *ZIPA* na huduma mbali mbali ikiwemo vifaa vimeshawekwa pale. Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi asiwe na wasi wasi *One Stop Centre* tayari imeanza kazi yake.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu Mhe. Spika.

Mhe. Hamida Abdalla Issa: Nakushkuru Mhe. Spika, kwa kuniona pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye (a), na (b). Kwa kuwa *DCU* ina utaratibu wa kushirikiana na Manispaa na Halmashauri kwenye utoaji wa vibali na sehemu ya malipo yake hutumika kwenye undeshaji pamoja na kuzigawia manispaa hizo swala

a) Je, utaratibu wa mgao wa pato la vibali ushaanza kuratibiwa.

b) Kama umeanza ni kiasi gani cha fedha kilichotolewa kwenye fidia kwa manispaa husika kwa mawaka wa fedha 2017 - 2018. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ni kwamba kweli tunashirikiana nao na kinachopatikana ni sehemu ya uendeshaji wa hiyo *DCU* kwa sababu *DCU*, miongoni mwa wajumbe wake ni hawa Wakurugenzi wa Halmashauri sasa sikufahamu tu kama aliposema fidia kwamba wapewe Halmashauri kwa lipi labda angefafanua vizuri lakini ninachokielewa ni kwamba kile ambacho kinakusanywa ni sehemu ya uendeshaji wa kazi za *DCU* ambayo wajumbe wake pia wanatoka huko Halmashauri.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, wakati wa maswali umekwisha kabla hatujenda kwenye hoja inayofuata naomba nitoe matangazo ya wageni walotufikia. Waheshimiwa Wajumbe, wageni wetu wa leo wa kwanza kabisa ni wageni wa Spika wa Baraza la Wawakilishi wageni wake, huyu wa kwanza ni Mhe. Laila Burhani Ngozi, huyu ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM. Lakini pamoja nae ameambatana na mumewe Ndugu Ramadhan Ali Kimara huyu ni katika lile kundi la G1 kama mnalifahamu karibuni sana Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Wageni wengine ni wageni wa Mhe. Masoud Abrahman Masoud Mwakilishi wa Jimbo la Bububu watoka Tawi la CCM Chemchem Bububu wageni hawa ni kama ifuatavyo:-

1. Ndugu Halima Twaha ni Mwenyekiti wa UWT kwenye hilo tawi, naomba usimame ahsante karibu. (*Makofi*)
2. Ndugu Fatma Faki Makame Katibu Mwenezi kwenye hilo tawi.
3. Ndugu Mwanahindu Khamis Katibu wa Tawi. Karibuni sana.

Wageni wanaofuata ni wageni wa Mhe. Mohamed Said Mohaamed Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae.

Wanamtandao wa safari ya CCM 2020 jumla yao ni wanne na naomba wasimame.

1. Ndg. Ruth Fabian Panhe
2. Ndg. Chiku Marzouk Ali
3. Ndg. Ahmeid Justin Mussa
4. Ndd. Mohamed Nassor Theney

Karibuni sana.

Wengine ni wanafunzi wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere *campus* ya Zanzibar wakiwa pamoja na viongozi wa Tawi la UVCCM chuoni hapo jumla yao ni saba wanaongozwa na Ndugu Haji Shekha Khamis pamoja na mwalimu wao Advert Chamz naomba musimame nyote kwa pamoja.

Karibu sana, matangazo ya wageni yamekwisha

Mhe. Spika: nimeona watu watatu Waheshimiwa Wajumbe nitaenda kwa mtu mmoja mmoja nitaanza na Mhe. Jaku Hashim Ayoub nitakuja kwa Mhe. Simai Mohammed Said halafu nitamalizia na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, nimesimamia Kanuni ya 63 (43) sijui nina haja ya kuisoma au nisipoteza muda, kauli ya serikali nisome...

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe endelea huna haja ya kuisomo tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, Alhamis au Ijumaa nilitaka kauli ya serikali lakini naona kauli haikupata alikaa Mwenyekiti akanambia serikali imesikia lakini vile vile Mhe. Spika hicho kitu hakileti taswira nzuri .....

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, kuhusu kitu gani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kuhusu hali ya barabara iliyoko pale kila mwaka Kiembesamaki inatengenezwa. Mhe. Spika, hana wewe ukaja humu tunakuonea huruma shida unayoipata pale barabara ilivyooza Kiembesamaki ni muda mrefu sasa hivi viongozi wakuu akiwepo Mhe. Balozi wetu anapata usumbufu wa pale, viongozi hata wageni wanaoingia katika nchi hii na kwa siku tunapokea karibu ndege tatu mpaka nne haileti taswira nzuri, angalau eneo lile tu kila mwaka lilikuwa likifanyiwa ukarabati sababu gani za msingi nataka muongozo wa kiti chako nilisema hapa lakini Mhe. Mwenyekiti akanambia serikali imesikia lakini *activity* yoyote iliyofanyika mpaka muda huu naomba muongozo wa kiti chako.

Mhe. Spika: Ahsante nimekusikia Mhe. Mjumbe. Mhe. Simai Mohammed Said na wewe.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, ahsante sana nasimama kwa kutumia Kanuni ya 42 (1) lakini lengo mimi kwanza sina lengo la kutaka majibu au hoja yangu ijadiliwe Baraza lako tuakhirishe lakini tuendelee na ratiba zetu kama zilivyo, lakini hoja yangu ni kwamba inafanana na Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi makini wa Jimbo la Paje ilikuwa ni hoja ni kwamba katika mvua hizi za masika maeneo mengi ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba hasa barabara

za mjini kumekuwa na mahandaki sio mashimo ni mahandaki sasa kwamba hata ukiingia hutoki unakwama.

Sasa, barabara hizi zimekuwa ni hatari pia kwa wananchi wetu hasa wanaotumia vyombo vya moto hasa ni lini kauli ya serikali tunaitaka ambayo halikadhalika kuhusiana majibu tutakayoyapata kwa barabara ambayo Mhe. Jaku Hashim Ayoub ametangulia ya Kiembesamaki na mimi naongeleza kwa barabara zote Unguja na Pemba juu ya mashimo au mahandaki haya sasa yaliokuwepo ni lini serikali itachukua hatua za haraka na niombe kwamba suala hili limewahi kugusiwa pia nafikiri na mheshimiwa kama sikosei Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Dimani juu ya mashimo ambayo yako katika barabara zetu.

Tukiangalia Baraza la Wawakilishi, Kiembesamaki, Mwanakwerekwe, barabara ya *Majestic* maeneo mengi kwa kweli Mhe. Spika, kwa hiyo mimi ningeomba tu kwamba tusijadili lakini tupate kauli ya serikali juu ya suala hili.

Nakushukuru sana Mhe. Spika kwa nafasi uliyonipa ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante sana. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: *Bismillah Rahman Rahim* Mhe. Spika, nimesimama hapa kwa kanuni ya 45, 46. 45 inayosema kwamba inayosema maelezo binafsi lakini 46 kuhusu fursa na haki za wajumbe.

Siku ya Ijumaa tulipokuwa tukichangia Wizara ya Kilimo, Maliasili na Mifugo Mwenyekiti aliokuwa akiendesha kiti kile kwa kweli anasikitisha sana na niliinuka na utaratibu, niliinuka na muongozo hakutaka kunipa wakati tunatumia kanuni ya Baraza la Wawakilishi na inaturuhusu mimi nilimchangia hoja ile kwa kusema na niliweka nikasema nazuwia shilingi na nilitaka maelezo Mhe. Waziri nimpongeze sana alitujibu majibu mazuri lakini kuna mambo mawili muhimu ya wananchi wangu wa Jimbo la Chaani alisahau kuyajibu wakati nilipokuwa nikisimama hakunipa fursa ile hata nafasi moja.

Sasa, naomba sana kwamba nafasi zinapopitshwa bajeti basi uwepo wewe mwenyewe Mhe. Spika au Mhe. Naibu Spika hawa ndio kwa sasa hivi wenye uzoefu wa kuendesha kiti chako, tunafahamu kwamba unawafundisha lakini kiti kinayumba sana na hawawezi kazi hiyo kabisa. Mhe. Spika, naomba sana muongozo wako na pindipo kama ataendelea hivyo siku zote tunaposimama nitakuja na Kanuni ya 123 ya kumpigia kura sina imani naye.

Mhe. Spika, naomba muongozo wa kiti chako.

Mhe. Spika: Ahsante, Waheshimia Wajumbe kwanza hili la Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Simai Mohammed Said ni vitu viwili ambavyo vimefanana. Mhe. Jaku kidogo alikuwa *specific* tu lakini Mhe. Simai yeye ame *cover* maeneo yote, hili tatizo kweli ni kubwa na waheshimiwa serikali nadhani imelisikia lakini labda nitampa Mhe. Waziri wa Fedha hapa kusaidia maneno machache tu kwa niaba ya serikali ili kwasababu tunajua na mvua hazijamalizika bado zipo, pengine wanategea zimalizike hizi mvua ili waweze kurekebisha.

Hili tatizo sio letu sisi tu lakini ni la wananchi wote lakini hata wao serikali ni miongoni mwetu sisi linawasumbua vile vile, kabla sijampa Mhe. Waziri wa Fedha nije kwenye hili la Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf siku hizi tuna utaratibu mnapokuwa mnachangia waheshimiwa pamoja na kwamba sote wachangiaji pamoja na tunaokaa kwenye hivi viti ni binadamu lakini tumewaelekeza makatibu mezani wawe wanaandika majina ya wale ambao wanatoa nia ya kuja kuzuwia vifungu, sasa mara nyingi sana Mwenyekiti anapokuwepo hapo anafanya *reference* kwenye yale majina ambayo yameandaliwa na makatibu inawezekana kwa bahati mbaya na wao wakapitikiwa wakawa hawasikia ile nia yako ya kuja kuziwia kifungu.

Kwa hiyo, mambo kama haya yanatokezea lakini ni kwa bahati mbaya tu lakini huwa si mwisho kwamba likishindikana tena jambo lako litakuwa limekwisha unakuwa bado unayo fursa zinapokuja zile wizara nyengine au uje ukae na mawaziri wanaohusika kuwaelezea, najua wengi mnataka mambo yenu wayasikie wananchi lakini bado una uwezo wa kukaa na mawaziri bila wananchi wako kukusikia jambo likatatuka hilo hilo ukamuelekeza waziri vizuri tu halafu akaweza kukutatulia hilo jambo. Baada ya hapo pamoja na maelezo yako sisi tunaoendesha hivi vitu tutajitahidi sana na wenyeviti tunazidi kuelimishana, ili tuhakikishe kwamba tunakuendesheni kama ambavyo kanuni zinahitaji.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Waziri wa Fedha nakuomba kidogo kwa niaba ya serikali maelezo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kutoa maelezo kutokana na masuala mawili yalioulizwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Simai Mohammed Said.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub yeye alikwenda *specific* kwenye barabara ya Kiembesamaki na nimueleze tu kwamba suala la mvua ni suala ambalo hatuwezi kulizuwia na kila mwaka mambo haya yanatokea na si kwetu tu lakini nchi zote ambapo yakitokea mvua kubwa basi uharibifu wa miundombinu inatokea na kwa wenzetu huwa inatokea kubwa zaidi Mwenyezi Mungu atuepushie balaa za namna hiyo.

Lakini kuna maeneo madaraja yanakatika, majumba yanaanguka kwa hili ni jambo la kawaida na kila mwaka yanapotokea haya serikali inachukua juhudi yakuirudisha hiyo hali kama ilivyokuwa mwanzo. Lakini kwa barabara ya Kiembesamaki serikali ya Dkt. Ali Mohamed Shein imeshalifanyia kazi suala hilo. Limeonekana serikalini limetafakariwa kwa kina kabisa na kujua nini kifanyike katika eneo lile lakini mwisho wa habari ilioneka ni lazima ujengwe mtaro unakayoyachukua maji yale na kufata njia ya asili ya kuyapeleka baharini. *(Makofi)*

Kutokana na kazi nzuri iliyofanyika iliyofanywa na wenzetu wa *CRJE* kupitia mradi wa *ZUSP* ilionekana kazi ile wapewe *CRJE* kwa kuongeza mkataba wa kazi yao ile nzuri waliyoifanya katika mitaro ya maeneo mengine, mkataba tayari umeshafungwa na Wizara ya Fedha na Mipango tayari imeshalipa asilimia 30. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wananchi watarajie kwamba hivi karibuni kazi ya ujenzi wa mtaro katika eneo lile litafanyika wako katika hatua ya ku *design* na kufuata ule mtiririko wa maji utakaokuwa rahisi zaidi na ufupi zaidi wa kupeleka baharini. Kwa hiyo, kazi *almost* imeshapata mkandarasi na *advance payment* ya *thirty percent* imeshalipwa kazi inatarajia kuanza wakati wowote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu kuharibika kwa barabara katika maeneo mengine. Serikali hivi sasa imeshafanya tathmini ya barabara zote na bajeti tayari imeshawasilishwa na wizara inayohusika, serikali inafanya mazingatio ya jinsi ya kupata fedha hizo kwa ajili ya matengenezo na nadhani miye mara baada ya kumalizika hizo mvua shughuli za kuzirejesha barabara hizo katika hali ya uhalisia wake itafanyika.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa maelezo yako mazuri.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Afya

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwanza nikuombe radhi kifua changu sio kizuri kwa muda wa wiki moja sasa.

Mhe. Spika, kufuatia taarifa ya bajeti ambayo iliwasilishwa katika kikao cha Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi ambayo imechambua bajeti ya Wizara ya Afya naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako likae kama Kamati ya Matumizi kwa madhumuini ya kupokea na kujadili na hatimaye kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Wizara ya Afya na vipao umbele vyake kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu muumba mbingu na ardhi kwa kutujaalia neema na uhao mzima tukaweza kukutana hapa leo sote tukiwa wazima na afya kwa nchi yetu ikiwa katika hali ya amali, utulifu na mshikamano.

Mhe. Spika, naomba nimshukuru kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa uongozi wake mahiri katika kuiongoza Zanzibar namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema, umri mrefu na ampe nguvu ya kuendelea kutuongoza kwa hekima na busara. Aidha nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuendelea kuipa kipao umbele Sekta ya Afya pamoja na kuhakikisha kwamba bajeti kwa ajili ya huduma za afya inaongezwa ili kuimarisha ubora ya huduma zinazotolewa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pongezi za pekee ziende kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi kwa kuweza kusimamia vyema utekelezaji wa shughuli za serikali, hotuba aliyoitao katika baraza lako wakati wa kuwasilisha hotuba yake ya bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 imetoa mwelekeo na dira ya utekelezaji wa shughuli za serikali kwa mwaka wa fedha ujao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nachukua fursa hii ya pekee kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuniamini na kuniteuwa kuwa kiongozi wa wizara hii ambayo ni muhimu ya maisha ya watu wetu, naahidi sitomuangusha naitumikia kwa juhudi zote namuomba Mwenyezi Mungu anisaidie. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nachukua fursa hii kukupongeza kwa dhati kabisa wewe mwenyewe binafsi kwa kutekeleza majukumu yako kwa uweledi katika kuliongoza Baraza hili.

Aidha nampongeza Mhe. Naibu Spika na Wenyeviti wawili wa baraza hili kwa kusimamia vyema mjadala wa Baraza wakati wa kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Ustati wa Jamii chini ya Mwenyekiti mahiri Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Dimani pamoja na wajumbe wake wote kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano mazuri waliotupa katika utekelezaji wa kazi za wizara kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na kupitia taarifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi, vipaumbe na malengo ya bajeti kwa mwaka 2018/2019.

Mhe. Spika, ushauri na maelekezo ya kamati hii yamesaidia katika kuandaa hotuba hii ambayo leo nawasilisha mbele ya Baraza hili. Wizara ya Afya inaendelea kuzingia maelekezo ya kamati wakati wa utekelezaji wa malengo kwa mwaka ujao wa fedha. Aidha napenda kuwashukuru Makatibu wa kamati hii pamoja na watendaji wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, pia niwapongeze wajumbe wote wa Baraza hili kwa michango na miongozo katika mijadala mbali mbali ambayo yamesaidia kuimarisha utendaji kazi katika kutoa huduma bora za za afya kwa wananchi wa Zanzibar. Wizara inamini kuwa wajumbe wa Baraza hili wanataendelea kutoa mashirikiano na miongozo ili lengo la kuwapatia wananchi kwa Zanzibar hii huduma bora za afya lifikikiwe.

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila nisipotoa shukrani za dhati kwa Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kwa kufanya kazi nzuri na kusimamia Ilani ya CCM na miongozo yote ya kiserikali katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za kila siku za Wizara ya Afya, namshukuru ameweka misingi mizuri ambayo imenirahisishia utekelezaji wa majukumu yangu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda kumshukuru Mhe. Haji Omar Kheir Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa ushirikiano wanaotupa katika kusimamia ugatuzi wa huduma ya afya ya msingi ni imani yetu kwamba chini ya uongozi wake huduma za afya za msingi zitaendelea kuimarika zaidi.

Mhe. Spika, kwa kuthamini juhudi za wanamichezo wa Zanzibar nachukukua fursa hii kuipongeza timu yetu ya Taifa ya Mipira wa Miguu *Zanzibar Heros* kwa kuonyesha umahiri katika mashindano ya *CECAFA* yaliofanyika nchini Kenya mwaka 2017 na kuwa washiriki nafasi ya pili, pia pongezi ziwaendee wachezaji na viongozi wa timu ya mpira ya ufukweni kwa kutwaa ubingwa wa mashinano hayo, tukumbuke kwamba michezo ni afya na ndio maana tunachukua nafasi hii kuwapongeza sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda kutowa mkono wa pole kwa wananchi wote walioathirika katika mafuriko ya mvua kubwa zinazoendelea kunyesha hapa nchi. Aidha, natoa pole kwa wale wote waliopoteza ndugu na jamaa na marafiki kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo maradhi, ajali na majanga katika mwaka wa fedha tuliomaliza pia namuomba Mwenyezi Mungu awape nafuu wagonjwa walioko hospitalini na walioko majumbani amin.

Baada ya kusema hayo sasa naomba nitoe maelezo ya utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi na

vipaoumbele vya wizara mwaka 2018/2019 mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Afya (Fungu H01) iliidhinishiwa jumla ya shilingi 72,936,229,000/=, kati ya hizo, shilingi 22,673,962,000/= ni kwa ajili ya mishahara na maposho; shilingi 14,300,000,000/= kwa matumizi ya uendeshaji; shilingi 533,400,000/= kwa ajili ya ruzuku. Aidha, shilingi 35,428,867,000/= kati ya hizo shilingi 10,906,000,000/= kutoka serikalini na shilingi 24,522,867,000/= kutoka kwa washirika wa maendeleo zote zilitengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi 2018, Wizara ya Afya imeingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 56,085,137,747/= sawa na asilimia 76.9 ya fedha zilizotengwa. Matumizi ya fedha hizo yameelezwa katika utekelezaji wa kila programu husika. Pia, Hospitali ya Mnazi Mmoja (Fungu H02) imeingiziwa shilingi 8,385,142,554/= sawa na asilimia 81.3 ya shilingi 10,380,579,000/= zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya hospitali. Kama kiambatisho namba 1 kinavyoonesha muhtasari wa mapato na matumizi kwa Fungu H01 na Fungu H02.

Mhe.Spika, Wizara ilipangiwa kukusanya mapato ya Shilingi 221,143,000/= ambapo hadi kufikia Machi 2018, shilingi 144,609,700/= sawa na asilimia 65.4 zimekusanywa. Aidha, Hospitali ya Mnazi Mmoja ilipangiwa kukusanya Shilingi 931,022,000/=, ambapo hadi kufikia Machi 2018, shilingi 375,910,687/= sawa na asilimia 40.4 zimekusanywa kama ilivyooneshwa katika Kiambatisho Namba 2.

MAFANIKIO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mhe. Spika, naomba nitumie fursa hii kuwaeleza wananchi baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha utekelezaji wa mwaka huu wa fedha, kama yafuatayo:-

i. Kuongezeka kwa wataalamu wa kada mbali mbali za afya wakiwemo madaktari (46), Wauguzi (170), Wafamasia (3) na Fundi Sanifu Maabara (34). Kwa jumla hadi kufikia April, 20 2018 Wizara ya Afya ina jumla ya madaktari 236 wakiwemo madaktari bingwa 30. Hivyo, inafanya kuwa na uwiano wa daktari mmoja kuhudumia watu 642 ikilinganishwa na Machi, 2017 ambapo daktari mmoja alihudumia watu 11,647. Kwa ukanda wa Afrika Mashariki Zanzibar ni ya tatu ikitambuliwa na Uganda na Kenya katika daktari mmoja kuwahudumia wananchi.

ii. Kupanuka kwa huduma za matibabu ikiwemo huduma za usafishaji wa figo na matibabu ya saratani;

iii. Kuimarika kwa huduma za uchunguzi ikiwemo kufungwa na kufanyakazi kwa mashine ya *MRI* na mashine za kidijitali za *X-ray;*

iv. Bodi ya Chakula na Dawa imepandishwa hadhi kuwa Wakala wa Serikali;

v. Maabara ya Wakala wa Chakula na Dawa imepata ithibati ya kimataifa ya ubora wa huduma;

vi. Kitengo cha Maradhi ya Ubongo na Uti wa mgongo kimepata ithibati ya Kikanda (*COSECSA*) kuwa kituo cha kufundishia madaktari bingwa wa maradhi hayo;

vii. Kuanzishwa kwa mfumo wa kielektroniki wa utoaji wa huduma za afya pamoja na uwekaji wa kumbukumbu (*EMR*);

viii. Kuwepo kwa mfumo wa mawasiliano ya tiba baina ya Hospitali ya Mnazi Mmoja na hospitali nyingine duniani (*Telemedicine*);

ix. Kuongezeka kwa upatikanaji wa dawa muhimu katika hospitali na vituo vya afya;

x. Kujengwa na kufanyiwa ukarabati mkubwa vituo vya afya 15;

xi. Kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Afya;

xii. Kufanya ukarabati mkubwa wa wodi ya zamani ya wazazi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja;

xiii. Kuongezeka kwa chanjo za watoto walio chini ya umri wa mwaka mmoja kutoka asilimia 75 mwaka 2016 hadi asilimia 84.4 mwaka 2017;

xiv. Kuanzishwa kwa chanjo mpya ya saratani ya shingo ya kizazi kwa watoto wa kike wenye umri wa miaka 9 -14; na

xv. Kuendelea kudhibiti maradhi ya malaria na maambukizi ya VVU/UKIMWI chini ya asilimia moja.

Mhe. Spika, mafanikio haya pamoja na mengine yaliyopatikana ambayo sikuyataja hapo juu yameelezewa kwa kina katika utekelezaji wa sekta kwa kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 kwa mujibu wa programu husika.

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU KWA KIPINDI CHA JULAI 2017 HADI MACHI 2018

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ilitekeleza program zifuatazo:-

i. Programu ya Kinga na Elimu ya Afya (PH0101);
ii. Programu ya Tiba (PH0102);
iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu (PH0103); na
iv. Programu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja (H02).

PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0101)

Mhe. Spika, programu hii inahusisha utoaji wa huduma za kinga na elimu ya afya zikiwemo huduma za afya ya mama na mtoto, huduma za kudhibiti VVU/UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma, huduma za Kumaliza Malaria Zanzibar, huduma za Lishe, Utoaji elimu ya Afya, Afya ya Mazingira, huduma za ufuatiliaji mienendo ya maradhi, Afya ya wafanyakazi, huduma za maradhi yasiyoambukiza, huduma za maradhi yasiyopewa kipaumbele *(Negleted Tropical Diseases- NTD)*, huduma za afya ya akili ya msingi, huduma za afya ya macho ya msingi na huduma za afya Bandarini na Uwanja wa Ndege.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, wizara ilitenga jumla ya shilingi 21,237,830,000/= kwa ajili ya Programu ya Huduma za Kinga na Elimu ya Afya. Hadi kufikia Machi 2018, jumla ya shilingi 15,022,451,964 /= (asilimia 70.7) zilitumika (Kiambatisho Namba 3).

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, programu ya Kinga na Elimu ya Afya ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendeleza kudhibiti maradhi ya kuambukiza, ikiwemo UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma pamoja na mpango wa kujima afya kwa hiari.
ii. Kuimarisha “Kampeni ya Kumaliza Malaria Zanzibar” kwa kuongeza kasi ya kufuatilia wagonjwa wanaogundulika na maradhi hayo;
iii. Kuanzisha utoaji wa chanjo ya kinga ya Saratani ya Shingo ya Kizazi kwa wasichana walio na umri wa miaka 14
iv. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi;
v. Kuimarisha huduma za elimu ya afya;
vi. Kuimarisha huduma za afya maskulini;
vii. Kuimarisha huduma kwa kudhibiti maradhi yasiyoambukiza ikiwemo uchunguzi wa kansa ya matiti, shingo ya uzazi na tezi dume;

Mhe. Spika, utekelezaji wa malengo haya ulifanyika kupitia huduma mbali mbali kama ifuatavyo:-

Huduma ya Kinga Dhidi ya Maradhi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma

Mhe. Spika, wizara imeweza kudhibiti maradhi ya UKIMWI ambapo kati ya watu 144,159 (wanawake 80,042 na wanaume 68,117) walichunguzwa asilimia 0.9 walionekana na virusi. Pia kati ya watu 215 ambao wamezaliwa na mama wenye maambukizi ya UKIMWI asilimia 2.8 walionekana kupata maambukizi.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwishoni mwa Machi 2018, wagonjwa 10,464 walisajiliwa kwenye kliniki 13 (Unguja 9 na Pemba 4) zinazotoa huduma za kinga na tiba kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Wagonjwa 8,191 (asilimia 78.3) walianzishiwa dawa za kupunguza makali ya VVU (*ARVs*). Jumla ya wagonjwa 5,538 wanaendelea na huduma; kati yao, wagonjwa 5,439 (asilimia 98.2) wanaendelea kutumia dawa za kupunguza makali ya VVU. Lengo la dunia la

asilimia 90 ya watu wanaojijua kuwa wanaishi na virusi vya UKIMWI kuanzishiwa dawa za *ARVs* limefikiwa. Sambamba na hayo, asilimia 66 ya watu wanaotumia dawa za kupunguza makali ya VVU wamepimwa wingi wa virusi vya UKIMWI.

Mhe. Spika, katika jitihada za kupunguza athari za dawa za kulevya, vijana 490 wanaotumia dawa za aina ya "*heroin*" wamesajiliwa kwenye kliniki ya "*Methadone*" iliyopo Hospitali ya Kidongo Chekundu kwa lengo la kupunguza uraibu. Kati yao, vijana 303 (asilimia 62.6) wanaendelea kupatiwa dawa hiyo, 166 wameacha dawa na 21 wamefariki hadi kufikia mwezi Machi 2018.

Mhe. Spika, kwa upande wa maradhi ya kifua kikuu wagonjwa 587 (Unguja 376 na Pemba 211) waligundulika kuambukizwa maradhi ya Kifua Kikuu, ambapo wawili (2) waligundulikana na Kifua Kikuu sugu *(MDR TB*) na tayari wameanzishiwa matibabu. Wagonjwa 584 (asilimia 99.5) walipimwa maambukizi ya virusi vya UKIMWI, ambapo wagonjwa 68 (asilimia 12) wamebainika kuwa na maambukizi. Aidha, asilimia 91.3 ya wagonjwa waliogundulika na Kifua Kikuu mwaka 2016/2017 wamepona maradhi hayo. Maelezo kamili yote hayo yako kwenye ukurasa wa 24 mpaka wa 30 wa hotuba yangu.

Mhe. Spika, wizara inaendelea kutekeleza mkakati wa kufanya ufuatiliaji wa jamaa na jirani ya wagonjwa wa Kifua Kikuu ili kuweza kuibua wagonjwa wapya. Jumla ya watu 942 ambao ni jamaa wa wagonjwa 282 walifuatiliwa na kuchunguzwa maradhi hayo, 94 walionekana kuwa na dalili za maradhi na 21 walithibitika kuwa na maradhi hayo. Katika zoezi hilo watoto 138 (Unguja 94 na Pemba 44) wenye umri chini ya miaka mitano (5) wamepatiwa dawa za kinga dhidi ya maradhi ya Kifua Kikuu.

Mhe. Spika, kwa upande wa huduma za maradhi ya Ukoma, jumla ya wagonjwa 52 (Unguja 37 na Pemba 15) waligundulika kuwa na ugonjwa huo, kati yao, wagonjwa 37 (asilimia 71) walikuwa na ukoma mpevu (mabaka mengi) na 15 (asilimia 29) walikuwa na ukoma hafifu (mabaka machache).

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi 2018, jumla ya wagonjwa 194 (wanawake 58 na wanaume 136) wanaoishi na virusi vya homa ya ini "B" (*Hepatitis "B")* walisajiliwa kwa ajili ya utafiti wa majaribio unaoendelea katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hadi sasa ni wagonjwa 10 ndio waliofikia vigezo na kuanzishiwa dawa za kupunguza makali ya virusi hivyo. Vigezo vinavyotumika katika kufikia kiwango cha kutumia dawa ni pamoja na wingi wa virusi na hali ya ini kufanya kazi.

Huduma za Kumaliza Malaria Zanzibar

Mhe. Spika, katika jitihada za kumaliza Malaria Zanzibar, wizara imechukuwa hatua mbali mbali katika kudhibiti maradhi hayo. Hatua hizo ni pamoja na uhamasishaji jamii juu ya matumizi ya vyandarua vyenye dawa, uchunguzi pamoja na matumizi ya tiba sahihi ya Malaria. Jumla ya wagonjwa 394,766 walichunguzwa ambapo 1,657 (asilimia 0.4) walionekana kuwa na vimelea vya malaria. Wagonjwa 1,481 (asilimia 89.4) walifuatiliwa majumbani ndani ya saa 48 kwa kufanyiwa uchunguzi zaidi. Wagonjwa wote waliogundulika na Malaria walitibiwa kwa

dawa ya safu ya kwanza kama muongozo unavyoeleza. Katika kipindi hicho mgonjwa mmoja alifariki dunia kutokana na Malaria.

Mhe. Spika, juhudi mbali mbali zinaendelea kuchukuliwa ikiwemo kutoa elimu ya afya kwa jamii ili kumaliza tatizo hili. Hivyo, kwa kutumia vyombo vya habari, vipindi 26 (asilimia 92.9) kati ya 28 vilivyopangwa vya redio na televisheni vilirushwa kupitia *ZBC, Zenj FM*, redio Mtegani na ya Micheweni. Vile vile vipeperushi, elimu ya malaria katika skuli na njia nyengine mbali mbali zilitumika katika kutoa elimu kwa jamii.

Mhe. Spika, upigaji wa dawa majumbani umefanyika katika maeneo maalum ambayo yameonekana kutoa wagonjwa wengi wa malaria katika Wilaya za Magharibi "A", Magharibi "B", Kati, Kusini, Kaskazini "A", Kaskazini "B", Chake Chake, Wete na Micheweni. Jumla ya nyumba 63,672 zilipangwa kupigwa dawa, hadi mwisho wa zoezi nyumba 67,971 (zaidi ya asilimia 100) zilipigwa dawa. Mafanikio hayo ni makubwa ukilinganisha na shabaha iliyowekwa na Shirika la Afya Duniani ambalo linasisitiza angalau asilimia 85 ya nyumba zote ziwe zimepigwa dawa. Maelezo ya kina yanapatikana katika ukurasa wa 31 hadi 33.

Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto

Mhe. Spika, katika mwaka 2017 wajawazito 61,981 sawa na asilimia 91 ya lengo walihudhuria katika kliniki za mama na watoto angalau mara moja kabla ya kujifungua. Hata hivyo, wengi wa mama hao hufika kliniki wakiwa wanakaribia kujifungua jambo ambalo linapelekea kutokamilisha muda wa mahudhurio yaliyopendekezwa (mara nne kwa kila mimba) hivyo, kukosa huduma muhimu za kutambulika matatizo ya ujauzito huo. Kiutaratibu, mama mjamzito anatakiwa ahudhurie kliniki kuanzia wiki ya 12-14 ya ujauzito kwa hudhurio la kwanza, wiki ya 20-24 kwa hudhurio la pili, wiki 28-32 kwa hudhurio la tatu na wiki ya 36 kwa hudhurio la nne. Takwimu zinaonesha ni asilimia 24 tu ya wajawazito ndio wanahudhuria kliniki chini ya wiki 16 ya mimba kama inavyopendekezwa. Wizara inaiomba jamii isaidie kuwahamasisha mama wajawazito kuhudhuria kliniki mapema kuanzia wiki ya 12 ya ujauzito.

Mhe. Spika, uhamasishaji wa wajawazito kujifungulia katika hospitali umeendelea kufanyika kupitia watoa huduma za afya wa kujitolea, wafanyakazi wa vituo vya afya, mikutano ya kijamii na kupitia katika vipindi mbali mbali vya redio na televisheni. Hadi kufikia Machi 2018, wajawazito 29,637 walijifungua katika hospitali na vituo vya afya ya msingi vya daraja la pili (hospitali/vituo vya afya vya Serikali 28,344 na hospitali za binafsi 1,293). Kati yao, wazazi 27,275 walijifungua kwa njia ya kawaida na wazazi 2,362 (asilimia 8) walijifungua kwa upasuaji (Kiambatisho Namba 4). *WHO standard* kwa mujibu wa vile viwango vya *WHO* upasuaji wa asilimia 5 mpaka 10 hapo inaonekana mnafanya vizuri. Kwa hospitali za serikali tuna asilimia 7.2 na *private hospital* ni asilimia 24.1. Kwa hiyo, bado serikali inatoa huduma nzuri zaidi kuliko *private hospital*.

Mhe. Spika, huduma za mama baada ya kujifungua ziliendelea katika vituo vyote vya afya. Hata hivyo, mahudhurio ya mama katika kliniki baada ya kujifungulia ni madogo. Nitoe wito kwa Waheshimiwa Wawakilishi kwa nafasi zao na ushawishi mkubwa walionao katika jamii, kuendelea kuwaelimisha wananchi, hususan wazazi, umuhimu wa kuhudhuria katika kliniki kwa mujibu wa maelekezo ya wataalamu ndani ya kipindi cha siku 42 baada ya kujifungua.

Mhe. Spika, wizara ina utaratibu wa kufuatilia sababu ya kila kifo kinachotokana na uzazi na vifo vya watoto wachanga ili kuweza kuchukuwa hatua stahiki. Mhe. Spika, kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Machi, 2018; jumla ya mama 58 wamefariki dunia kutokana na matatizo ya uzazi katika hospitali. Miongoni mwa sababu zilizogundulika kupelekea vifo hivyo ni zile zinazotokana na jamii ikiwemo kuchelewa kufika hospitali. Aidha, sababu nyengine ni zile za kiafya ambazo ni kifafa cha mimba, kupasuka kwa fuko la uzazi, kupoteza damu nyingi na maambukizi wakati na baada ya kujifungua. Matatizo mengi ya vifo vya uzazi yangeweza kupungua kwa asilimia 30 kama kina mama watahudhuria kliniki kwa mapema na vile vile baada ya kujifungua wataweza kufika kwenye kliniki zetu.

Mhe. Spika, shughuli za chanjo za watoto chini ya umri wa miaka mitano na wanawake wenye umri wa kuzaa (miaka 15-49) na wajawazito ziliendelea vizuri kwa vituo vyote vya afya Unguja na Pemba. Mhe. Spika, takwimu za chanjo zinaonesha kuwa asilimia 84.4 ya watoto walio chini ya mwaka mmoja walipata chanjo ya *PENTA* 3 kwa mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 78 mwaka 2016. Kiambatisho namba 5 kinatoa ufafanuzi wa hali ya chanjo kwa wilaya.

Mhe. Spika, mbali ya kuhakikisha chanjo zinapatikana wakati wote, wizara imekuwa ikichukuwa hatua kadhaa kuimarisha huduma hii. Hatua hizo ni pamoja na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa watoa huduma za chanjo na utoaji wa mafunzo kwa watoa huduma katika vituo vya afya na watoa huduma wa kujitolea ambao huwatafuta wale waliokatiza chanjo. Aidha, watoto 18 wenye umri chini ya miaka 15 ambao wamepata ulemavu wa ghafla wamefatiliwa na kuchunguzwa; hata hivyo, hawakugundulika na virusi vya ugonjwa wa Polio.

Mhe. Spika, katika hotuba ya mwaka jana, wizara iliahidi kuanzisha chanjo mpya dhidi ya ugonjwa wa saratani ya shingo ya kizazi kwa wasichana wa miaka 9 -14. Napenda kulijulisha Baraza hili tukufu na wananchi wote kuwa chanjo hiyo imeshaanzishwa na kuzinduliwa rasmi tarehe 10/4/2018 na Mhe. Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mwanamwema Shein alizindua kampeni hiyo. Naomba kumpongeza sana kwa kazi nzuri aliyoifanya Uzinduzi wa chanjo hiyo umeenda sambamba na ushajihishaji jamii, viongozi wa Wilaya, Mikoa, Taifa na watendaji kutoka vituo vya afya. Utoaji wa chanjo hiyo ni muendelezo wa chanjo zinazotolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa wananchi wake kwa nia ya kuyadhibiti maradhi yanayoweza kukingika. Ni matumaini yangu kuwa Waheshimiwa Wawakilishi mtaendelea kuhamasisha jamii kuwaruhusu watoto wa kike wenye umri wa miaka 9-14 katika majimbo yenu kufika katika vituo vya uchanjaji vilivyowekwa maalumu kwa utoaji wa huduma hizo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, huduma za uzazi wa mpango zimeendelea kutolewa katika vituo vya afya na kupitia huduma za mikoba. Jumla ya wateja wapya 19,885 walipatiwa huduma hizo kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Machi, 2018. Mafunzo ya wiki mbili kwa watendaji 50 (Unguja 25 na Pemba 25) yalifanyika ili waweze kutoa huduma za uzazi wa mpango kwa kutumia njia za muda mrefu. Hata hivyo, utumiaji wa njia za uzazi wa mpango bado uko chini, ambapo hadi hivi sasa ni asilimia 14 tu ya akina mama wenye umri wa kuzaa ndio wanaotumia huduma hizi na lengo ni kufikia lengo ikiwa ni kufikia asilimia 20 ifikapo 2022. Maelezo kamili yanapatikana kwenye paragraph 34 mpaka 43 ya hotuba yangu.

Mhe. Spika, huduma rafiki kwa vijana zimeendelea kutolewa katika vituo saba (7) viliopo Unguja na Pemba, ambapo wateja 1,422 walihudumiwa. Kituo kipya cha huduma hiyo

kinaendelea kujengwa katika maeneo ya Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA*). Kukamilika kwa kituo hicho kutatoa fursa kwa kundi kubwa la vijana wanaosoma katika chuo hicho kupata huduma hizo, ikiwemo uchunguzi wa VVU, huduma za uzazi wa mpango na elimu ya afya.

Mhe. Spika, katika hatua za kukinga maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, wajawazito 57,660 (asilimia 93) walichunguzwa afya zao katika kliniki za mama wajawazito na wodi za wazazi katika mwaka 2017. Akina mama 149 waligundulika kuwa na VVU, hivyo walipewa dawa za kupunguza makali ya VVU (*ARV*). Aidha, kati ya wenza wa mama wajawazito 6,410 waliopimwa VVU, 24 waligundulika kuwa na maambukizi ya virusi.

Huduma za Kupambana na Maradhi yasiyoambukiza (*NCD*)

Mhe. Spika, Wizara inatambua ongezeko la maradhi yasioambukiza kwa miaka ya hivi karibuni. Utafiti uliofanywa kwenye jamii mwaka 2017 umeonesha kwamba kati ya watu 2,106 waliochunguzwa; asilimia 7.5 wanasumbuliwa na maradhi ya kisukari, asilimia 36 wanasumbuliwa na shindikizo la damu (Presha) na asilimia 23.3 wana uzito uliokithiri. Hivyo, juhudi mbali mbali zimekuwa zikichukuliwa katika kudhibiti ongezeko hilo ikiwemo kutekeleza mkakati wa miaka mitano ambao umejikita katika kutoa elimu ya afya juu ya vichocheo vya maradhi hayo na kushajihisha jamii juu ya ufanyaji wa mazoezi.

Mhe. Spika, jumla ya mama wajawazito na watu wazima 702 (wanawake 582 na wanaume 120) wamepatiwa elimu juu ya kujikinga na maradhi ya kisukari na umuhimu wa lishe. Mafunzo hayo yamefanyika katika vituo vitano (5) vya afya vya KMKM, Fuoni, Mpendae, Sebleni na Magogoni. Sambamba na hayo, watendaji wa vituo vya afya wanao utaratibu wa kutoa elimu ya afya kwa kuzingatia mada mbali mbali ikiwemo maradhi yasiyoambukiza.

Mhe. Spika, matumizi ya tumbaku yamekuwa yakipigwa vita duniani kote kutokana na athari za kiafya zinazotokana na zao hilo. Hivyo, katika kuhakikisha kunakuwepo na udhibiti wa matumizi ya tumbaku, kanuni maalum zilizotayarishwa zimezinduliwa mwezi wa Julai 2017. Uzinduzi huu ulienda sambamba na utoaji wa mafunzo kwa waandishi wa habari na wadau wengine. Jumla ya waandishi wa habari 55 wa vyombo tofauti, maafisa wa Baraza la Mji na Polisi walishiriki mafunzo hayo. Pia, viongozi 30 wa Serikali na Taasisi mbali mbali walipatiwa uelewa juu ya umuhimu wa kanuni hizi ili waweze kuzifanyia kazi.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya kwa mashirikiano na "*Tanzania Dental Association*" ya Dar-es-Salaam imeendesha huduma za ukaguzi wa kinywa na meno katika kituo cha Afya Rahaleo. Katika ukaguzi huo, jumla ya wananchi 300 walijitokeza na waliogundulika kuwa na matatizo walipatiwa ushauri na matibabu stahiki. Vile vile, wanafunzi 2,089 wa skuli za msingi 33 Unguja na Pemba walifanyiwa uchunguzi wa maradhi ya moyo, kinywa na meno. Matokeo yameonyesha kwamba wanafunzi 18 wana matatizo ya moyo, 519 utandu wa meno, 253 matatizo ya ufizi na 607 uzito mdogo. Ushauri na tiba ilitolewa kwa waliopatikana na matatizo mbali mbali ya kiafya.

Huduma za Kupambana na Kichocho, Minyoo na Matende

Mhe. Spika, wizara imepiga hatua nzuri katika kudhibiti maradhi ya Kichocho. Utafiti uliofanywa mwaka 2017 umeonesha kwamba kiwango cha maradhi haya kimepungua kutoka asilimia 3.4 mwaka 2016 hadi asilimia 1.7 (2017). Licha ya kupunguwa huko, bado yapo maeneo yenye maambukizi makubwa yakiwemo Mwera, Chaani, Bandamaji, Kinyasini na Makoba kwa Unguja na Pemba ni Vitongoji, Kinyasini, Kiuyu Minungwini na Uwandani.

Mhe. Spika, Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, jumla ya wagonjwa 273 wa maradhi ya kichocho na 69 wa maradhi ya matende walipatiwa matibabu. Tathmini ya zoezi la ulishaji dawa kwa mzunguko wa 11 imefanyika mwezi wa Septemba 2017, ambapo matokeo yameonesha asilimia 91.5 ya wananchi wamekula dawa za minyoo, lengo ni kufikia asilimia 95.

Huduma za Lishe

Mhe. Spika, wizara imeendesha zoezi la ugawaji wa matone ya vitamin A na dawa za minyoo kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano mara mbili kwa mwaka, kwa lengo la kuwaongezea kinga ya maradhi mbali mbali. Katika zoezi lililofanyika mwezi wa Disemba 2017, watoto 206,202 wa umri wa miezi 6-59 walilengwa kupatiwa matone ya Vitamini A ambapo matokeo yameonesha kuwa watoto 202,055 sawa na asilimia 98 walipatiwa matone hayo. Kwa upande wa utoaji dawa za minyoo watoto 183,453 wenye umri kati ya mwaka mmoja hadi miezi 59 walitarajiwa kupatiwa dawa za minyoo. Hadi mwisho wa zoezi asilimia 97.9 walipatiwa dawa hizo. Katika zoezi lililofanyika mwezi Juni 2017 asilimia 95.5 ya waliokadiriwa walipatiwa matone ya Vitamini A na asilimia 96.1 walipatiwa dawa za minyoo. Kwa ujumla wastani wa waliopatiwa dawa hizo umeongezeka ikilinganishwa na miaka iliyopita. Kiambatisho namba 6 kinatoa ufafanuzi kwa kila Wilaya.

Mhe. Spika, wizara imeendelea kuhamasisha jamii juu ya matumizi ya chumvi yenye madini joto. Jumla ya kilo 200 za madini joto zimegawiwa kwa wazalishaji wa chumvi kisiwani Pemba. Sampuli 89,075 za chumvi zilichukuliwa kutoka katika maduka kuchunguzwa uwepo wa madini joto. Uchunguzi huo umegundua asilimia 33 ya sampuli za chumvi zilizochunguzwa hazikuwa na madini joto; hivyo, wazalishaji wa chumvi na wauzaji walielimishwa kuhakikisha chumvi wanayozalisha au kuuza imewekewa madini joto.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, watoto 1,238 walibainika kuwa na utapiamlo mkali. Aidha, tafiti zinaonesha kuwa bado wapo watoto wengi wenye utapiamlo ambao hawahudhurii hospitali au vituo vya afya kwa kupatiwa matibabu. Wizara inawaomba wananchi kuwapa watoto lishe bora yenye virutubisho vinavyojenga mwili ili kuwakinga na utapiamlo. Aidha, watoto ambao hali zao ni mbaya kutokana na utapiamlo mkali, Wizara inashauri wapelekwe katika hospitali na vituo vya afya vilivyo karibu. Ni lazima tutambuwe watoto wenye afya bora ndio mtaji wa nguvu kazi ya taifa.

Huduma za Afya Bandarini

Mhe. Spika, Wizara ya Afya imeendelea kuvifanyia ukaguzi vyombo vya usafiri kupitia Bandarini na Uwanja wa ndege, ili kudhibiti maradhi. Hadi kufikia Machi 2018, vyombo vya

usafiri baharini vilifanyiwa ukaguzi mara 2,127; ambapo meli kubwa mara 99, meli za kitalii mara 10, vyombo vidogo vidogo mara 458 na boti za kawaida za abiria zilifanyiwa ukaguzi mara 1,560. Meli 10 zilifukizwa kutokana na athari za kiafya zilizobainika. Aidha, ukaguzi wa makontena 45 ya nguo, makontena 76 ya friji na makontena manne (4) ya viatu umefanyika. Jumla ya kilo 85 za nguo zimechomwa moto baada ya kuonekana hazifai kwa matumizi ya binadamu.

Mhe. Spika, jumla ya abiria 470,306 wanaoingia nchini kupitia bandarini na uwanja wa ndege walifanyiwa ukaguzi wa kiafya. Kati yao, abiria 284,300 ilibainika kuwa wamechanjwa na abiria 186,006 hawakuchanjwa. Abiria 65 walioonekana kwamba wanastahiki kuchanjwa walipatiwa chanjo kwa mujibu wa taratibu. Wananchi 2,209 waliohitaji kusafiri nje ya nchi walipatiwa huduma za chanjo, ambapo wasafiri 1,733 walipatiwa chanjo ya homa ya manjano, 416 homa ya uti wa mgongo na wasafiri 60 walichanjwa chanjo ya Homa ya Ini "B".

Mhe. Spika, jumla ya wagonjwa 75 na maiti 77 waliopitishwa Bandarini na Uwanja wa ndege walikaguliwa, wagonjwa 6 walibainika kuwa na malaria na waliosalia hawakuwa na maradhi ya kuambukiza. Ukaguzi wa taarifa za maiti ulionesha vifo vyao vilisababishwa na ugonjwa wa presha, saratani, sukari, moyo pamoja na ajali.

Huduma ya Afya ya Mazingira

Mhe. Spika, kazi ya ufuatiliaji wa usalama wa maji ili kujikinga na maradhi ya miripuko imeendelea kufanyika, sampuli 13 kutoka katika visima vya maji vya jamii zilichunguzwa. Kati ya sampuli hizo, tano zimegundulika kuwa na vimelea vya maradhi ambapo hatua za kutibu zilichukuliwa. Sambamba na hilo, jumla ya vidonge 2,972,800 vya dawa za kutibu maji viligawiwa kwa wananchi wenye visima na matangi ya maji.

Mhe. Spika, nchi yetu imekuwa ikishuhudia mripuko wa maradhi ya kipindupindu kwa miaka mitatu mfululizo iliyopita kila baada ya mvua za masika na kusababisha vifo na athari za kiuchumi. Kwa kutambua hilo, Wizara kwa kushirikiana na Wakala wa Maji Zanzibar (*ZAWA*); Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali; Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati; Mabaraza ya Manispaa na Serikali za Mikoa; Idara ya Udhibiti wa Mazingira (ZEMA); na Mamlaka ya Utalii Zanzibar; jumuiya zisizokuwa za kiserikali (Msalaba Mwekundu na Jumuiya za kidini na kijamii -*CBOs*) pamoja na wadau wa maendeleo (*WHO, UNICEF*, *Ivo de Carneri* na *JICA*) imeandaa imeandaa Mpango Mkakati wa miaka mitano (5) wa kuondoa maradhi hayo, shughuli inayoratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambapo Wizara ya Afya ni mtekelezaji mkuu. Maelezo kamili yanapatikana kwenye *paragraph* 44 mpaka 68.

Mhe. Spika, mpango huo una lengo la kuweka mazingira wezeshi ili kutokomeza maradhi ya Kipindupindu. Mikakati iliyopendekezwa katika mpango huo inajumuisha uimarishaji wa mfumo wa ufatiliaji na kujiweka tayari dhidi ya mripuko; uimarishaji wa Elimu ya Afya na Mbadiliko ya tabia katika jamii, uimarishaji wa upatikanaji wa usafi na usalama wa Maji na mazingira, utoaji wa matibabu sahihi ya wagonjwa ikiwemo chanjo ya Kipindupindu.

Mhe. Spika, skuli nne (4) za sekondari na 132 za msingi (74 za Unguja 58 za Pemba) zilikaguliwa na kutolewa elimu ya afya iliyohusu matumizi sahihi ya choo pamoja na unawaji wa mikono. Takriban wanafunzi 40 kwa kila Skuli kutoka madarasa tofauti walipatiwa mafunzo hayo. Wauza vyakula 305 wamekaguliwa, kati yao, 14 walizuiliwa kuendelea na biashara kutokana na kutozingatia masharti ya usafi katika maeneo wanayofanyia biashara.

Mhe. Spika, jumla ya makaazi 5,672 yamekaguliwa, ambapo 4,700 katika Shehia 35 za Manispaa ya Mjini, 137 kwa Manispaa ya Magharibi "A" na 835 Manispaa ya Magharibi "B". Shughuli nyengine zilizofanyika ni pamoja na kutoa mafunzo kwa maafisa wa afya na wananchi katika Shehia za Kijini na Mbuyutende Matemwe, Wilaya ya Kaskazini 'A' na wafanyakazi wa afya wa kujitolea 79 kutoka katika Wilaya za Magharibi 'A' na 'B' na Micheweni. Mafunzo hayo yalihusu mikakati ya kuishajihisha jamii kujenga na kutumia vyoo.

Huduma za Ufuatiliaji wa Mienendo ya Maradhi

Mhe. Spika, wizara imeendelea kufuatilia mienendo ya maradhi ya kuambukiza kutoka katika vituo vya afya kwa kila wiki na hatimae kutoa tahadhari juu ya maradhi yanayoibuka ndani na nje ya nchi, ili kujiandaa kwa kuyakabili maradhi hayo. Kuanzia Julai 2017 hadi Machi 2018, jumla ya wagonjwa 6,104 waliripotiwa kuugua; kati yao, 1,239 wameugua homa ya viungo, 4,140 kuharisha, 340 homa ya matumbo, 28 surua, 173 tetekuanga, mmoja (1) homa ya uti wa mgongo na 183 wametafunwa na mbwa.

Huduma za Elimu ya Afya

Mhe. Spika, wizara kuelimisha na kuhamasisha jamii juu ya kutunza afya zao dhidi ya magonjwa, ikiwemo kufanya uchunguzi wa afya mara kwa mara na kujenga tabia inayozingatia kanuni za afya. Jumla ya vipindi 48 vya elimu ya afya vilirushwa hewani kupitia redio na televisheni za Serikali na za binafsi. Mada kuu zilizotolewa ni pamoja na utayarishaji wa maji safi na salama; usafi wa mazingira hususan kinga juu ya maradhi ya kipindupindu; uzazi salama ikiwemo kujifungulia hospitali; umuhimu na faida za unyonyeshaji wa ziwa la mama; na umuhimu wa chanjo ikiwemo chanjo mpya ya kinga dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi.

Mhe. Spika, kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara imezifikia jumla ya skuli 164 za Serikali na binafsi zilizopo katika wilaya mbali mbali za Unguja na Pemba. Takriban wanafunzi 21,000 walipatiwa elimu juu ya kinga dhidi ya maradhi mbali mbali ya miripuko ikiwemo namna ya kunawa mikono.

Mhe. Spika, mikutano ya shehia 22 za Unguja na Pemba ilifanyika yenye lengo la kutathmini shughuli za elimu ya afya katika ngazi za shehia. Katika mikutano hiyo wanajamii 4,300 kutoka katika kamati za afya za shehia, kamati za maendeleo za shehia, viongozi wa dini na wahudumu wa afya wakujitolea walihudhuria.

Huduma za Afya ya Wafanyakazi

Mhe. Spika, jumla ya wafanyakazi 17,266 wamechunguzwa afya zao, ambapo 745 walibainika na matatizo mbali mbali ya kiafya. Aidha, rasimu ya Muongozo wa Afya ya Wafanyakazi imetayarishwa na hivi sasa upo katika hatua za kupokea michango ya wahusika.

Huduma ya Msingi ya Afya ya Macho

Mhe. Spika, katika kuimarisha huduma za macho iliendesha huduma za masafa katika vijiji tisa (9) na jumla ya watu 5,103 walipatiwa huduma hizo. Vijiji hivyo ni Vumba, Mjini Tumbatu, Kiungani, Mbuzini, Uzini, Ukongoroni, Matemwe, Uroa na Chwaka.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, jumla ya watu 24,446 (wanawake 12,773 na wanaume 11,673) walifanyiwa uchunguzi wa macho; kati yao, watu 14,936 wameonekana kuwa na tatizo la macho tongo; 192 wameonekana kuwa na tatizo la mtoto wa jicho; 2,738 waliogundulika na maumivu na uvimbe kutokana na ajali na wengine waligundulika na matatizo mbali mbali ya macho. Aidha, watu 700 walifanyiwa upasuaji wa macho.

Huduma za Afya ya Akili ya msingi

Mhe. Spika, huduma za afya ya akili zimeendelea kutolewa kupitia hospitali na huduma za afya ya masafa. Huduma hizi zimetolewa katika hospitali zote za Vijiji na Wilaya kwa Unguja na Pemba. Jumla ya ziara 22 zilifanyika, ambapo wagonjwa 388 (wanawake 188 na wanaume 200) wenye matatizo ya afya ya akili walipatiwa huduma karibu na maeneo wanayoishi. Katika kuengeza uelewa juu ya afya ya akili, elimu ya afya ilitolewa kwa jamii wakati wa maadhimisho ya siku ya afya ya akili ambapo, skuli za Wilaya ya Kaskazini A na Kusini Unguja zilipatiwa elimu ya afya ya akili na dawa za kulevya. Kongamano na waganga wa jadi lilifanyika, ambapo waganga wa jadi 27 walihudhuria kongamano hilo, lengo ni kuelimishana juu ya afya ya akili.

PROGRAMU YA HUDUMA ZA TIBA (PH0102)

Mhe. Spika, programu ya huduma za Tiba imegawika katika programu ndogo mbili ambazo ni;

a) Programu ndogo ya huduma za uchunguzi inayohusisha shughuli za:-
   i. Huduma za udhibiti wa Kemikali, Chakula, Dawa na Vipodozi; na
   ii. Huduma za uchunguzi wa Maabara na Mionzi.

b) Programu ndogo ya huduma za matibabu ambayo inajumuisha:
   i. Huduma za Upatikanaji, utunzaji na usambazaji wa dawa; na
   ii. Huduma za Mpango wa Damu salama.

Programu hii pia, inahusisha Bodi na Mabaraza mbali mbali ambayo ni:- Bodi ya Madaktari, Bodi ya Ushauri ya Hospitali Binafsi, Bodi ya Afya ya Jamii na Mazingira, Bodi ya Wakala wa Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Bodi ya Wakala wa Chakula na Dawa, Bodi ya Afya ya Akili, Baraza la Wauguzi na Wakunga na Ofisi ya Muuguzi Mkuu Kiongozi. Pia, programu hii

inatekeleza Mradi wa Kupandisha hadhi Hospitali za Vijiji kuwa za Wilaya na Wilaya kuwa za Mkoa. Lengo la program hii ni kuimarisha utoaji wa huduma bora za afya.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/18, Wizara ilitenga jumla ya shilingi 35,177,366,000/= kwa ajili ya Programu ya Huduma za Tiba. Hadi kufikia Machi 2018, jumla ya shilingi 22,540,543,270/= (asilimia 100.5) kutoka serikalini na shilingi 8,102,716,678/= sawa na asilimia 63.6 kutoka zilitumika.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2017/18, katika Programu ya Huduma za Tiba wizara ilijiwekea malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha upatikanaji wa dawa muhimu kwa mujibu wa muongozo uliopo (*essential medicines list*), vifaa tiba, "*reagents*" na vifaa vya uchunguzi wa huduma za mionzi (*Radiology*);
ii. Kuimarisha mfumo wa rufaa wa wagonjwa katika ngazi tofauti;
iii. Kununua vifaa vya uchunguzi (ikiwemo mashine ya *DNA*);
iv. Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi;
v. Kutayarisha Sheria ya Maabara;
vi. Kukamilisha ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali;
vii. Kujenga nyumba za madaktari katika Hospitali ya Abdalla Mzee;
viii. Kujenga jengo la wodi za watoto na wajawazito katika Hospitali za Kivunge na Makunduchi;
ix. Kuanza matayarisho ya ujenzi wa Hospitali ya Binguni kwa kufanya uchambuzi yakinifu;
x. Kufanya ukarabati wa Hospitali ya Chake Chake; na
xi. Kuimarisha huduma za tiba asili na tiba mbadala.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, jumla ya mahudhurio ya wagonjwa wa nje 295,974 (wanawake 166,002 na wanaume 129,972) yaliripotiwa katika hospitali za serikali. Vile vile, wagonjwa 54,997 (wanawake 41,901 na wanaume 13,096) walilazwa katika hospitali hizo, ambapo wagonjwa 1,217 wamefariki dunia (Kiambatisho Namba 7 mpaka 8). Aidha, jumla ya wagonjwa 5,009 walifanyiwa upasuaji mkubwa wa aina mbali mbali. Kiambatisho Namba 8 kinaonesha aina na idadi ya waliofanyiwa upasuaji kwa kila hospitali.

Mhe. Spika, jumla ya wagonjwa 271 walisafirishwa nje ya Tanzania kwa matibabu zaidi. Kati yao, watoto 30 wamepelekwa kwa upasuaji wa moyo nchi Israel na 241 walipelekwa India kwa matatizo mbali mbali. Hadi kufikia Machi, 2018, Jumla ya shilingi bilioni 6.9 zilitumika kulipia gharama za matibabu na usafiri ambapo bajeti kwa huduma hii ilikisia bilioni moja tu na badala yake tukatumia *OC* yetu kuweza kuwasafirisha watu kwenda nje.

Mhe. Spika, wizara imeendelea kuimarisha huduma za uchunguzi wa Maabara na mionzi katika hospitali katika hospitali za Unguja na Pemba. Mashine mpya za "*Ultrasound*" na "*X-ray*" zimepelekwa katika Hospitali za Kivunge na Hospitali ya Micheweni imepatiwa mashine mpya ya "*Ultrasound*". Hadi Machi 2018, jumla ya vipimo 139,110 vilichunguzwa. Kiambatisho Namba 9 kinaonesha aina na idadi ya vipimo kwa hospitali.

Mhe. Spika, Hospitali ya Chake-Chake imeendesha kambi nne (4) za matibabu kwa mashirikiano na madaktari kutoka ndani na nje ya nchi. Jumla ya wagonjwa 1,396 walihudumiwa (wanawake 524 na wanaume 872). Kwa upande wa vifaa hospitali imepokea mashine ya kufulia nguo na kukaushia, kitanda cha upasuaji na taa ya chumba cha upasuaji. Vifaa vingine ni vitanda 22 na magodoro pamoja na "*oxygen concentrator*".

Mhe. Spika, ili kuimarisha uhifadhi na uwepo wa damu salama, "*panel*" za umeme wa jua na friji kubwa limewekwa katika chumba cha maabara katika hospitali ya Micheweni. Aidha, upanuzi na ukarabati mkubwa wa vyumba viwili ambavyo vitatumika kwa ajili ya huduma za uchunguzi na matibabu ya UKIMWI na Kifua Kikuu umefanyika. Kituo cha Mkono kwa Mkono ambacho ujenzi wake ulioanza mwaka jana umekamilika kufunguliwa rasmi. Vifaa kadhaa, vimepelekwa vikiwemo "*oxygen concentrator*", kitanda cha upasuaji, taa ya chumba cha upasuaji, mashine ya nusu kaputi, mashine ya kutakasia vifaa, frigi na vifaa tofauti vya upasuaji. Jengo la huduma za watoto njiti katika Hospitali ya Makunduchi limefanyiwa matengenezo. Vile vile, vifaa mbali mbali vya tiba na uchunguzi vimewekwa katika hospitali hiyo.

Mhe. Spika, katika kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na "*reagents*" wizara imeingia Mkataba na Bohari Kuu ya Dawa (*MSD*) ya Dar-es-Salaam kwa lengo la kuwa na mashirikiano katika ununuzi, ambapo zinanunuliwa kwa pamoja kutoka kiwandani. Hii imepunguza kiasi kikubwa cha gharama za kuagizia dawa. Aidha, dawa ambazo hazipatikani *MSD* ununuzi unafanyika kwa kupitia mfumo wa "*Framework Contract*" kwa Wazabuni ambao Wizara imeingia nao Mkataba.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Afya iliidhinishiwa shilingi 7,000,000,000/= kwa ajili ununuzi dawa na vifaa tiba. Hadi kufikia Machi 2018, dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi 8,088,631,879/= (shilingi 4,803,783,857/= kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi 3,284,848,022/= Wahisani wa Maendeleo) Kiambatisho namba 10 kinatoa ufafanuzi huo. Naomba sana nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake ambao umeiwezesha wizara kuhakikisha kuwa inapata dawa muhimu na wananchi wanapata huduma ya kupata dawa bila ya kulipia gharama yoyote. Nataka tumshukuru sana Mhe. Rais.

Mhe. Spika, shughuli za usambazaji dawa katika vituo na hospitali zimefanyika ambapo zaidi ya asilimia 95 ya maombi yalishughulikiwa kwa wakati. Ufanisi wa kazi za usambazaji wa dawa kwa wakati umeimarika baada ya kupata lori moja la kusambazia dawa na gari moja ndogo kwa kazi za kiofisi. Aidha, mafunzo ya wafamasia wa Wilaya juu ya ujazaji wa taarifa na maombi ya dawa (*Report and Request*) kwa kutumia mfumo wa kielektroniki yamesaidia kuleta ufanisi katika mfumo wa uombaji dawa.

Mhe. Spika, hatua za kujenga Bohari ya dawa kisiwani Pemba zimeanza kwa mashirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na *Global Fund*. Usarifu wa jengo na makisio ya ujenzi tayari yameandaliwa na taratibu za kumpata mkandarasi zinaendelea.

Mhe. Spika, kikao cha Baraza hili cha tarehe 21 Februari, 2017 kilipitisha marekebisho ya Sheria ya Bodi wa Chakula, Dawa na Vipodozi kuwa Wakala wa Chakula na Dawa. Napenda kuwajuilisha Wajumbe wa Baraza hili kuwa sheria hiyo mpya nambari 3 ya mwaka 2017

imeanza kazi. Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala ya Chakula na Dawa ameshateuliwa na Bodi imeundwa na imeanza kufanya kazi.

Mhe. Spika, miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni kufanikisha upatikanaji wa ithibati ya kimataifa kulingana na kiwango cha kimataifa cha *ISO* 9001:2015. Pia, wakala imezindua mfumo wa utendaji kazi wa kieletroniki ambao utarahisisha mawasiliano baina ya Wakala na wafanya biashara. Aidha, *ZFDA* imeingia mkataba na Taasisi ya Chakula na Dawa ya Tanzania (*TFDA*) ili kushirikiana katika shughuli ya utendaji kazi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuondoa baadhi ya kero za wafanya biashara. Maamuzi yatakayotolewa hapa na maamuzi yatakayotolewa na *TFDA* yatakuwa yanaheshimika bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Spika, Wakala wa Chakula na Dawa imeweza kukagua jumla ya maeneo 1,429 (asilimia 97.6) kati ya maeneo 1,464 ya biashara za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba yaliyolengwa. Matokeo ya ukaguzi huo, yalipelekea kuyafunga maeneo 4 kwa kutokidhi viwango na tani 569.38 za mchele usiofaa kwa matumizi ya binadamu zimekamatwa, ambapo tani 74.89 zimeteketezwa, tani 58.05 zimerejeshwa zilikotoka, tani 28.44 zinasubiri kuangamizwa na tani 408 zinasubiri kurejeshwa nchi zilizotoka baada ya kukamilika taratibu za kisheria.

Mhe. Spika, shughuli za ukaguzi wa viwanda vya nje ya Zanzibar zilifanyika kwa lengo la kuhakikisha ubora wa bidhaa zinazozalishwa na kuingia nchini. Jumla ya viwanda vya dawa 13 (Uturuki - 5, India - 3, China - 2, Poland - 2 na kimoja Pakistani) vilikaguliwa; kiwanda kimoja cha Uturuki hakikukidhi viwango. Mpango Uwiyano wa Usajili wa Dawa kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kushiriki ukaguzi wa pamoja kwenye viwanda vya dawa (Joint GMP Inspection) umeendelea kutekelezwa. Jumla ya viwanda viwili (2) vimekaguliwa na dawa 8 zimefanyiwa tathmini.

Mhe. Spika, maeneo ya biashara 1,013 (asilimia 69.2 ya lengo) yalisajiliwa. Maeneo hayo ni ya uzalishaji wa bidhaa za chakula (621), dawa (308), vipodozi (83) na vifaa tiba (1). Kwa upande wa usajili wa bidhaa, jumla ya aina 51 ya bidhaa zimesajiliwa baada ya kukidhi viwango, bidhaa hizo ni Chakula (40), dawa (8) na "*reagents*" (3). Aidha, sampuli 1,053 (792 za chakula, 233 za dawa, 26 za vipodozi na 2 za dawa za mitishamba) zilifanyiwa uchunguzi. Kati ya hizo, sampuli 17 za chakula zilionekana hazifai kwa matumizi ya binadamu.

Mhe. Spika, wizara kupitia Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imefanya uchunguzi wa vielelezo mbali mbali. Hadi kufikia Machi 2018, vielelezo 804 kutoka Jeshi la Polisi, taasisi mbali mbali na watu binafsi vilichunguzwa. Ufafanuzi wa uchunguzi huo unaonekana katika Kiambatisho Namba 11. Usajili wa wajasiriamali, wazalishaji na wasafirishaji wa kemikali umefanyika, ambapo vibali vya kuingiza kemikali 717 nchini vimetolewa.

Mhe. Spika, katika kuimarisha huduma za Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Wizara imekamilisha ujenzi wa jengo la Maabara na sasa ipo katika hatua za ununuzi wa samani na vifaa vya maabara. Mkataba wa ununuzi wa mashine ya uchunguzi wa vinasaba (*DNA*) tayari umesainiwa, mzabuni anategemewa kuleta na kufunga mashine hiyo ndani ya robo ya kwanza ya mwaka ujao wa fedha.

Huduma za Mpango wa Damu Salama

Mhe. Spika, katika kuhakikisha upatikanaji wa damu salama, wizara kupitia Kitengo cha Damu Salama imeendelea kukusanya, kuchunguza, kuhifadhi na kusambaza damu katika hospitali. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, jumla ya uniti 11,527 za damu zilikusanywa ambazo ni zaidi ya asilimia 100 ya lengo la mwaka la kukusanya uniti 10,800. Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyingine imeendesha mabonanza ya uchangiaji damu ili kuhakikisha inakuwepo damu ya kutosha katika mwezi mtukufu wa Ramadhan. Kiambatisho Namba 12 kinaonesha uniti za damu zilizokusanywa hadi Mei 2018.

Napenda kuwashukuru wale wote walioandaa bonanza, waliochangia na wananchi wote wakiwemo wana michezo, vikosi vya ulinzi na usalama, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kushiriki katika zoezi la uchangiaji damu hususan kwa mwezi wa Ramadhani ambapo mahitaji ya unit 1,250 yalizidi na tukakusanya unit 1,700. Nawapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Maelezo ya utekelezaji wa huduma za hospitali binafsi na utaratibu wa wauguzi na wakunga na huduma za tiba za asili zinapatikana katika hotuba yangu ukurasa wa 92 mpaka 97.

Mhe. Spika, kupitia Baraza hili napenda kuchukuwa fursa hii kuwashukuru walioshirikiana na Wizara katika mabonanza hayo pamoja wananchi wote wanaojitolea kuchangia damu. Aidha, nitoe rai kwa wananchi wachangie damu ili kuokoa maisha ya wagonjwa hasa wajawazito na watoto.

Mhe. Spika, jengo jipya la ofisi za damu salama lililoko Wete limezinduliwa rasmi sambamba na uwekaji wa vifaa vya ukusanyaji damu. Aidha, kituo kimefanikiwa kuwa na mfumo wa taarifa za ukusanyaji, upimaji na usambazaji damu wa kielektroniki, mfumo ambao unaimarisha uwekaji na upatikanaji wa taarifa za damu.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba programu inahusisha shughuli za Bodi na Mabaraza yaliyomo ndani ya Wizara. Hivyo, naomba nitoe maelezo ya utekelezaji wa huduma za taasisi hizi kama ifuatavyo:-

Huduma za Usimamizi wa Hospitali Binafsi

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi 2018, maombi matano (5) ya kufungua vituo na hospitali yalipokelewa; moja (1) la hospitali ya kulaza wagonjwa, matatu (3) vituo vya kawaida na moja (1) kliniki ya huduma za meno. Maombi yote hayo yalikubaliwa baada ya kukidhi vigezo na kupewa usajili. Kwa ujumla vituo na hospitali binafsi 112 Unguja na Pemba vimepatiwa usajili na kutambuliwa rasmi.

Mhe. Spika, ukaguzi ulifanyika katika vituo na hospitali 72; vituo 22 vilisimamishwa kwa muda kutokana na kasoro zilizobainika. Vituo vitatu (3), kimoja Unguja na viwili Pemba, vimefutiwa usajili kutokana na kutokidhi masharti na vituo 14 vilipewa barua za onyo. Pia, mtu mmoja amekamatwa kwa kutoa huduma bila ya usajili, ambapo hatua za kisheria zinaendelea.

Huduma za Uratibu wa Wauguzi na Wakunga

Mhe. Spika, Baraza la Wauguzi na Wakunga limesajili na kuwapa leseni wauguzi 514. Jumla ya malalamiko mawili (2) ya utendaji kazi wa wauguzi yaliwasilishwa kwa maandishi katika Baraza. Malalamiko hayo yalifanyiwa uchunguzi na wahusika kupewa barua ya onyo kwa mujibu wa sheria ya baraza. Katika kuimarisha hadhi na taswira ya Uuguzi kwa jamii, vipindi vinne vya televisheni vilirushwa kwa ajili ya kuelimisha jamii juu ya shughuli za uuguzi na baraza kwa ujumla.

Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala

Mhe. Spika, Baraza la Tiba Asili na Mbadala limesajili waganga 35, wasaidizi waganga 27, kliniki 7, maduka ya dawa matano (5) na vilinge 23. Aidha, Baraza linaendelea kuelimisha jamii juu ya kutumia dawa zilizo na viwango na kuwataka waganga wa tiba asili kufuata masharti yaliyowekwa. Jumla ya makosa matano (5) ya uvunjaji wa sheria yaliripotiwa; kosa la kuvunja miiko na maadili ya taaluma ya tiba asili ambapo mhusika mmoja amefungiwa kutoa huduma kwa kipindi cha mwaka mmoja, mwengine ametozwa faini ya shilingi laki moja na wengine watatu dawa zao zilitaifishwa. Hukumu zote hizo zilitolewa kwa mujibu wa Sheria ya Tiba Asili namba 8 ya mwaka 2008.

Huduma za Baraza la Madaktari

Mhe. Spika, kwa mwaka wa Fedha 2017/2018 Baraza la Madaktari limesajili na kuwapa leseni Madaktari (232) wakiwemo Madaktari Bingwa (3), Daktari Bingwa wa Kinywa (1), Madaktari wa kawaida (102), Madaktari wasaidizi (3), Daktari msaidizi wa Kinywa (1), Afisa Tabibu (105) na Afisa Tabibu Kinywa (17). Aidha, Baraza limepokea lalamiko moja la daktari kuvunja maadili, daktari huyo amesimamishwa kutoa huduma kupisha uchunguzi.

Mhe. Spika, rasimu ya Sheria mpya ya Madaktari Tiba na Madaktari wa Meno imeandaliwa na inategemewa kuwasilishwa katika ngazi husika. Aidha, muongozo wa Madaktari wa mafunzo ya vitendo (*Internship*) katika Hospitali za kufundishia umetayarishwa na umeanza kutumika.

Mradi wa Kupandisha Hadhi Hospitali za Vijiji kuwa za Wilaya na Wilaya kuwa za Mkoa

Mhe. Spika, mradi huu unahusika na ujenzi na ukarabati wa majengo ya hospital za Wete, Micheweni, Chake Chake, Vitongoji, Abdalla Mzee, Kivunge na Makunduchi. Ujenzi wa jengo la ghorofa mbili litakalokuwa na wodi ya wazazi, huduma za watoto na chumba cha upasuaji katika Hospital ya Kivunge umeanza. Maandalizi ya ujenzi wa paa la Hospitali ya Chake Chake yamekamilika, mkandarasi anatarajiwa kuanza kazi hivi karibuni. Aidha, ukamilishaji wa ukamilishaji wa nyumba ya madaktari katika Hospitali ya Makunduchi unaendelea na uko katika hatua za mwisho.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba ya bajeti ya mwaka jana kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina azma ya kujenga nyumba za Madaktari katika Hospitali ya Abdalla Mzee. Napenda kuliarifu baraza kwamba hatua za awali za michoro ya nyumba nne (moja ya

ghorofa nne na 3 za ghorofa 3) zimekamilika. Jumla ya shilingi bilioni 2 zimetengwa kutoka serikalini kwa mwaka wa fedha 2018/19 na fedha nyengine zitachangiwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China naomba tuwapongeze sana ndugu zetu hawa wamekuwa bega kwa bega na sisi.

Mhe. Spika, wakati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akizindua Baraza la Nane la Baraza la Wawakilishi, Novemba 11, 2010 alisema naomba kunukuu.

"Hospitali zilizo katika kiwango cha '*Cottage'* za Micheweni na Vitongoji Pemba na Makunduchi na Kivunge Unguja, nazo zitapandishwa daraja, ili zifikie hadhi ya kiwango cha hospitali za wilaya". Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Wizara, imeendelea kutekeleza agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar, ambapo hatua zifuatazo zimefikiwa kwa Hospitali za Kivunge na Makunduchi, kuna viwango maalum zifikiwe, ili hospitali hizo ziweze kuwa za Wilaya au Mikoa.

i. Wapo wafanyakazi wa kukidhi kuwa hospitali ya wilaya;
ii. Zina huduma za kutosha za kulaza wagonjwa;
iii. Vyumba vya upasuaji (*theatres*) vipo katika hali nzuri, kila hospitali ina mashine ya kutoa nusu kaputi; zinaweza kufanya upasuaji wa dharura;
iv. Zinapata mgao wa dawa unaokidhi mahitaji ya hospitali ya wilaya;
v. Zinatoa huduma zote za uzazi ikiwemo upasuaji wakati wa kujifungua;
vi. Zinatoa huduma za uchunguzi na matibabu ya meno;
vii. Kila hospital ina *generator* la dharura;
viii. Zipo huduma za uchunguzi wa Maabara na *X-ray;*
ix. Zina majiko ya kuchomea taka hatarishi za hospitali (*incinerators*); na
x. Gari za kusafirishia wagonjwa (*ambulance*) katika kila hospitali.

Hivi ni viwango kwa mujibu wa *WHO* ziwepo ili hospitali iweze kuwa ya wilaya au mkoa.

Mhe. Spika, kwa vigezo nilivyoviainisha hapo juu, napenda kulitaarifu Baraza kwamba hospitali hizi zimekidhi kuwa na hadhi ya Hospitali za Wilaya. Hatua zinazoendelea kuchukuliwa hivi sasa ni kuifanya hospitali ya Kivunge kuwa ya Mkoa.

Mhe. Spika, wizara imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma katika Hospitali ya Abdalla Mzee kwa kupeleka wataalamu wa afya hadi kufikia 115 wakiwemo Madaktari 26, Afisa Tabibu 4, Wauguzi 55, Wataalamu wa Mionzi 4, Fundi sanifu Dawa 8 na Fundi sanifu Maabara 14. Taarifa za mahudhurio ya wagonjwa zinaonekana katika *Kiambatisho Namba 7.* Jumla ya operesheni 525 zimefanyika katika kipindi cha Julai 2017 – Machi 2018. Aina za upasuaji mkubwa zinaonekana *Kiambatisho Namba 8.*

Mhe. Spika, zoezi la upembuzi yakinifu la ujenzi wa hospitali ya Binguni linaendelea. Uhakiki wa eneo umefanyika na kuzungushwa nguzo katika mipaka yote pamoja na kuwekwa mabango kila baada ya mita 100 yanayoonesha umiliki wa eneo hilo. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na mazungumzo na nchi za Falme za Kiarabu, Oman, Kuwait, Saudi na Badea ili

kuangalia uwezekano wa kugharamia ujenzi wa hospitali hiyo. Maeelezo kamili yanapatikana katika ukurasa wa 69 - 103.

PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA AFYA (PH0103)

Mhe. Spika, Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Afya inatekeleza majukumu yake kupitia programu ndogo tatu, ambazo ni:-

i. Uongozi na Utawala;
ii Sera, Mipango na Utafiti; na
iii Uratibu wa Shughuli za Afya Pemba.

Mhe. Spika, katika kuimarishauendeshaji na uratibu wa Wizara ya Afya, wizara katika mwaka wa fedha 2017/2018, ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kukamilisha mchakato wa uanzishwaji wa Bima ya Afya Zanzibar;
ii. Kufanya mapitio ya mfuko wa fedha kwa timu za Afya ili uendane na mpango wa ugatuzi wa madaraka;
iii. Kuendelea kuimarisha mfumo wa taarifa za afya na uibuaji wa tafiti za afya na zinazohusiana a afya;
iv. Kupitia na kutengeneza miongozo ya kisera ya utoaji wa huduma za afya;
v. Kuimarisha nguvu kazi hususan kusomesha madaktari bingwa;
vi. Kufanya marekebisho ya sheria mbali mbali ikiwemo Sheria ya kuendesha hospitali za binafsi na sheria ya madaktari;
vii. Kuanzisha rasmi zoezi la upimaji wa ufanisi wa wafanyakazi kwa ngazi zote Unguja na Pemba;
viii Kufanya ukarabati mkubwa wa jengo la huduma za macho; na
ix. Ujenzi wa wodi ya wagonjwa wa akili katika Hospitali ya Kidongo Chekundu

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ilitenga jumla ya Shilingi 16,521,033,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Afya. Hadi kufikia Machi 2018, jumla ya Shilingi 10,310,707,136/= (asilimia 62.4) zilitumika.

Programu ndogo ya Uongozi na Utawala (*PH010301*)

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara imeajiri jumla ya wafanyakazi 435; kati yao, madaktari (*46),* Wafamasia (3), Wakemia (9), Wauguzi (170), Fundi Sanifu Dawa (25), Afisa Tabibu (57) na Afisa wa Afya ya Mazingira (21), Afisa Tabibu Meno (10), Viungo Bandia (2), Fundi Sanifu Maabara (34), Wataalamu wa Mionzi (3), Maafisa Tehama (11), na 44 kwa kada nyengine mbali mbali. Jumla ya wafanyakazi 110 wamerejea kutoka masomoni.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, wizara imepeleka masomoni wafanyakazi 17 kusomea udaktari bingwa ndani na nje ya nchi, idadi hii inafanya kuwa na madaktari bingwa walioko masomoni kufikia 50**.** Kati yao, madaktari bingwa 13 wamepelekwa nchini Misri na 8 nchini Cuba. Miongoni mwa fani wanazosomea ni pamoja na maradhi ya Mkojo (Urology), Ngozi (*Dermatology*), Ganzi na usingizi (*Anaesthesiology*), Saratani (*Surgical Oncology*),

maradhi ya kina mama (*Obstetrics & Gynecology*), Mishipa ya fahamu *(Neuro-surgery)*, Maradhi ya watoto (*Pediatric*), Mionzi (*Radio-Diagnostic*), Maabara (*Pathology, Haematology na Forensic Medicine*) na Mifupa (*Orthopedic*). Vile vile, Madaktari (71) na Wauguzi (103), Maofisa wa Ganzi na Usingizi (13) na Maofisa wa Mionzi (6) wanaendelea na masomo.

Mhe. Spika, jumla ya wafanyakazi 47 (13 Unguja na 34 Pemba) wamestaafu kwa kutimiza muda wa utumishi. Wafanyakazi 74 wamefukuzwa kazi kwa sababu za kinidhamu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na 15 wapo likizo bila ya malipo. Aidha, wafanyakazi 15 wamefariki dunia, Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema Peponi, Amin.

Mhe. Spika, wizara imeendelea kushughulikia upatikanaji wa maslahi, stahiki na kusimamia nidhamu za wafanyakazi. Jumla ya wafanyakazi 700 wamelipwa malimbikizo ya posho la likizo. Aidha, ukarabati wa majengo ya wizara ikiwemo ofisi ya kuhifadhia nyaraka za Wizara umefanyika. Pia, zoezi la uhakiki wa mali (*assets*) zinazomilikiwa na Wizara zikiwemo nyumba za wafanyakazi, hospitali, vituo vya afya, gari, vyombo vya moto vya maringi mawili, viwanja na vifaa mbali mbali linaendelea.

Programu Ndogo ya Sera, Mipango na Utafiti (*PH010302*)

Mhe. Spika, wizara imefanya mapitio ya Kitita cha utoaji wa huduma za afya katika ngazi ya msingi (*Essential Primary Health Care Package*) ambacho kinafafanua aina ya huduma zinazostahiki kutolewa katika ngazi hiyo. Katika mapitio hayo, baadhi ya huduma zimeongezwa katika ngazi ya msingi daraja la pili (*PHCU +*) ikiwemo huduma ya *"ultra-sound"* na maradhi yasiyoambukiza. Pia, katika kila vituo imependekezwa awepo fundi sanifu dawa ili kuimarisha upatikanaji na udhibiti wa dawa. Aidha, huduma za afya ya msingi zisimamiwe tokea ngazi ya kaya.

Mhe. Spika, muongozo kwa ajili ya kutayarisha mpango kazi wa mwaka 2018/2019 umeandaliwa, ambapo watendaji 85 kutoka katika timu za afya za Wilaya, miradi na vitengo vyote vya wizara wamepatiwa mafunzo ya muongozo huo. Katika hatua nyengine, wafanyakazi wa afya 80 kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba wamejengewa uwezo wa kupanga mipango yenye kuleta matokeo kwa kutumia mfumo wa *"Bottleneck Analysis".*

Mhe. Spika, Wizara ya Afya imetengeneza mfumo wa kielektoniki ambao utaweza kukusanya taarifa za mama wajawazito (*Ante Natal Care tracking System*), mfumo huu unamuezesha mama majamzito kupata taarifa ya kuhudhuria kliniki na elimu mbali mbali kuhusiana na ujauzito wake kupitia simu yake ya mkononi. Vile vile, mfumo wa kukusanya taarifa za afya kutoka katika jamii (*Community Health Information System*) umeandaliwa. Katika kuhakikisha mifumo hiyo inafanya kazi kwa ufanisi, Wizara imepeleka komputa 200 katika vituo vya afya Unguja na Pemba vikiwemo baadhi ya vituo vya binafsi vinavyotoa huduma za mama wajawazito.

Mhe. Spika, katika kuimarisha mifumo ya upatikanaji takwimu, wizara imeanzisha mfumo wa kielektroniki wa kukusanya taarifa za wagonjwa katika hospitali za Mnazi Mmoja, Mwembe ladu, Kidongo Chekundu, Kivunge na Makunduchi kwa Unguja na Wete, Micheweni, Chake Chake, Vitongoji na Abdalla Mzee kwa Pemba. Mfumo huu unategemewa kuanza kutumika rasmi katika mwaka ujao wa fedha 2018/2019.

Mhe. Spika, jumla ya vituo vya afya 124 vilifanyiwa uhakiki wa taarifa za afya katika robo ya kwanza ya na vituo 68 katika robo ya pili. Halikadhalika, maafisa viungo 28 wamejengewa uwezo wa namna ya kufanya ufuatiliaji na tathmini katika idara na vitengo.

Mhe. Spika, ripoti za utekelezaji zimetayarishwa zikiwemo utekelezaji kwa mwaka 2016/2017 (*Annual Health Sector Performance Report - AHSPR*), ripoti za taarifa za afya (*Bulletin* 2015 na 2016) zimekamilika na kuchapishwa. Vile vile, Jarida la Afya toleo namba 2 limetayarishwa na kusambazwa kwa wananchi.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya ugatuzi wa huduma za afya ya msingi katika serikali za mitaa kuanzia mwaka huu wa bajeti. Wizara ya Afya ikiwa ni miongoni mwa Wizara zilizohusika na ugatuzi imefanya mapitio ya mkataba wa mfuko wa afya (*Health Basket Fund*) ili kwenda sambamba na mabadiliko hayo. Vikao vya pamoja baina ya Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ vya kujadili utekelezaji wa ugatuzi vimefanyika. Wizara tayari imekabidhi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ nyaraka husima, mishahara ya wafanyakazi na orodha ya majengo (Vituo vya Afya na Nyumba za Wafanyakazi) na vivaa vikiwemo magari, pikipiki, samani na kadhalika.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kwamba huduma za *"lift"* katika Hospitali ya Mnazi Mmoja zinapatikana muda wote, wizara imeamua kununua "lift" moja mpya ambayo itagharamu Shilingi 229,000,000/= ndani ya mwaka huu wa fedha unaomalizika. Taratibu za ununuzi zimekamilika ikiwemo kusainiwa kwa mkataba na kampuni ya "*ORTIS*" ambayo "*lift*" hiyo itanunuliwa. Ni imani ya wizara kwamba kupatikana kwa "*lift*" hiyo kutapunguza kero iliyokuwa inawakabili wananchi, zile mbili ambazo zilikuwa mbovu moja inafanya kazi na hii mpya itafika hivi karibuni.

Mhe. Spika, katika kuimarisha shughuli za tafiti za afya Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha Taasisi ya Utafiti wa Afya (*Zanzibar Health Research Institute - ZAHRI*). Lengo la taasisi hii ni kufanya tafiti ambazo zitasaidia kupata matokea chanya yatayokayoweza kustawisha afya ya jamii na kuimarisha utoaji wa huduma. Aidha, matokeo ya tafiti hizo yatasaidia kuandaa sera na miongozo mbali mbali. Taasisi hii imeanzishwa kwa mujibu wa "*Legal notice*" nambari 125 ya mwaka 2018, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tayari ameshamteua Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo na Bodi ya Ushauri tayari imeshazinduliwa.

Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Afya Pemba (PH010303)

Mhe. Spika, Afisi ya Uratibu wa Shughuli za Afya Pemba imeendelea kutekeleza kazi za uratibu wa shughuli za uendeshaji wa sekta ya afya zilizopangwa kufanyika Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Afisi ya Uratibu wa Shughuli za Afya Pemba ilitengewa jumla ya shilingi 9,682,916,000/=. Hadi kufikia Machi 2018, shilingi 6,778,443,130/= zimetumika, sawa na asilimia 70 ya fedha zilizotengwa.

PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (H02)

Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja ni miongoni mwa programu ya za Wizara ya Afya ikiwa na lengo la kuimarisha huduma za uchunguzi, matibabu, tafiti na kutoa mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wa kada za afya. Programu hii inahusisha programu ndogo mbili; ambazo ni:-

a) Programu ya Huduma za Uchunguzi na Matibabu; na
b) Programu ya Uongozi wa Hospitali na Utawala.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, serikali ilitenga jumla ya shilingi 10,380,579,000 kwa ajili ya Programu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hadi kufikia Machi 2018, jumla ya shilingi 8,435,616,804 (asilimia 81.3) zilitumika kwa ajili ya kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto;
ii. Kuimarisha huduma za uchunguzi na matibabu;
iii. Kuwapatia mafunzo na kuwajengea uwezo wafanyakazi wa hospitali katika fani mbali mbali ili kuimarisha ubora wa huduma za afya;
iv. Kufanya matengenezo ya miundo mbinu na ununuzi wa vifaa tiba;
v. Kuimarisha mafunzo ya vitendo yanayotolewa kwa wanafunzi wa kada mbali mbali;

Utekelezaji wa Programu ya Uchunguzi na Matibabu

Mhe. Spika, wakati Mhe. Rais wa Zanzibar alipokuwa akifungua majengo mapya ya mama na watoto katika Hospitali ya Mnazi Mmoja aliahidi kufungwa kwa mashine ya *MRI* kwa ajili uchunguzi. Napenda kuchukuwa fursa hii kuliarifu Baraza na wananchi kwa ujumla kwamba mashine hiyo tayari imeshaanza kufanya kazi za uchunguzi wa maradhi na huduma hizo zinatolewa bila malipo. Aidha, kituo cha mawasiliano cha matibabu masafa (*Telemedicine*) kimeanzishwa katika hospitali hiyo, ambacho kitasaidia kufanya mawasiliano na hospitali za nje ili kurahisisha uchunguzi na matibabu kwa wagonjwa.

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi 2018, jumla ya vipimo 117,828 vilifanyika katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Vipimo hivyo vinajumuisha uchunguzi wa maabara (84,350), *Endoscopy* (293), *Colonoscopy* (29), *X-ray* (13,876) *Ultra-sound* (16,706), *CT-Scan* (1,541) na *MRI* (1,033). Katika kuimarisha huduma hizi za uchunguzi, hospitali hii imepokea *X-ray* mbili, mafriji mawili ya Maabara kwa ajili ya kuhifadhia damu salama na jokofu la kuhifadhia maiti.

Mhe. Spika, jumla ya mahudhurio ya wagonjwa wa nje 74,975 **(**wanawake 39,148 na wanaume 35,827) yaliripotiwa katika Hospital za Mnazi Mmoja. Vile vile, wagonjwa 27,185 (wanawake 20,895 na wanaume 6,290) walilazwa; kati yao, wagonjwa 803 wamefariki dunia. Jumla ya wazazi 12,658 wamejifungua katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na Mwembeladu; wazazi 1,268 walijifungua kwa njia ya upasuaji. Aidha, jumla ya wagonjwa 2,322 walifanyiwa upasuaji wa maradhi mbali mbali. *Viambatisho namba 4, 7 na 8 vinatoa mchanganuo wa takwimu hizo.*

Mhe. Spika, huduma za matibabu zimeendelea kutolewa katika kliniki za maradhi mbali mbali zikiwemo huduma za saratani, huduma za kusafisha damu kwa wagonjwa wa mafigo na huduma za maradhi ya ubongo na uti wa mgongo. Jumla ya wagonjwa 410 wamepatiwa huduma za

matibabu ya uti wa mgongo kuanzia Januari 2018 hadi Machi 2018. Takwimu za wagonjwa waliohudumiwa katika kliniki maalum kwa hospitali za serikali zinaonekana katika Kiambatisho namba 13.

Mhe. Spika, katika kuwapunguzia wananchi na Serikali gharama za matibabu nje ya nchi, hospitali imeendesha kambi za uchunguzi na matibabu kwa mashirikiano na madaktari bingwa kutoka nchi za Spain, Uholanzi, Misri, China, India, Israeli pamoja na Jumuiya ya Wazanzibari wanaoishi nje ya Tanzania (*Diaspora*). Hadi kufikia Machi 2018, kambi 14 ziliendeshwa ambapo wagonjwa 3,736 walichunguzwa na kupatiwa matibabu ikiwemo wagonjwa 297 kufanyiwa upasuaji vichwa maji, midomo cheka pamoja na maradhi mengine mbali mbali (Kiambatisho Namba 14).

Programu Ndogo ya Uendeshaji na Utawala ya Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar awamu ya saba (7) imejidhatiti kuimarisha huduma za afya kwa kuongeza wataalamu wa afya katika Hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na kuhakikisha kwamba dawa na vifaa tiba vinapatikana muda wote. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Hospitali ya Mnazi Mmoja imepata jumla ya madaktari bingwa wanane (8) wakiwemo daktari wa macho, upasuaji wa watoto, matatizo ya kina mama, upasuaji wa masikio, pua na koo, upasuaji wa kinywa na Meno na matibabu ya watoto. Pia, hospitali imepokea wauguzi bingwa watano (5**)** wa huduma za kina mama na watoto na muuguzi mmoja (1**)** wa huduma za wagonjwa mahututi. Aidha, wauguzi wawili (2) wa shahada ya kwanza wamerudi masomoni na kuanza kazi.

Mhe. Spika, miongoni mwa mafanikio mengine ni kuendelea kwa mashirikiano na taasisi za kimataifa zikiwemo Hospitali ya ”*Drum Tower”* ya China, Hospital ya Chuo Kikuu cha *Haukeland* ya Norway na Hospitali ya ”*Nile Hope”* ya Misri. Mashirikiano hayo yanajumuisha mafunzo, kubadilishana wataalamu na kufanya kambi za matibabu. Jumla ya wauguzi watano na madaktari watano wanaendelea na taaluma ya vitendo nchini China.

Mhe. Spika, wafanyakazi 5 (*Radiographer* 2 na *Techinician* 3) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ya kutumia mashine ya *MRI*, wafanyakazi wawili (2) wamepatiwa mafunzo ya kutumia dialysis katika hospitali ya Muhimbili na wengine wawili (2) walipatiwa mafunzo ya vitendo ya utoaji wa huduma za fiziotherapi nchini Denmark. Aidha, wafanyakazi 20 wamepatiwa mafunzo ya matumizi ya mashine ya *Gene Xpert*.

Mhe. Spika, kwa upande wa elimu na utafiti, hospitali inaendelea kutoa mafunzo ya vitendo kwa madaktari kutoka taasisi za ndani na nje ya nchi. Jumla ya madaktari 24 wamemaliza mafunzo yao ya vitendo na wengine 27 wanaendelea na mafunzo hayo. Pia, hospitali inaendelea kufanya tafiti mbali mbali kwa kushirikiana na taasisi za elimu ya juu ndani na nje ya Tanzania. Aidha, vibali na ruhusa zimetolewa kwa madaktari watafiti 41 kufanya tafiti zao ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ikiwa ni sehemu ya mafunzo yao. Watafiti hao wanajumuisha ngazi ya stashahada, shahada ya kwanza, shahada ya pili na shahada ya uzamivu.

Mhe. Spika, miundombinu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja inaendelea kuimarishwa kwa kufanyiwa matengenezo ya aina mbali mbali ikiwemo, ukarabati wa jengo la wodi ya Mapinduzi

Mpya, upakaji wa rangi katika jengo kuu na kuwekewa alama za maegesho ya vyombo vya usafiri. Matengenezo mengine yamefanyika katika vyumba vinavyotoa huduma kwa kina mama Hospitali ya Muembeladu na matengenezo madogo madogo ya baadhi ya vyumba katika Hospitali ya Kidongo Chekundu.

Mhe. Spika, ujenzi wa ghala jipya la kuhifadhia dawa umekamilika, ghala hilo litaweza kuhifadhi dawa za miezi miwili kwa wakati mmoja na katika hali inayoridhisha. Vile vile, hospitali imefanya ukarabati wa jengo la huduma za "*Physiotherapy*" na kulifanya jengo hilo kuwa na mazingira mazuri kwa wafanyakazi na wagonjwa.

Mradi wa Kupandisha hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Spika, katika kuimarisha huduma za mama na mtoto, wodi ya wazazi ya zamani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja imefanyiwa ukarabati mkubwa. Wodi hii pia imepatiwa vifaa vipya na vya kisasa na inatarajiwa kurejeshwa kwa huduma za uzazi hivi karibuni. Kuanza kwa huduma katika wodi hii, kutasaidia kupunguza msongamano katika wodi mpya ya wazazi. Ujenzi huu ni awamu ya pili ya mradi wa kuimarisha huduma hizo ambao umehusisha ujenzi wa vituo 15 vya afya (Unguja 8 na Pemba 7), vya Unguja vyote tayari vimekamilika na vya Pemba tunategemea wakati wowote katika bajeti inayokuja vitakuwa vimekamilika kwa lengo la kuviongezea uwezo vituo vya afya na hatimae kupunguza mzigo katika hospitali za rufaa. Vituo hivyo ni Uroa, Umbuji, Tunguu, Kizimkazi Dimbani, Kijini, Kiboje, Chaani Kubwa, Bambi, Chambani, Kangani, Kisiwani, Kiuyu Kipangani, Makongeni, Shumba vyamboni na Wambaa. Vituo vya Unguja vimekamilika na vituo vya Pemba ujenzi wake unaendelea.

Mhe. Spika, pia matengenezo makubwa ya jengo la huduma za macho katika hospitali ya Mnazi Mmoja yanaendelea na ujenzi wake unategemewa kukamilishwa mwezi wa Novemba mwaka huu. Aidha, ujenzi wa jengo jipya katika eneo la hospitali ya wagonjwa wa akili umeanza. Kukamilika kwa jengo hilo kutasaidia kuimarisha mazingira ya utoaji wa huduma kwa wagonjwa wa akili.

Mhe. Spika, wizara imeendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi cha Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020 ambapo hadi sasa imeweza kutekeleza zaidi ya asilimia 70. Wajumbe wote nafikiri wamepewa programu zile za utekelezaji wa maagizo ya Ilani ya Uchaguzi. (Uk. 121 - 136)

CHANGAMOTO

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, kulikuwa na changamoto mbali mbali ambazo ziliathiri utekelezaji wa kazi zilizopangwa katika mwaka wa fedha 2017/2018. Changamoto hizo ni pamoja na:-

i. Uhaba wa rasilimali watu (madaktari bingwa, wauguzi, fundi sanifu dawa, fundi sanifu maabara, *radiologist, anaesthetist, medical imaging, biomedical engineers*, maafisa afya na kadhalika) na baadhi yao ni shida kuwapata katika soko;
ii. Upungufu wa dawa, vifaa tiba na "*reagents*" kwa baadhi ya wakati;

iii. Vifo vinavyotokana na uzazi na watoto wachanga;
iv. Kuongezeka kwa gharama za matibabu nje ya nchi hali iliyopelekea sehemu kubwa ya fedha za *OC* kutumika katika kiwasafirisha wagonjwa;
v. Uchakavu na upungufu wa baadhi ya vifaa vya kutolea huduma (*elevator*, mtambo wa *gas, CT-Scan*, vifaa vya maabara, *unaesthetic machines, Biochemistry and hematological analyser)* pamoja na uharibikaji wa mara kwa mara wa vifaa hivyo;
vi. Muitikio mdogo wa jamii katika kutumia huduma za mama wajawazito katika muda unaopendekezwa (chini ya wiki 16 za ujauzito) na baada ya kujifungua (ndani siku 42);
vii Matumizi madogo ya huduma za uzazi wa mpango;
viii. Ongezeko la maradhi yasio ya kuambukiza; na
ix. Matumizi ya lugha isiyoridhisha kwa baadhi ya wafanyakazi.

MWELEKEO WA BAJETI NA VIPAUMBELE YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA WA FEDHA, 2018/2019

Mhe. Spika, utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2018/2019 utajikita zaidi katika kuhakikisha kwamba kero na malalamiko ya wananchi yanapatiwa ufumbuzi. Kwa kipindi kirefu wizara imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo nilizozitaja hapo juu. Changamoto hizi zimekuwa zikiathiri utoaji wa huduma na kupelekea kero pamoja na malalamiko miongoni mwa wananchi walio wengi. Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imejipanga kuona kero hizo pamoja na malalamiko ya walio wengi yanatatuliwa.

Mhe. Spika, mwelekeo, vipaumbele na malengo ya bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2018/2019 umezingatia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (*Vision 2020*), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA III), Sera na Miongozo ya Sekta ya Afya, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2015 – 2020 pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (*SDGs 2030*).

Mhe. Spika, **k**auli mbiu ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2018/2019 inasema “Matibabu Bure ni Haki ya Kila Mwananchi”. Kauli mbiu hii inaelekeza upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wote bila ya ubaguzi wa aina yoyote kama ilivyoasisiwa katika Sera ya Afya ya mwaka 1965 mara tu baada ya Mapinduzi ya 1964 na kufanyiwa mapitio 2011. Hivyo, vipaumbele na malengo yatajikita katika kuimarisha utoaji wa huduma bora za afya ili wananchi wote hasa wanyonge waweze kufaidika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kutokana na azma hii, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibara imeongeza bajeti ya Wizara ya Afya kwa ongezeko la asilimia 27.9 na ongezeko la asilimia 97.6 kwa bajeti ya uendeshaji. Kwa upande wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, imeongezwa kwa ongezeko la zaidi ya asilimia 100. Ongezeko hili la bajeti haijapatapo kutokea; hivyo,wizara inaamini kwamba litasaidia kupunguza baadhi ya changamoto zilizopo katika Sekta ya Afya.

Mhe. Spika, wakati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipokuwa akizindua miradi ya Sherehe hizi za Miaka 54 ya Mapinduzi Zanzibar, alielezea nia ya kuziimarisha huduma za afya hasa katika suala la upatikanaji wa dawa, katika kuhakikisha

kwamba wananchi wanapata huduma za dawa kwa wakati wote. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeongeza bajeti ya dawa marudufu kutoka shilingi bilioni nne mwaka 2016/2017 hadi shilingi bilioni saba mwaka 2017 na kufikia shilingi 12.6 bilioni mwaka huu kwa mwaka wa fedha ujao. Ongezeko hili bajeti haijapata kutokea hata mara moja, naomba tumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuwa karibu na wananchi na kuona umuhimu wa wananchi wetu kupata afya inayostahiki. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wizara imepanga kuchukuwa hatua mbali mbali za kukabiliana na changamoto zinazojitokeza za utoaji huduma...

Mhe. Spika: Mhe. Waziri samahani kidogo, naomba nimpishe Mwenyekiti ili akalie kiti na uweze kumalizia hotuba yako. Mhe. Mwenyekiti karibu sana.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti, Mwanaasha Khamis Juma alikalia kiti)

Mhe. Mwenyekiti: Endelea Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, wakati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipokuwa akizindua miradi ya Sherehe hizi za Miaka 54 ya Mapinduzi Zanzibar, alielezea nia ya kuziimarisha huduma za afya hasa katika suala la upatikanaji wa dawa, katika kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma za dawa kwa wakati wote. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeongeza bajeti ya dawa marudufu kutoka shilingi bilioni nne mwaka 2016/2017 hadi shilingi bilioni saba mwaka 2017 na kufikia shilingi 12.7 bilioni mwaka huu kwa mwaka wa fedha ujao (2018/2019). Ongezeko hili bajeti haijapata kutokea hivyo wizara inaamini kwamba itasaidia kupunguza baadhi ya changamoto zilizopo katika sekta ya afya.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imepanga kuchukua hatua mbali mbali za kukabiliana na changamoto zinazojitokeza za utoaji huduma. Naomba nichukuwe fursa hii kueleza vipaumbele vya wizara kwa mwaka 2018/2019 kama ifuatavyo:-

i. Kuimarisha utoaji wa huduma katika hospitali na vituo vya afya;
ii. Kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na "*reagents*";
iii. Kuzipandisha hadhi wa hospitali za vijiji kuwa za Wilaya na Wilaya kuwa za Mkoa;
iv. Kuongeza upatikanaji wa rasilimali watu na maslahi yao;
v. Kusimamia nidhamu na maadili ya wafanyakazi; na
vi. Kuandaa muongozo wa kuhudumia wagonjwa wenye Bima ya Afya;

Mhe. Mwenyekiti, vipaumbele hivi pamoja na malengo yatatekelezwa kupitia program za wizara kama ifuatavyo:-

Programu ya Kinga na Elimu ya Afya

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa huduma ya kinga ya maradhi ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza zinaimarika**,** kwa mwaka wa fedha 2018/2019, programu hii imepangiwa

kutumia shilingi 14,074,387,000/= sawa na asilimia 15.1 ya bajeti ya wizara kwa ajili ya kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea kudhibiti maambukizi ya VVU;
ii. Kuendelea na mikakati ya kumaliza Malaria hasa katika maeneo ambayo bado maambukizo ya ugonjwa huu yanaripotiwa;
iii. Kuongeza kiwango cha chanjo kwa watoto walio chini ya umri wa miaka miwili kufikia zaidi ya asilimia 90 pamoja na kuendelea kutoa chanjo ya saratani ya shingo ya kizazi kwa watoto wa kike wenye umri wa miaka 9 - 14;
iv. Kuhamasisha jamii juu ya usafi wa mazingira ili kujikinga na maradhi mbali mbali yakiwemo maradhi ya kuharisha na kipindupindu;
v Kuhamasisha jamii juu ya masuala ya afya pamoja na kuendesha programu za afya maskulini;
vi. Kufuatilia mienendo ya maradhi ili kuweza kubaini mapema uwepo wa maradhi na kuchukuwa tahadhari zinazostahiki;
vii Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa yanayoambukiza na yasio ya kuambukiza;
viii. Kutekeleza mkakati wa kimataifa wa kudhibiti maradhi (*International Health Regulation - IHR*); na
ix. Kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vya watoto wachanga.

Programu ya Tiba

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, programu hii imetengewa shilingi 60,574,595,000/= sawa na asilimia 65.0 ya bajeti ya wizara kwa ajili ya kuimarisha miundombinu na utoaji wa huduma za afya katika hospitali za mikoa, wilaya na vijiji; kuimarisha upatikanaji wa damu salama, huduma uchunguzi wa kimaabara; na uendeshaji wa mabaraza na bodi za kusimamia maadili ya taaluma. Ili kufikia hayo, programu hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuongeza upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na "*reagents*";
ii. Kudhibiti upoteaji na matumizi mabaya ya dawa;
iii. Kubadilisha mfumo wa maombi na usambazaji dawa, vifaa tiba na "*reagents*" na kutoka Bohari Kuu ya Dawa (mwezi mmoja badala ya miezi mitatu**)**;
iv. Kuanza ujenzi wa bohari ya dawa Pemba;
v. Kununua vifaa vya maabara, vifaa vya chumba cha upasuaji na vya huduma ya meno ili kuweza kutoa huduma stahiki katika ngazi ya wilaya;
vi. Kuanza kwa ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika Hospitali ya Abdalla Mzee na kuendelea na ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali nyingine;
vii. Kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa mbili la wodi za wazazi na watoto katika Hospitali ya Kivunge**;**
viii. Kuanza kwa ujenzi wa jengo la ghorofa la wodi za wazazi, watoto na wanawake katika Hospitali ya Chake Chake;
ix. Kuendelea na hatua za ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Binguni**;**
x. Kufanya ujenzi na ukarabati mkubwa wa Hospitali ya Wete;

xi. Kukamilisha marekebisho ya Sheria za Baraza la Madaktari na ya Hospitali Binafsi;
xii. Kuimarisha shughuli za ukaguzi na uchunguzi wa chakula, dawa, vipodozi na kemikali; na
xiii. Kuanza ujenzi wa jengo la Maabara yaWakala wa Chakula na Dawa.

Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi zinategemea sana uwepo na usimamizi imara wa nguvu kazi, utekelezaji wa sheria na miongozo ya afya na uwepo wa sera na mipango inayotekelezeka. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019, programu hii imetengewa shilingi 18,604,017,000/= sawa na asilimia 20 ya bajeti ya wizara kwa ajili ya kuteketeleza malengo yafuatayo:-

i. Kusimamia maadili ya kazi kwa wafanyakazi (madaktari, wauguzi na watendaji wengine) na utoaji wa huduma kwa mujibu wa miongozo;
ii. Kuajiri wataalamu wa afya (madaktari, wauguzi, wafamasia, mafundi sanifu wa dawa na maabara, *radiographer, medical imaging, anaesthetist, biomedical engineers,* maafisa afya ya mazingira na kada nyingine za mifumo ya afya);
iii. Kukamilisha na kuanza kutekeleza mpango wa kuwapa motisha wafanyakazi (*retention and motivation strategy*);
iv. Kufanya mapitio ya mpango wa mafunzo ili uendane na mahitaji halisi ya utoaji wa huduma;
v. Kuwapeleka masomoni madaktari kwa ajili kujiunga na fani mbali mbali za ubingwa na kusomesha kada adimu (*radiographer, medical imaging, anaesthetist, biomedical engineers)*;
vi. Kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa takwimu za sekta ya afya ikijumuisha taarifa za afya kutoka katika jamii;
vii. Kufanya mapitio ya matumizi ya afya kiujumla - *NHA* (Serikali na Binafsi);
viii. Kuandaa Mpango Mkakati wa Nne wa Afya;
ix Kuandaa utaratibu wa kuwahudumia wagonjwa wenye bima ya afya katika hospitali za umma;
x Kukamilisha ujenzi wa jengo jipya la Hospitali ya Wagonjwa wa Akili;
xi. Kununua *Lift* la pili jipya kwa ajili ya Hospitali ya Mnazi Mmoja;
xii. Kununua mashine mpya ya *CT-Scan* pamoja na vifaa vya maabara (mashine 2 za *electrolyte analyser*);
xiii. Kufanya utafiti wa mimea inayotumika kwa tiba asili Zanzibar; na
xiv. Kuandaa miongozo ya kuendesha taasisi na tafiti za afya;

Programu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, ambayo ndio hospitali pekee ya rufaa hapa Zanzibar. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetenga shilingi 14,802,000,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali katika hospitali hiyo. Hivyo, pamoja na shughuli za kawaida Hospitali ya Mnazi Mmoja imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kutoa huduma za uchunguzi wa maabara, saratani *"histopathology", X-Ray, CT-Scan, MRI* na vipimo vya *Ultra-sound* kwa wakati wote;
ii. Kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vya watoto wachanga kwa kuhakiki kila kifo ili kujua sababu na hatimae kuchukuwa hatua stahiki;
iii. Kupunguza rufaa za wagonjwa wanaosafirishwa nje ya nchi;
iv. Kuingia mkataba wa matengenezo ya vifaa na vifaa tiba vyote muhimu pamoja kuajiri kampuni binafsi ya usafi;
v. Kujenga sehemu ndogo ndani ya uzio wa hospitali itakayowezesha jamaa za wagonjwa kukaa kwa ajili ya kusubiri taarifa za wagonjwa wao; na
vi. Kusimamia ulinzi na usalama wa vifaa.

SHUKURANI

Mhe. Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Afya kwa mwaka 2017/2018 yamechangiwa na juhudi na mashirikiano ya Washirika wa Maendeleo mbali mbali wa ndani na nje ya nchi yetu, taasisi za serikali na zisizo za serikali, sekta binafsi na wananchi ambao wote kwa pamoja walitoa michango yao ya fedha na utaalamu katika kuhakikisha malengo yaliyopangwa yanafikiwa. Wizara inatoa shukrani za dhati kwa moyo waliouonesha na tunawaomba waendelee kushirikiana nasi katika kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya nchini ili kufikia lengo la afya kwa wote.

Mhe. Mwenyekiti, shukrani za pekee ziende kwa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Serikali ya Denmark, Cuba, Uholanzi, Canada, Israel, Norway, Misri, Ujerumani, Korea, Uturuki, India, Kuwait, Marekani, Italy, Saudi Arabia, Oman, Uingereza, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, tunatoa shukrani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mashirikiano tunayoyaendeleza. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda kutoa shukrani kwa Mke wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Mama Mwanamwema Shein kwa mashirikiano yake na kuwa pamoja nasi katika shughuli zetu za afya na Mke wa Makamu wa Pili wa Rais, Mama Asha Balozi. Shukurani ziende kwa mashirika mbali mbali yakiwemo; *DANIDA*, Shirika la Afya Ulimwenguni (*WHO*), *UNICEF, UNFPA, HAUKELAND UNIVERSITY HOSPITAL* ya *Norway, Neurosurgical Education Development* ya *Spain, SAVE the CHILDREN, Ivo de Carneri, Engender Health, Dtree International, World Diabetic Foundation, World Bank, Sight Saver, HIPZ, JHIEPIGO,* Mfuko wa Kupambana na UKIMWI, Ukoma, Kifua Kikuu na Malaria *(GFATM), Measure Evaluation*, Mfuko wa Rais wa Marekani *(PMI), THPS, DFID, JHPU, IHI, WATER AID, Rotary UK, PEPFAR, ZOP, Zanzibar Milele Foundation*, kundi la G-20, na wale wote ambao sikuweza kuwaorodhesha katika hotuba hii. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha naomba kuwashukuru wale wote waliochangia katika kutayarisha hotuba hii. Shukurani maalum ziwaendee Naibu Waziri wa Afya, Mhe. Harusi Said Suleiman, Katibu Mkuu, Bi Asha Ali Abdulla, Naibu Katibu Mkuu, Bi. Halima Maulid Salum, Mkurugenzi Mkuu, Dr. Jamala Adam Taib, Afisa Mdhamini Pemba, Bi Shadia Shaaban Seif, Wakurugenzi wote, Wakuu wa Taasisi na wenyeviti wa Bodi na Baraza pia Mkurugenzi wa

Hospitali ya Mmazi Mmoja. Pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa kufanyakazi kwa ulewedi na umakini, ambapo juhudi na jitihada zao zinanisaidia kutekeleza majukumu ya wizara ninayoiongoza. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, maelezo yote yaliyomo katika hotuba hii ambayo sikuyasoma pamoja na muhutasari niliueleza naomba yaingie kwenye *hansard*. (*Makofi*)

HITIMISHO

MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

a) Matumizi ya kawaida

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019, Wizara ya Afya (Fungu H01) inakadiriwa kutumia kiasi cha shilingi 14,679,400,000/= kwa ajili ya mishahara; Shilingi 28,258,000,000/= kwa kazi za uendeshaji; na shilingi 2,051,800,000/= kwa ajili ya ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya Wizara. Aidha, Hospitali ya Mnazi Mmoja (Fungu H02) inakadiriwa kutumia shilingi 14,802,000,000/=, ambapo shilingi 10,424,000,000/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 4,378,000,000/= kwa kazi za uendeshaji.

b) Matumizi ya maendeleo

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa shughuli za maendeleo, wizara inakadiria kutumia shilingi 48,263,800,000/=. Kati ya fedha hizo, Shilingi 15,926,000,000/= ni kutoka serikalini; shilingi 22,337,800,000/= ruzuku kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na shilingi 10,000,000,000/= mkopo.

c) Mapato

Mhe. Mwenyekiti, , katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 Wizara imekadiriwa kukusanya mapato ya shilingi 252,939,000/= na shilingi 712,417,000/= kwa upande wa Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nawaomba wajumbe wa Baraza lako waijadili hotuba hii na hatimae waidhinishe matumizi ya shilingi 93,253,000,000/= kwa Wizara ya Afya (Fungu H01); shilingi 14,802,000,000/= kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja (Fungu H02); na mapato ya shilingi 252,939,000/= kwa Wizara ya Afya na shilingi 712,417,000/= kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba Wajumbe wa Baraza lako wajadili hotuba hii na hatimae waidhinishe matumizi ya shilingi 93,253,000,000/ kwa Wizara ya Afya (Fungu H01) shilingi 14,802,000,000 kwa Hospitali ya Mmazi Mmoja (Fungu H02) na Mapato shilingi 252,939,000,000/= Kwa Wizara ya Afya na shilingi 712,417,000/= kwa Hospitali ya Mmazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya wizara www.mohz.go.Tz. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Waziri, Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono.

(Hoja imetolewa iamuliwe)

Mhe. Mwenyekiti: Sasa naomba nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: (Kny. Mwenyekiti wa Kamati wa Ustawi wa Jamii): Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa 2018-19.

Utangulizi

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu katika kutekeleza majukumu ya kulijenga taifa letu. Pia, nachukua nafasi hii adhimu kwa moyo wa dhati kabisa, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kutoa maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Tunapozungumzia maendeleo ya sekta ya afya Zanzibar, vyovyote lazima tumwagie sifa maalum Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa dira na miongozo imara ya kuimarisha afya nchini mwetu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Waziri wa Afya Mhe. Hamad Rashid Mohammed kwa kuteuliwa kuiongoza wizara hii ambayo ina changamoto kubwa. Kutokana na kasi aliyoanza nayo Kamati ya Ustawi wa Jamii inaamini kuwa changamoto nyingi zitapungua na baadhi yao kumalizika kabisa. (*Makofi*)

Naomba nimpongeze tena Mhe. Waziri kwa kasi yake hiyo na naahidi mbele ya Baraza lako tukufu kuwa Kamati ya Ustawi wa Jamii na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa ujumla wake, tutampa ushirikiano wa hali na mali katika kutatua matatizo yaliyopo katika sekta ya Afya. Aidha, naomba nimpongeze Naibu wa Wizara hii Mhe. Harusi Said Suleiman kwa mashirikiano makubwa anayoendelea kuipatia kamati hii. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Naomba nichukue nafasi hii nitoe pongezi za kipekee kwa Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ambapo michango yao kwa kiasi kikubwa imekua inajenga na kulisogeza mbele gurudumu la maendeleo ya sekta ya afya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:

1. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini — Mwenyekiti
2. Mhe. Tatu Mohammed Ussi — Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Hidaya Ali Makame — Mjumbe

4. Mhe. Makame Said Juma Mjumbe
5. Mhe. Masoud Abrahman Masoud Mjumbe
6. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma Mjumbe
7. Mhe. Viwe Khamis Abdalla Mjumbe
8. Ndg. Aziza Waziri Kheir Katibu
9. Ndg. Khamis Hamad Haji Katibu

Mhe. Mwenyekiti, sekta ya afya ni miongoni mwa sekta nyeti ambazo zinahitaji umakini wa hali ya juu kutokana na huduma zinazohitajika kwa wananchi. Ni wazi kuwa kutokana na unyeti wa huduma hizo, bajeti inayohitajika ni kubwa ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka kila siku kutokana na ongezeko la idadi ya watu na mwamko mkubwa wa jamii kwenda hospitali wanapoumwa tofauti na zamani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inachukua nafasi hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa uamuzi wake wa kuiongezea bajeti Wizara ya Afya kwa asilimia 27.9 na ongezeko la asilimia 97.6 kwa bajeti ya uendeshaji ambazo ni shilingi 101,554,000,000/= ambapo bajeti ya mwaka jana 2017/2018 ilikuwa ni shilingi 72,936,229,000/. Kwa upande wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, imeongezwa kwa ongezeko la zaidi ya asilimia 100. Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa dhati kabisa inaipongeza serikali kwa uamuzi wake huu ambao ni uamuzi wa busara hasa tukizingatia hali halisi ya maisha na uchumi wa wananchi wake. Jambo hili linaonesha kwa uwazi nia ya serikali ya kuwaondolea mzigo wananchi wake ambao kwa muda mrefu walikua na kilio cha ukosefu wa dawa katika hospitali zetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa bajeti Wizara ya Afya ina program kuu nne ambazo ni:-

i) Programu ya Kinga na Elimu ya Afya;
ii) Programu ya Tiba;
iii) Programu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja; na
iv) Programu ya Usimamizi wa Sera na Utawala.

Mhe. Mwenyekiti, **k**atika utekelezaji wa programu hizo, bajeti ya kutosha inahitajika ili lengo liweze kufikiwa na wananchi waweze kunufaika. Pamoja na juhudi zilizochukuliwa na serikali za kuongeza bajeti ya Wizara ya Afya hasa katika suala zima la ununuzi wa dawa, kamati inasisitiza uongezwaji wa bajeti hiyo katika sekta nzima ya afya hasa tukizingatia kuwa afya ndio nguzo ya kila kitu kwa mwanadamu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeridhishwa na juhudi za kuimarisha huduma za afya zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuviwezesha vituo vya afya vilivyopo maeneo mbali mbali ambavyo vingi vimegatuliwa. Bado ipo haja kubwa ya kuimarishwa vituo hivi kwa kuweka wafanyakazi wa kutosha, kuwepo kwa madaktari katika vituo pamoja na dawa basi vitasaidia sana kupunguza idadi ya wananchi wanaokwenda Hospitali kuu ya Mnazi Mmoja ambayo hivi sasa serikali imefanya ndio Hospitali ya Rufaa kwa wananchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa ugatuzi, mamati imeshuhudia mafanikio kadhaa ambapo hapo awali hayakuwepo. Hata hivyo, Kamati inaona ipo haja kwa serikali kuharakisha juhudi za

kuwapatia mafunzo watendaji wanaohusika na ugatuzi ili changamoto zilizopo kwa sasa kutokana na ugatuzi ziweze kupungua au kuondoka kabisa.

PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA

Mhe. Mwenyekiti, programu hii utekelezaji wake unahitaji fedha za kutosha ili lengo liweze kufikiwa kutokana na mambo mengi ya msingi kubebwa na program hii. Masuala ya kinga pamoja na kuimarisha kampeni za chanjo na utoaji wa elimu ya afya ni miongoni mwa mambo muhimu ambayo yanahitaji kupewa kipaumbele cha hali ya juu. Kamati ya Ustawi wa Jamii inazidi kusisitiza umuhimu wa kutoa elimu kwa wananchi kutokana na maradhi mbali mbali yanayoweza kuibuka katika jamii yetu kama hivi mripuko uliopo wa homa ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii inazidi kuisisitiza serikali kuongeza bajeti katika program hii kutokana na malengo yaliyopangwa kutekelezwa yakiwemo ya kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa yasiyoambukizwa ukiwemo ugonjwa wa saratani. Wakati wa ziara za kamati, kamati ilielezwa kuwa wizara ina mpango maalum wa kuliimarisha jengo la wagonjwa wa saratani. Hata hivyo, kamati inasikitika sana kutokana na jengo kutokarabatiwa kwa wakati ambao ulipangwa na kusababisha huduma zilizokusudiwa kutopatikana kama ilivyoahidiwa mbele ya kamati ingawa baadhi ya huduma hizo zimeanza kutolewa.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Kinga na Elimu ya Afya kwa mwaka 2017/2018 ilipatiwa jumla ya shilingi 21,237,830,000/= ambapo hadi kufikia Machi 2028 jumla ya shilingi 15,022,451,964/= sawa na asilimia 70.7 zilitumika. Kwa mwaka ujao wa fedha Programu ya Kinga na Elimu ya Afya imetengewa jumla ya shilingi 19,669,126,000/- sawa na asilimia 19.4 ya bajeti ya wizara. Kamati inaiuliza wizara hivi tuko "*serious*" na kukinga maradhi kwa kutenga asilimia 19.4 ya bajeti ya wizara.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaiomba wizara kwa bajeti ya mwakani ihakikishe inaongeza fedha kwa ajili ya kutekeleza malengo mengi yaliyokusudiwa kufanywa, ili kuwasaidia wananchi wetu na hasa ikizingatiwa kuwa maradhi mengi ya kuambukiza hayana miadi na yanakuja kwa mripuko. Kwa kuzingatia hali hiyo ni vyema kuimarisha huduma za afya ya mazingira na elimu ya afya katika sehemu zote. Suala la uingiaji wa watu katika sehemu za bandari na viwanja vya ndege lipewe uzito unaostahiki kwa kuweka bajeti ya kutosha.

PROGRAMU YA TIBA

Mhe. Mwenyekiti, bajeti iliyopita ya Wiazara ya Afya katika program hii ilijipangia mambo mengi na miongoni mwao ni pamoja na kuimarisha upatikanaji wa dawa pamoja na kununua vifaa vya uchunguzi na kusimamia sheria mbali mbali za taasisi zinazosimamiwa na Wizara ya Afya. Hata hivyo, mipango hiyo haikuweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na ufinyu wa bajeti uliokuwa unaikabili wizara na kupelekea baadhi ya hospitali na vituo vya afya kukosa vifaa muhimu. Halikadhalika bajeti kubwa kutumika katika kusafirisha wagonjwa kupelekwa nje ya nchi kwa uchunguzi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii katika ziara zake za kikazi ilikutana na changamoto nyingi ambazo chanzo chake kikuu ni ukosefu wa fedha. Katika ziara hizo kamati

ilielezwa kufanyiwa ukarabati kwa baadhi ya hospitali ikiwemo Hospitali ya Chake Chake ambapo ukarabati wake haukufanyika kutokana na ufinyu wa bajeti. Ukarabati jengo la wagongwa wa saratani na mengineyo. Kamati inaisistiza serikali kuongeza bajeti kwa ajili ya kukamilisha yale yote yaliyopangwa na wizara ili huduma za afya ziweze kuimarika. Haipendezi kuona wodi ya wagonjwa ndani ya hospitali inavujiwa *ceiling* zote zimeoza na inahitaji kuweka mabeseni kukinga maji na kuweka pembeni vitanda . Suala kama hili haliwezi kungoja katika utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, Katika bajeti ya mwaka huu, bajeti ya ununuzi wa dawa imeongezeka ikiwa na lengo la kupunguza malalamiko ya wananchi. Ongezeko hilo litasaidia kuondoa malalamiko mengi ambayo yalikua yakijitokeza kutokana na kukosekana kwa dawa katika hospitali zetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi kuisistiza serikali kufanya juhudi za makusudi za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Binguni kutokana na ukweli kuwa kwa bajeti hii ya sasa tunayoipitisha fedha hazitotosha kuanza ujenzi mkubwa wa hospitali hiyo ambayo inatarajiwa kuwa ya kisasa na yenye vifaa vingi vya gharama kubwa.

PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ina lengo la kuimarisha huduma zinazotolewa katika hospitali ya Mnazi Mmoja, Muembeladu na Hospitali ya Kidongo Chekundu. Bajeti iliyopita, program hii ilitengewa shilingi 10,380,579,000/= kwa lengo la kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa ili kuwaondolea kero wananchi wanaopokea huduma zinazotolewa katika hospitali hizo. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti baadhi ya majukumu hayakuweza kufikiwa lengo lake lililokusudiwa kutokana na ukosefu wa fedha. Miongoni mwa majukumu yaliyopangwa ni pamoja na kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto huduma ambazo kwa namna ya kipekee zinahitaji fedha nyingi kwa lengo la kukinga afya ya mama na mtoto.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka ujao wa fedha 2018/2019 bajeti ya Hospitali ya Mnazi Mmoja imetengewa shilingi 14,802,000,000/=. Tunaipongeza sana serikali kwa kuitikia wazo la kamati na wajumbe la kuongeza bajeti ya program hii muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa suala hilo, Wizara ya Afya kwa namna ya kipekee ilifanya uzinduzi wa mpango mkakati wa uzazi wa mpangilio kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2018/2019 - 2022/2023. Kamati ya Ustawi wa Jamii ilikuwa ni miongoni mwa wadau walioalikwa katika uzinduzi huo kwa lengo la kutoa mawazo yatakayosaidia kuimarisha mpango huo na kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii inaipongeza wizara kwa uamuzi wake huo wa kuzindua mpango huu wa Jamhuri yas Muungano wa Tanzania chini ya *UNFPA* ambao ndio wahisani wakubwa. Lengo kubwa la mradi huu ni kulinda afya ya mama na mtoto. Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imekuwa na kiwango kikubwa cha vifo vya akina mama vitokanavyo na uzazi wakati wa kujifungua au baada ya kujifungua na vifo vya watoto wachanga.

Mhe. Mwenyekiti, Utumiaji wa Uzazi wa Mpango unawezesha kuimarisha afya ya mama na mtoto. Tafiti zinaonyesha kuwa endapo uzazi wa mpango utakuwa unafanya kazi vizuri basi vifo vya akina mama wajawazito vitapungua kwa asilimia 30. Kutokana na ukweli huo, naomba nichukue nafasi hii, kuwahamasisha wajumbe wenzangu kufanya juhudi mbali mbali za kuwahamasisha wananchi wetu kuzingatia suala la uzazi wa mpangilio.

Mhe. Mwenyekiti nachukua nafasi hii kuelezea suala hili kutokana na ukweli kwamba, vituo vyetu vya afya vilivyopo ni vichache na mahitaji ni makubwa sana na kupelekea baadhi ya kina mama wajawazito kulala watatu watatu kwa wakati wa kujifungua na wengine hata kulazwa chini.

Mhe.Mwenyekiti, kwa wingi wa idaid ya wazazi wakati wa kujifungua basi hata kile kitanda cha kujifungulia hakitumiki.Wazazi wanajifungua kwenye vitanda vya kulalia ndani ya wodi. Hivyo, ipo haja Waheshimiwa sote kuunga mkono mpango huu kwa faida ya wananchi wetu. Suala hili linakubalika kidini na silka za Kizanzibari. *(Makofi)*

PROGRAMU YA USIMAMIZI WA SERA NA UTAWALA

Mhe.Mwenyekiti ,wizara kupitia program hii kwa bajeti iliyopita ilipanga kutekeleza mambo mbali mbali ikiwemo kufanya mapitio ya mfuko wa fedha kwa timu za afya ili uendane na mpango wa ugatuzi wa madaraka pamoja na kutengeneza miongozo ya kisera ya utoaji wa huduma za afya. Hii ni rai nzuri. Kamati inatoa baraka zake kwa asilimia mia moja.

Mhe.Mwenyekiti, kamati inaipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kauli ya mgonjwa kufanyiwa vipimo vyote katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ikiwemo *CT-Scan, MRI* na *X-Ray* bila malipo. Pongezi pia kwa kazi nzuri ya Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi kwa kusimamia vyema ukaguzi wa chakula na dawa zinazoingizwa nchini.

Mhe.Mwenyekiti, kamati inaipongeza sana kwa kukamilisha kazi ya ujenzi wa jengo la Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Aidha, hatua ya kuwekwa mashine ya *DNA* ni ya mfano wa utekelezaji mzuri. Utafiti ni suala la msingi katika maendeleo ya taasisi au fani yoyote. Kuanzishwa kwa Taasisi Maalum ya Tafiti za Afya (*ZAHRI*) ni wazo zuri sana na tunapongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohammed Shein kwa maelekezo yake kufanikisha azma hio.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, mwisho naomba nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii katika Baraza lako tukufu, pia niwashukuru Wajumbe wako kwa utulivu wao waliouonesha wakati nawasilisha hotuba hii.

Mhe.Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wako waichangie bajeti hii, wahoji na watoe mapendekezo yao panapohitajika na hatimaye kuipitisha baada ya kuafikiana kwa hoja mbali mbali watakazoibua wakati wa mjadala.

Mhe.Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru sana, Mhe. Massoud Abrahman Massoud kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Usatawi wa Jamii.

Mhe. Masoud Abrahaman Massoud: Mhe. Mwenyekiti naomba na mimi nichangie mawili matatu baada ya kuniruhusu

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nimekuruhusu Mhe. Mjumbe.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi niendeleza kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kujali afya za wananchi wake wote wa visiwa vya Unguja na Pemba lakini pia na wale wageni ambao wapo Zanzibar. Vile vile, nimpongeze na Mhe.Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya yeye na Mhe. Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Afisa Mdhamini, madaktari, wauguzi na wafanyakazi wote wa afya hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka niseme maneno mawili katika mchango wangu. Jambo la kwanza Mhe. Mwenyekiti katika kikao kilichopita Mhe. Waziri aliniahidi kwenye jimbo langu kuwa Hospitali ya KMKM lakini pia Hospitali ya Jeshi Bububu itapata mgao wa dawa. Kwa hivyo, nimuombe tu Mhe. Waziri atakapokuja hapa aniambie lini wakwezi na wakulima wa majimbo hayo na wao watapata dawa kwenye hospitali hizo ambazo zipo karibu na wao watapata huduma hio.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nilitaka nilizungumzie ni suala zima la Hospitali ya Mbuzini najua suala hili liko kwenye ugatuzi lakini hapa pana ahadi ya Mhe. Rais, Mhe Waziri aliyepita alihangaika sana kutafuta wafadhili maeneo mbali mbali lakini Mwenyezi Mungu hakumjalia kufanikiwa kupata hao wafadhili, nimuombe Mhe. Waziri Hamad Rashid na Naibu waziri na watendaji wake wote wafanye kazi ya kututaftia wahisani, ili ile ahadi ya Mhe. Rais aliyoitowa kwenye Hospitali ile ya Mbuzini iweze kutekelezwa ipasavyo. Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niunge mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja mimi na wananchi wa Jimbo langu la Bububu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Nakushukuru Mhe. Masoud Abrahman Masoud kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea mchangiaji wetu wa mwanzo nitamwita Mhe. Asha Abdalla Mussa atafuatiwa na Mhe. Ali Suleiman Ali na Mhe. Simai Mohammed Said ajiandae.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii kuwa mchangiaji wa mwanzo katika Wizara ya Afya. Mhe. Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kunipa afya njema na kuweza kusimama hapa kuweza kuchangia hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri wa Afya pamoja na Naibu wa Waziri wa Afya wakiambatana na watendaji wake wote wa wizira hii. Kwa kweli Mhe. Waziri wake pamoja na Naibu wake wanajitahidi sana katika kufatilia hatua kwa hatua katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba kwa kuwa sasa tuna mtindo humu ndani wakati wa kupitisha vifungu lazima wakati wa kuchangia uweke nia ya kuzuia fungu. Mhe. Mwenyekiti, nazui kabisa hapa natangaza nia nataka kuzuia fungu ambalo linasemema kwamba H0101 Huduma za Kinga na Elimu ya Afya, lakini pia fungu la H0102 Huduma za Tiba na Uendeshaji wa Uratibu wa Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli viongozi wetu hawa wanafanya kazi kubwa sana na wizara hii ni wizara muhimu kwa nchi yetu lakini pia kwa jamii yetu na nimeona katika kitabu chao hichi cha hutuba kuna kauli mbiu ya mwaka 2019/2019 ambayo inasema "Matibabu Bure ni Haki ya Kila Mwananchi wetu". Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana kwa kuleta na kufikiria kauli mbiu hii. Lakini pia nimpongeze Mhe. Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuona kwamba kupau mbele hii huduma ya afya bure kwa wananchi wetu ni muhimu kwa nchi yetu hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuchangia nianze uk.12 ambayo unazungumzia masuala mazima huduma ya afya ya uzazi ya mama na mtoto, Mhe. Mwenyekiti wizara ina utaratibu wa kufatilia sababu ya kila kifo kinachotokana na uzazi na vifo vya watoto wachanga pamoja na wamama wajawazito.Mhe. Mwenyekiti, hapa wametuorodheshea jumla kwa mwaka 2017/2018 kuna jumla ya mama 58 wamefariki dunia kutokana na matatizo ya uzazi katika hospitali. Miongoni mwa sababu zilizogundulika zimepelekea vifo hivyo ni zile zinatokana na jamii zikewemo zimetajwa hapa.

Lakini katika kiambatanisho na hapa pia zinaonesha ni twakimu za wamama ambao wamefariki kutokana na ujauzito lakini nasikitika sana kwamba hakuna takwimu sahihi ambayo inaonesha vifo vya watoto wanchanga. Namuomba sana waziri atakapokuja kwenye majumuisho aniletee takwimu halisi ya vifo vya watoto wachanga kwa mwaka 2016/2017 vilikua vingapi, na kwa mwaka 2017/2018 kwa sasa viko vingapi. Namuomba sana Mhe. Waziri hapo ndipo tutakapopima kwamba idadi ya vifo vya watoto wachanga vimepungua au vimeongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 24 na 25 kuna Programu ya Huduma za Tiba katika ukurasa wa 25 hapa 71 kuna fedha hapa ambazo zilitengwa kwa ajili ya programu ya humuda za tiba hii inasema kwamba kuimarisha upatikanani wa dawa muhimu kwa mujibu wa muongozo uliyopo pamoja na vifaa tiba, lakini niseme kwamba fedha zinatengwa na tunapitisha Barazani. Kwa kweli, Mhe. Rais wa Zanzibar kupitia Wizara ya Fedha na Mipango zinatenga fedha nyingi na zinatoa fedha kwa ajili ya kupatikana tiba pamoja na madawa katika hospitali za vijiji, za Wilaya pamoja na Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja.

Lakini cha kusikitishwa kwamba wananchi wetu wanapokwenda katika vituo hivi kwa kweli waambiwa dawa hakuna lakini wanahitaji wakanunue. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli masuala haya yanasikitisha sana kwa sababu mgonjwa anapokwenda katika Hospitali ya Mnazi Mmoja au ya Kivunge ana matatizo makubwa lakini anafika pale dokta anamwambia huwezi kupata huduma hii mpaka uchangie fedha kiasi fulani, kwa kweli suala hili linasikitisha sana tena linasikitisha sana.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa kwa kuwa kila mwaka tunatenga fedha kwa ajili ya huduma za tiba katika hospitali zetu za vijiji za wilaya pamoja na

Hospitali ya Mnazi Mmoja nataka kujua kwamba hivi vifaa tiba ambavyo vinapelekwa vinakuwa ni vidogo au vinakuwa vinakwenda lakini havijulikani vinakokwenda, lakini pia au madaktari waliopo hawatekelezi wajibu wao na kama hatatekelezi wajibu wao ipasavyo serikali inawachukulia hatua gani.

Vile vile, kuna pesa ambazo pia zinatengwa kwa ajili ya kupata huduma wananchi wetu ambao wanasafirishwa nje ya nchi kwa ajili ya matibabu ya maradhi ya moyo kensa na mambo mengine. Lakini utakuta kwamba wananchi hawa wanatoleshwa pesa kwa ajili ya kupata yale matibabu na tukizingatia kwamba huduma hizi ni huduma bure na fedha zinatengwa na serikali kwa ajili ya kuhudumiwa watu hawa. Kwa hivyo, nataka kujua baadae atakapokuja hapa Mhe. Waziri atueleze ni sababu gani zinazopelekea kwamba wananchi wetu wanapokwenda katika hospitali hizi wanatakiwa wachangie fedha nyingi kwa ajili ya kupelekwa kupata huduma hizi.

Lakini kuna suala zima katika ukurasa wa 26 kipengele hapa kinazungumzia kuimarisha ujenzi wa Maabara wa Mkemia Mkuu wa Serikali. Mhe. Mwenyekiti, mwaka 2017/2018 tulipitisha fedha kwa ajili ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na fedha hizo zilikuwa jumla ya shilingi bilioni 1,800,000 na kwa mwaka huu tumeona kwamba wameomba tena milioni 900, Mhe. Waziri atakapokuja hapa naomba kwamba anipe ufafanuzi kwamba kwa mwaka 2017/2018 hizi bilioni 1 na milioni mia nane walipatiwa kiasi gani na wamezitekelezea kwenye matumizi yapi, lakini pia na hizi fedha ambazo wameziomba sasa hivi milioni 900 ni kwa ajili ya matumizi gani.

Lakini pia kwamba hapa katika ukurasa wa 27 wanasema kwamba jumla ya wagonwa 271 walisafirishwa nje ya nchi lakini kati ya hao kuna watoto 30 walipelekwe katika upasuaji wa moyo nchini. Kwa hiyo, naomba kujua kwamba hizi fedha ambazo wanatumia hawa watoto wetu 30 waliokwenda kufanyiwa upasuaji, matumizi yao hizi gharama zilitolewa na serikali au gharama hizi wametoa wenyewe wagonjwa. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti niseme kwamba kutokana na haya ambayo nimeyaomba hapa nipewe ufafanuzi naomba sana kwamba wizara ijuwe kwa kuwa kauli mbiu ni "Matibabu Bure ni Haki ya Kila Mwananchi" naomba sana wizara husika ifuatilie kwa sana kuhakikisha kwamba huduma hizi zinatolewa bure.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli masuala haya yanasikitisha sana, wananchi wanapopatwa na matatizo wanapokimbilia katika vituo vyetu vya huduma wanaona kule ni sehemu ambayo waaweza kupata matibabu na kuhakikisha kwamba afya zao zinakaa vizuri. Lakini jambo la kusikitisha tarehe 6/5/2018, kuna wananchi wa Jimbo la Kiwengwa walipata maafa ya kichaa cha mbwa, na hatimae wananchi wale walipopelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kivunge kwa ajili ya matibabu kwa kweli wananchi wale huduma ile nyengine muhimu hawakuipata siku ile, matokeo yake siku ya pili walipokwenda hakuweza kufanyiwa matibabu yale bure madatari baadhi yao wakahitaji fedha kwa ajili ya kutoa fedha ili wapate ile huduma ambayo ya msingi.

Jambo la kusikitisha kwamba ile hospitali ni ya serikali, madaktari ni wa serikali lakini ni sababu gani ambazo wao kimewapelekea kuwatolesha fedha wagonjwa wale Mhe. Mwenyekiti ,inasikitisha sana sasa hivi kuna msiba mkubwa katika Jimbo la Kiwengwa wananchi wawili wamepoteza maisha yao. Mhe. Mwenyekiti haya masuala yametosha, tena yametosha sana watoto wadogo wamepoteza maisha yao kwa ajili ya madaktari uzembe wao Mhe. Mwenyekiti nakuomba sana Mhe. Waziri afanye uchunguzi, ili kuhakikisha kwamba madaktari waliofanya

uzembe huu wanachukuliwa hatua. Mhe. Mwenyekiti, kwa haya machache naonga mkono kwa asilimia ishirini(*Kilio/Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Asha Abdalla Mussa kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Ali Suleiman Ali, atafuatiwa na Mhe. Simai Mohammed Said na Mhe. Zulfa Mmaka Omar ajiandae.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Afya kwa bajeti ya mwaka fedha 2018/2019. Lakini pili ni mimi niwape pole watu wa Kiwengwa kwa bahati mbaya ya yaliyotokea na tumuombe Mwenyezi Mungu wenzetu wanaofikwa na mambo hayo wawe na imani kabisa katika nyoyo zao ili kuhakisha kwamba kazi ni kiapo, na kazi ya matibabu ni kiapo zaidi katika maisha ya kila siku kwa unao wahudumia.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri wa Afya, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, madaktari wetu, wauguzi wetu kwa kazi yao nzuri wanayofanya na ngumu,lakini Mwenyezi Mungu awape uwezo zaidi wafanye kazi zao ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpe salamu Mhe. Waziri wa Afya, kabla sijaingia kwenye kitabu kuna mambo mawili tu. Wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele wanatarajia kuondokana na shida ya kupata huduma katika Kituo cha Afya. Kituo hicho kila siku husema aliyekuwa mwakilishi wakati huo na lilipokuwa Jimbo la Mwanakwerekwe Mhe. Shamsi Vuai Nahodha ambaye sasa hivi ni mbunge na Mhe. Haji Juma Sereweji alikuwa mbunge mstaafu wa jimbo hilo, walijenga kituo kizuri na kina mama wajawazito na watu wengine wanakitegemea kwa huduma ambazo watazipata. Kwa hivyo, nimuambie Mhe. Waziri akimaliza bajeti yake na Mwenyezi Mungu atamjaali bajeti ipiti vizuri ili tuweze kuwahudumia wananchi huko mitaani.

Mhe. Mwenyekiti, akimaliza yeye na *taskforce* yake nitamuomba akakitembelee kituo hicho kwa manufaa ya wananchi wetu, hasa tukizingatia Mhe. Mwenyekiti, kituo cha Magirisi Taveta, kitawanufaisha wananchi wapatao 40,000. Msongamano wa Kituo cha Afya Fuoni utaondoka. Kwa hivyo, hiki pamoja na kuwepo katika ugatuzi, tutafahamiana huko mbele tutakapokwenda na maelezo mazuri kwa ajili ya wananchi wetu wa Jimbo la Kijitoupele.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nilipata salamu kutoka katika shehia mbali mbali za jimbo hilo hilo na kwengineko. Kuna wahamasishaji hawa wanaowatembelea mama wajawazito kwa ajili ya angalau kuwaelekeza kwamba wakati mzuri, wakishapata ujauzito kwenda kuchukua ushauri au kupata vipimo vya mapema au chanjo za mapema. Hawa wanafanyakazi nzuri na wanaendelea na juhudi zao. Lakini namuomba sana Mhe. Waziri angalau wafikiriwe chochote kwa sababu wanafanyakazi nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, amenipa taarifa juzi tu, nyuma walikotoka kulikuwa kuna mapungufu makubwa akinamama kuchelewa kufika vituoni. Lakini leo wanafika kwa wakati na kwa asilimia zaidi ya 90 wameshajihika wananchi au akinamama wajawazito wanafika katika vituo vya afya kuangalia afya zao salama. Kwa hivyo, naipongeza wizara na namuomba Mhe. Waziri hili tulifuatilie ili kuwaangalie wale wanaohusika katika angalau kujaaliwa chochote.

Mhe. Mwenyekiti, nende kwenye ukurasa wa 35. Kwanza niipongeze serikali, nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kuna nukuu yake hapa naomba niisome kama ilivyo katika *paragraph* ya 100, kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Rais alisema ifuatavyo. Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alizindua Baraza la Nane la Wawakilishi Novemba, 2010 alisema nukuu hii ifuatayo:

> "Hospitali zilizo katika kiwango cha *cottage* za Micheweni, Vitongoji Pemba na Makunduchi na Kivunge Unguja nazo zitapandishwa daraja zifikie hadhi ya kiwango cha hospitali za wilaya".

Mhe. Mwenyekiti, kuna maelezo mengine hapo mazuri tu. Kwanza awepo wafanyakazi wa kukidhi hospitali ya wilaya, hapa kwa ufupi pana maelezo mazuri tu, pawe na vigezo ambavyo vinakubalika. Kwa kweli, suala hili nalipongeza na nalipongeza kwa dhati kabisa kwamba linahitajika kwa wakati tulionao.

Lakini ukija kwenye ukurasa wa 50 na 51 kuna maelezo mengine mazuri zaidi, yanasema kwamba katika mwelekeo wa bajeti ya mwaka 2018/2019, *paragraph* ya 140. Nasoma kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti. Kaulimbiu ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2018/2019 inasema ifuatavyo na wananchi wanatusikiliza. "Matibabu Bure ni Haki ya Kila Mwananchi".

Mhe. Mwenyekiti, kaulimbiu hii inaelekeza upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wote bila ya ubaguzi wa aina yoyote, kama ilivyoasisiwa katika sera ya afya ya mwaka 1965 mara tu baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 na kufanyiwa mapitio mwaka 2011. Kwa hivyo, vipaumbele na malengo yatajikita katika kuimarisha utoaji wa huduma bora za afya, ili wananchi wote hasa wanyonge waweze kufaidika.

Mhe. Mwenyekiti, naliunga mkono kwa asilimia mia moja hili, lakini linatupa wasi wasi. Mhe. Waziri anajitahidi kwa uwezo wake wote aliojaaliwa, anajitahidi kufanyakazi kwa kila mbinu. Nafikiri kama angekuwa mwanajeshi kama mimi, basi tunaita mbinu za kivita. Anaweza kuingia usiku, anaweza kuingia wakati mwengine kavaa kama kanzu mtu wa kawaida tu. Mimi tetesi nazipata nyingi Mhe. Mwenyekiti, alikwenda pahala fulani simtajii, lakini baadae nitakuja kumtajia, alipofika akakaa kwenye foleni ya dawa, maskini mtoaji dawa hamjui, Hospitali ya Mnazi Mmoja hiyo.

Lakini kwa bahati nzuri au mbaya kakaa pale akaambiwa lete cheti chako, umekaa husemi hapo. Akapeleka cheti, kile cheti hakina muhuri wa aina yoyote. Lakini mtoaji dawa alikuwa madhubuti kidogo pamoja na ujeuri, maana yake kidogo alitumia maneno ya ujeuri sio mazuri, mtu mzima ukimuona useme, ah! Mzee wangu njoo kwa taratibu, lakini yeye alitumia lugha mbaya kidogo sipendi. Akamwambia hiki cheti hakina muhuri nenda zako. Mhe. Waziri yupo pale. Huyo aliyenipa salama alikuwepo, lakini tutakuja kuzungumza baadae. Kwa hivyo, hapa nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kufanyakazi zake kwa juhudi.

Ombi langu Mhe. Mwenyekiti, wasaidizi wake wote wakiwemo madaktari, wauguzi na wengineo tumsaidie Mhe. Waziri, kwa sababu Mhe. Waziri mmoja yote hatoyapata huko anakokwenda bila ushirikiano mzuri ambao utasaidia.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nilimuona kwenye televisheni juzi katika Kituo cha Afya cha Rahaleo, alipoingia alipata maelezo mazuri. Moja wapo Mhe. Waziri mbona nimesikia kuna moja, mbili, tatu. Mama yule ndiye mkuu wa kituo akasema. Mhe. Waziri kweli ulipata taarifa kaja mtu kalalamika huko, lakini alipokwenda ana cheti chake yule mtu hata hashughuliki, akiitwa jina hana habari. Alipokwenda pale mama akamueleza wazi, kweli mimi nilimtoa nje kwa sababu hakuzingatia wakati wake na kuna wengine wanasubiri.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, tuseme tu kwamba haya yote yanaonesha dhahiri kwamba watu wetu wanafanyakazi kutokana na uwezo wao na wengine hawana uwezo, kwa hivyo tushirikiane ili tupate uwezo wa kufanyakazi hizi kazi ni muhimu na hatari kwa wananchi wetu. Wananchi wanataka msaada na wanataka kauli nzuri ili waendelee na shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa bajeti ya mwaka huu imeongeza asilimia 100. Kwa kweli, naipongeza serikali kwa moyo safi kabisa na naipongeza kwa kuona umuhimu wa hospitali hii kama ni hospitali yetu kuu na ya rufaa ambayo wananchi wetu wanahitaji huduma wanyonge na wengineo, suala hili nalipongeza.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwamba panapoongezwa fedha basi ni kuongeza kasi ya kufanyakazi. Kwa hivyo, wale watendaji wetu nawaomba sana imani izidi wafanyekazi zao vizuri, ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata shughuli zao za kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa huo wa 51 namba 3 kinasema, kuzipandisha hadhi hospitali za vijiji kuwa za wilaya na kuwa za mkoa. Nafikiri wakati umefika, tusing'ang'anie vituo vya afya tu kila siku, lakini tutizame na hali vile vile. Miji yetu imekuwa na wananchi wameongezeka, kwa hivyo pakiwa na hospitali ya wilaya basi watu watakuwa na matumaini zaidi na ukienda mkoa halikadhalika itakuwa zaidi. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri suala hili lisimamiwe ili lilete manufaa kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 52 programu ya Kinga na Elimu ya Afya. Mhe. Mwenyekiti, naamini kwamba elimu ni suala zuri na muhimu kwa sababu wananchi wetu wanataka taaluma mbali mbali. Hapa kuna mambo mengi ambayo yamezungumzwa, kuendeleza kudhibiti maambukizi ya *VVU*, kuendelea na mikakati ya kumaliza maleria hasa katika maeneo ambayo bado maambukizi ya ugonjwa huu yanaripotiwa, hilo ni suala zuri. Kwa hivyo, tuamini kwamba katika baadhi ya maeneo yako vizuri na mengine hayako vizuri, hivyo wale wanaohusika na kazi yao hiyo, ielekezwe ili malaria iwe historia katika nchi yetu. Naamini historia kwa upande wa Afrika ya Mashariki na kati Zanzibar tuko vizuri, maradhi haya yameondoka kabisa katika maeneo yetu.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, tulizungumza suala la kuhamasisha jamii juu ya usafi wa mazingira ili kujikinga na maradhi mbali mbali, yakiwemo maradhi ya kuharisha na kipindupingu. Suala hili mimi nafikiri sheria kama zimewekwa basi ziongezwe hali ya kipindupindu na uchafu yamezagaa katika maeneo yetu. Kwa hivyo, mwananchi ni lazima tuhakikisha kwamba wakati umebadilika kuwe na sheria zinazomkataza mtu kufanya jambo baya chafu.

Kwa wenzetu Mhe. Mwenyekiti, ukitoka kwenda kutembea tu basi ujiti wa kibiriti huwezi kuutupa chini, lakini hapa imekuwa kama ni utamaduni, na mimi husema kila siku kwamba

maeneo yetu au mazingira yetu machafu yanatia aibu katika nchi yetu, sio sokoni, sio mashuleni na sio penginepo. Kwa hivyo, imefika wakati taaluma hii itolewe ili kuinusuru jamii yetu isipotee.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nitakalolizungumza hapa kwa ufupi ni kuhamasisha jamii juu ya masuala ya afya pamoja na kuendesha programu ya afya maskulini. Mhe. Mwenyekiti, hili ni suala zuri, kwa sababu katika skuli zetu ni mkusanyiko wa vijana wetu wengi, na ili mwanafunzi awe mzuri awe mnadhifu, lakini pia mazingira yake yakidhi kwamba hapa pahala panafundishwa jambo zuri. Ukimuelimisha mwanafunzi kuanzia huko anakotoka, basi atakuwa mazingira yake atayajenga vizuri mpaka anakoishi anakolala mwenyewe. Kwa hivyo, wakati umefika Mhe. Mwenyekiti, tuhakikishe kwamba taaluma hii tunaifikisha ili kuhakikisha kwamba jamii yetu tunaelekea katika mwelekeo mwema na mzuri huko mbele tunakokwenda.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, pamoja na yote yaliyotokea, ndugu yangu Mhe. Asha Abdalla Mussa katoa kilio kikubwa sana na kilio hiki kinatugusa sote humu. Narudia tena kauli yangu Mhe. Mwenyekiti, kazi yoyote ni kiapo, lakini kazi uliyopewa na Mwenyezi Mungu kumfanya mwenzio angalau kumpa nafuu au apone basi ni kazi ya mwisho. Maponesho anayo mwenyewe Mwenyezi Mungu, lakini na wewe kama umepewa kazi ile unaweza kumuhatarishia mtu maisha yake.

Kwa hivyo, niiombe sana serikali hili suala lililotokea lifuatiliwe na suala hili Mhe. Mwenyekiti, likiachiwa litakuwa kama endelevu ni hatari. Tunasikia mambo mengi, tumesikia Kilombero juzi, kuna watoto waliofariki, nafikiri ndio jimbo lake yeye hili. Mmoja kaparwa na mbwa kafa na mwengine kaparwa, kutokana na ukosefu wa mambo madogo madogo. Kwa hivyo, tukubaliane kwamba umefika wakati panapotokea haja ya kinga basi iwe ni bure na mwananchi asisumbuliwe kwenda huku na huku, kila mmoja na uwezo wake na ajali haina kinga.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nasema tu kwamba naikubali hotuba hii na namuomba Mhe.Waziri mara baada ya kwishakumaliza bajeti yake, basi tufuatane twende kwa wananchi wangu wa Taveta ambapo kuna kituo kitawasaidia sana kinamama wajawazito na wazee. Naunga mkono kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Ali Suleiman Ali kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Simai Mohammed Said, atafuatiwa na Mhe. Zulfa Mmaka Omar na Mhe. Suleiman Sarahan Said ajiandae.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Nichukuwe fursa hii kwanza nikushukuru wewe kwa kuniona na kunipa nafasi hii niweze kutoa mchango wangu katika Wizara yetu hii ya Afya. Niseme tu kwamba nawapongeza Mhe. Waziri na wajumbe wa kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi nianze kwa kusema kwamba nitangulie kwa kumpa pole ndugu yangu Mhe. Asha Abdalla Mussa Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa kwa mtihani uliomkuta, lakini pia nikiri kwamba mitihani hii ipo katika jamii zetu zote, na *Inshaa Allah* Mwenyezi Mungu ataweza kutusaidia na kuhakikisha kwamba hospitali zetu zinakuwa zinaboreshwa, ili mambo haya tutokane nayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi niseme kwamba siungi mkono hoja na ninazuwia mafungu ya PH0103, PH0201 na PH0202. Niseme tu Mhe. Mwenyekiti, kwamba inawezekana maelezo yatakapokuja yatasaidia, lakini siku ya Ijumaa pia nilinyimwa fursa yangu na mimi, baada ya kusema kwamba siungi mkono hoja Mhe. Mwenyekiti, aliyekuwepo na nilimuona mmoja katika wasaidizi wa Baraza hili, akininyooshea mkono akipora madaraka ya kiti, akiniambia kwamba wewe, akinifanyia ishara kwamba yeye hatanipa nafasi mimi ya kuchangia. Kwa hivyo, niseme tu kwamba leo nimeshaweka kabisa hapa kutaja, nafikiria jina lake ninalo nitakuletea. Lakini niseme tu kwamba madaraka ya kiti yaheshimike, wasaidizi waendelee kuwa wasaidizi wasitunyooshee mkono sisi, wao kama watendaji wetu wa kuweza kutusaidia katika Baraza hili wakajifanya wao sasa ni sehemu ya maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo sasa naomba niende katika mchango wangu moja kwa moja. Kwanza nichukuwe nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwamba sekta ya afya katika kipindi cha bajeti ya mwaka huu tumeona mabadiliko makubwa, lakini pia kwa upande wa bajeti. Nimeangalia katika kitabu kama malengo na shabaha. Nilipokuwa napasoma katika upande wa bajeti ya mwaka 2018/2019, ukiangalia kwa upande wa bajeti ya ununuzi wa dawa, vifaa vya tiba na *reagents,* mwaka jana kuelekea mwaka huu fedha ambazo zilitengwa ni bilioni saba. Lakini ukiangalia kwa mwaka 2018/2019, sasa tutakuwa tuna bilioni 12.7. Lakini bado mimi nina *reservation* zangu kwamba hili sijui kama litakuwa ni sahihi au litakuwa linafanyiwa moja kwa moja.

Lakini baada ya hapo sasa nitalirudia hilo baadae kidogo. Sasa nataka niseme kitu chengine. Kwanza nataka nizungumzie masuala ya *biomedical engineers* katika hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na wengine. Pia tuna upungufu wa hawa ma- *Nursetutor* pamoja na *Anaesthesiology* wa kuweza kufanya hasa katika masuala ya operesheni. Tuna changamoto japokuwa natambua kuwa changamoto hizi hutokezea katika maeneo yote duniani, lakini pale ambapo watu wanahitaji kufanyika maoperesheni bado ni changamoto kwa hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, tusisikie tunaposema kwamba Wizara ya Afya, macho yote ya wananchi yapo katika hospitali ya Mnazi Mmoja. Sasa ukiangalia kwa mfano upande wa *(ENT) Ear Nose and Throat*, na kwa upande wa vyumba vya upasuaji bado kuna changamoto. Kwa hivyo, bado haya mambo Mhe. Waziri atakapokuja atueleze ana mpango gani katika kutatua changamoto hizi, hasa *delay* za mambo ya operesheni, watoto, kinababa na kinamama.

Halikadhalika nataka niulize swali la hospitali ya Binguni, ukiangalia kwenye bajeti mwaka jana walipanga michoro na utaratibu utaanza. Lakini matarajio yangu ilikuwa ni kwamba mwaka huu hasa katika hospitali ya Binguni ningeona sasa tayari majengo yameshaanza kusimama, tayari wameshakwenda kwenye hatua nyengine tofauti. Sasa atakapokuja waziri atueleze suala la hospitali ya Binguni, maana yake ukiangalia kwenye bajeti mwaka huu wametenga bilioni mbili tu.

Pia Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze suala la madawa. Utaratibu wa serikali kwa mfano katika hospitali hizi za Kivunge pamoja na Makunduchi. Nilimsikia kauli ya Mhe. Waziri hivi karibuni anasema kwamba hasa kina mama wanapotaka kujifungua, kwamba wasichajiwe fedha iwe ni bure, serikali itakuwa ipo tayari kufidia. Lakini hizi hospitali pia zilikuwa zinatumia

katika mfumo wa *cost sharing*. Sasa endapo tunaamua kwamba tunaondoa mfumo huu usiwepo kwamba serikali itakuwa inafidia. Sasa hebu tuangalie mfumo mzima wa yale ambayo wanayahitaji.

Kwa mfano, ukiangalia mama mjamzito anataka kwenda kujifungua katika hospitali kama hizi ambazo ziko katika wilaya na mikoa huko, watakuwa wanahitaji kwa mfano anaambiwa ende na *jik*, dawa pamoja na vitu kama vile vitambaa ambavyo ni *marking toshi* vya kuweza kutandika katika vitanda. Sasa ukiangalia kwa mfumo huu ikiwa wale wenyewe fedha hawana na ukiangalia na huyu madawa ambayo yanatoka katika *centre medical store* na huyu msimamizi wa *head of durative services*, panakuwa pana mlolongo mkubwa na fedha yenyewe kama bajeti haitoshi ili kupeleka katika haya maeneo pia.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja japokua anasema bajeti anaongeza ni atatuhakikishiajie kwa mfano ukienda katika buku hili unasoma mikakati elekezi ya sekta kwa mwaka 2018/2019. Mwaka jana nimezungumza hapa changamoto ambayo *medical engineer* nikazungumzo suala *reagents* kwa ajili ya *labe* zetu za Mnazi mmoja. Mshine zipo nzuri nzuri lakini *re agancey* zinachelewa mwaka huu anasema ee, moja anafanya, kwenye namba 2 mfumo wa usambazaji dawa *reagents* na vifaa vya tiba, kutoka bahari kuu ya dawa utakuwa kila mwezi, badala ya miezi 3.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kuna kusema na kuna kutenda hapa tushazungumza mengi mwaka jana hapa, na tukatolewa ahadi nyingi sana katika maeneo hasa huu utaratibu wa mwezi mmoa hayo madawa yakifika kule, utakuwa unasimamiwa katika mafumo gani, utakuwa katika *computerize*, utakuwa na *communitor* vizuri na inaama mtu yoyote atakapo kwenda Mnazi mmoja kwenye *labor* tutahakikishiwa kuwa *reagents* zote kwa sababu nayo badawa ni ghali sana. Nitakupa mfano Mhe. Mwenyekiti, tunasema sisi *MRI* na hizi nazo wafanyiwe bure Mnazi mmoja. Lakini hii moja kufanya hapo katika hospitali za kiwaida za *private* ni shilingi 700,000 kama sio na kidogo, *difference* itakuwa ni ndogo kabisa, ukienda katika Muhimbili utambiwa shilingi 300,000 mpaka shilingi 400,000 lakini Zanzibar serikali inatoa bure, lakini hii huduma ni ghali, kwa maeneo mengine hasa tufikirie hizi fedha zote, tunasema tunatoa huduma bure, hasa mimi hapa nataka nishauri.

Mhe. Mwenyekiti, sisi Wajumbe Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuna hichi kipande, hichi chote kipande tunacho kinasema *National Health Insurance Fund*. Kipande hichi kwanini hapa tusiwe na *Zanzibar Health Insurance Fund* serikali kama ina malengo ya kutaka kufidia kwamba kila mwananchi apate huduma bure, basi serikali iwakatie bima ya afya, mtu anapokuwa na bima ya afya, ina maana moja kwa moja atakuwa anapata, hata akendea kwenye *private* anataibiwa hakuna nchi duniani itaweza kutoka *unless* katika hizo *developing country* au nchi hizi *first world nation* ambapo wana fedha za ziada ambapo bajeti zao wao, tatizo sio fedha tatizo wewe je utaweza kufanya. Sasa kama tutakwenda Bima ya Afya, tumeona katika nchi zetu za jirani kwa mfano Tanzania bara, tumeona kama nchi Botwana, *South Africa* maeneo mengine kama India maana nchi nyingi, wanatumia Bima Afya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo njia ambayo serikali itaweza kufidia ni kuwa na bima afya, na serikali kama italipia bima afya inamaana hata haya makampuni, ambayo yatakuwa yanawekea kwenye bima yatahakikisha kwamba zile huduma pia zinapatikana katika meneo, kwa mfano

angalia mahusiano ya Hospitali ya Muhimbili na pamoja na hawa *NHIF* itakuta hata mashine wanawasaidia. Sasa niombe sana na kwa mfumo wa serikali ambao unataka kwenda nao mikakati, au tuanze kupanda misingi mapaka mfumo wa miaka ya mbele, kuelekea katika mfumo wa kupaga bima afya na iwe kwa wazanzibar wetu wote, na mimi sioni sababu kwankini tutashinda kwa sababu *population* ipo, uwezo tunao, na serikali yetu ipo kawa kwa ajili ya wananchi, kwa sababu tayari tunatumia fedha nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu nyengine ninayotaka nizungumze Mhe. Mwenyekiti, ni *issue* ya Bohari Kuu na mfumo mzima wa madawa. Kwa kweli, sisemi kwamba kwa nikawanyooshea vidole watalamu wetu lakini mimi maisha yote ukisoma katika hichi kitabu. Hiki kitabu sio changu mimi Mhe. Mwenyekiti, ni kitabu cha Mhe. Waziri kuna sehemu hapa anasema kukamilisha na kuanza kutekeleza mpango wa kuwapa motisha wafanyakazi, sasa ikiwa mfanyakazi humpi motisha unatarajia atafanya nini, tunamfanyika makazi muda mrefu, maeneo ya kusimamia ni kazi mfumo mzima wa kuchukua madawa kuleta. Sasa kila dawa inayoingia Hospitali ya Mnazi Mmoja je, inatumika kwa ajili ya wananchi, kwa sababu serikali inatumia fedha nyingi sawa, inawezekana hazitoshi, lakini fedha je zinazotumika ni kidogo ni nyingi lakini hizi fedha zote zinatakiwa asilimia 99.9 na kidogo lazima zende kwa wanachi.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema mwanzo kwamba sawa tuna mahospitali yetu kama mfano mimi nina kituo cha Tunguu leo pale, ukienda kule katikia vituo vyetu wananchi bado watakuja zao Hospitali ya Mnazi Mmoja hilo elimu yenyewe haipo, watafata dawa wakiamini kama huduma ile wataipata Hospitali ya Mnazi Mmoja, hasa lazima katika mfumo tunaosimamia wa ugatuzi tunaokwenda nao elimu iende katika maeneo huko ili wananchi wetu katika wilaya na maeneo wapate, wazidi kujenga uelewa, wa kwenye masuala ya tiba, na kinga na afya zao wanapotaka kufanya, na ukiangalia kwenye hili buku.

Mhe. Mwenyekiti, humu ndani mwaka huu kwenye 2018/2019, waziri anasema kwamba katika mikakati yake elekezi kuwapeleka masomo madaktari kwa ajili ya kujiunga na fani mbali mbali za ubingwa wa kusomesha kada, adimu, *radiographer, medical imaging, anaesthetist, biomedical engeneers*, humu anaseme lakini pia kuwaajiri wataalamu wa afya madaktari, wauguzi, *pharmacia,* mafundi sanifu, dawa za maabara, *diographer, medical imagic*, hasa hawa wote, pamoja na *medical engeneers,* mambo yatakuwa mazuri, lakini nao wafanyakazi wetu watambue kwamba serikali hii ipo kwa ajili ya wananchi, imewaahidi wananchi, katika kutekeleza yale yote yaliotiwa katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sisemi kwa ni wote, mapungufu peye wengi pana mengi, naomba kwamba wajaribu kutumia lugha na kwenda katika kufanya madarasa ya semina zao, basi serikali isione tabu kuwatilia, tunaona madaktari kutoka Cuba, China, wanakuja Zanzibar lakini madaktari wetu na watu wengine wote, wauguzi, wapalekwe pia wasitoke Muhimbili wakafanyakazi Zanzibar, yaani Unguja na Pemba, wapelekwe pia maeneo mengine wakajifunze katika *exchange program* kama ni India, Botswana, Zimbabwe, na maeneo mengine wakajifunze pia tusione tabu fursa zinapokuja kuwapeleka watu wetu nje kwenda kujifunza, kwanza itasaidia katika kubadilisha mawazo yao, ee, kuwajengea uelewa, na kupata kufahamu vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia nataka niseme tu juu ya masuala ya ugatuzi kwa Wilaya ya Kati. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia Wilaya ya Kati na Mkoa wetu wa Kusini Unguja kwa upande

wa Jimbo la Tunguu, tuna *population* ambayo uhamiaji, ambayo wahamiaji wengi hivi sasa, lakini mbali ya changamoto tulizokuwanazo, mazingira ambayo wanayohamia ni wengi tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba wale ambao wanaotibiwa Zanzibar ndani ya Hosipitali ya Mnazi mmoja, kwa sababu mtu yeyote, sisemi na Ramadhani hii Mwenyezi Mungu anisamehe, sisemi kwamba mtu anapokuwa raia sio Mtanzania au sio Mzanzibari hastahiki kupata ile tiba bure, kwa sababu yeye hachangii, lakini inawezekana Zanzibar sasa tunapata chimbuko la waatu wengi sana, wanakuja kufata mahitaji ya huduma bure ya afya, lakini tunashindwa kuwatambua.

Mhe. Mwenyekiti, naomba katika mfumo huo na mnasaba huo unaozungumzwa naomba niunganishe hoja hiyo pia wazingatie na suala zima la Bima la Afya, ili kuhakikisha kwamba kila Mzanzibari atapokuwa na kitambulisho chake basi anapoto na nimuombe Mhe. Waziri alipata nafasi, ya fursa wakati alipokuwa Waziri wa Kilimo, kwenda kutembelea kwenye kisiwa cha Uzi, basi pia namuomba pia katika wilaya kati kuna maeneo kama Ukongoroni, na Charawe lakini pia katika Jimbo langu la Tunguu ende kutembelea kituo cha afya kwa upande wa Uzi, ili wananchi wale ambao wapo katika visiwa vile waweze kupata huduma na ajenge uelewa zaidi kwao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nichukue nafasi hii kujipongeza sana mimi mwenye kwa kutumia muda wangu vizuri, lakini pia ni kupongeze na wewe kwa kunipa fursa hii niseme kwamba siungi mkono hoja yote mpaka nitakapopata majibu sahihi kama nilivyoongea mwanzo, na naomba wasaidizi wako waandike, ili nisije nikanyimwa fursa wakati wakupitisha vifungu vya bajeti. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikiliza.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Simai Mohammed Said kwa mchango wako. Sasa nimwite Mhe. Zulfa Mmaka Omar, atafuatiwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said na Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali ajiandae.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi leo hii kuchangia katika Wizara hii ya Afya. Awali nianze kumshukuru Mwenye Mungu kwa kunijaalia uzimawa afya kuweza kurudi tena katika Baraza nikiwa katika hali nzuri ya afya.

Mhe. Mwenyekiti, pili nimpongeze Mhe Rais wa Zanzibar kwa imani yake aliyoilekeza katika Wizara hii ya Afya ambayo hii ni wizara ambayo anaina ni kama roho yake. Tumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar juhudi zake tunaziona na tunaona jinsi gani anaumia juu ya wizara hii hasa pale yanapotokea mabaya, na pia tunamuona ni furaha gani anayokuwa nayo pale wizara hii inapofanya vizuri kwa sababu na yeye anajua machungu ya wizara hii yote yanayouma kwa sababu ameshawahi kupitia.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze katika ukurasa wa 34. Ukurasa huu umetoa taarifa ya jengo la hospitali ya Chake Chake, hapa tumeona kwamba kuna ukarabati wa bati katika hospitali ya Chake Chake, lakini niseme tu suala la ukarabati wa jengo hili halikuanza leo wala halikutajwa leo lakini tujiulize mwaka mzima ambao ulipita je, suala hili lilichukuliwa vipi kwa sababu suala la kuvuja mimi nachukua ni suala la *emergency* na hasa maeneo ambayo yanavuja, unakuta kwamba hospitli ya Chake Chake eneo kubwa ambalo linavuja ni sehemu ya kujifungulia, na

sehemu ya *theater* pamoja na *maternity ward*. Mhe. Mwenyekiti, hapa panatakiwa kuwa pachukuliwe suala la *emergency*, lakini hapa Mhe. Waziri anayo ramani yake anatembea nayo mkononi kila siku ukimuuliza anakwambia tayari ramani nikonayo bado wajenzi kujenga. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tujiulize kweli tuko *serious* na kujenga ilie hospitali au tuko kuandika kwenye vitabu na sisi tuonekane, kwa kweli sio vizuri. Mhe. Mwenyekiti, tusimuangushe Mhe. Rais wa Zanzibar, kwa sababu anataka wizaara hii iwe ni wizara ya mfano, lakini watendaji kwa kweli wanamuangusha. Kutokana na hali hiyo, nawaomba watendaji wasimuangushe Mhe. Rais wa Zanzibar, kwa sababu wao wanaenda kula na kumdanganya, baadhi ya mambo wakienda waseme ukweli, wasifiche suala la kifo halitakiwa kuficha, hasa wewe unaacha kwamba suala la hospitali inavuja unakwenda pale unaenda pale kujifungua unaambiwa sogeza kitanda huku hapa panavuja, hebu angalia Mhe. Mwenyekiti wewe ni mzazi unaijua hali ya uzito ule unavyokuwa, lao unaambiwa kama hivi katika hali ile nzito, unaambiwa kwamba sogea huku hapa panavuja, hebu *imagine* inakuaje. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli aa! Wizara ya Afya inatuangusha, kwa sababu ni wizara ambayo inaingiziwa pesa nyingi sana, lakini tunaona utendaji wake umedorora, na umelala, tujiulize huku Wizara Afya tu watu wamelala, mbona wengine wameamka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nataka niende kwenye taarifa ya hali ya uzazi. Kwa kweli, nisipotetea hapa wazazi wenzangu sitawatendea haki. Mhe. Mwenyekiti, tunaona hapa Hospitali ya Chake Chake kuna watu wingi sana wamekwenda katika huduma ya uzazi na upasuaji, tukiacha Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo inaongoza ikifuatiwa na Hospitali ya Chake Chake, tujiulize hawa wanaokwenda Hospitali ya Chake Chake wanajifungua wapi. Wanajifungua katika hali gani.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunaenda hasa kukagua tutasema hasa ile ni *garage* ya kuweka vitanda vibobu, sio sehemu ya uzazi, kwa kweli inatilisha imani. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri, tunajua kwamba kaamua na anasimamia, lakini kwa suala hili tumwambie arudi tena aende kusimamia isiwe kama waliyopita akaanza kutembea na ramani katika mikoba yake, Mhe. tutakuja kukabana roho hapa, hatutokubali. Mwaka mwengine unakuja kupita ukajakutwambia aa! Sijui nilikwenda, nilifanya hivi Mhe. Waziri hatutakuja kukuamini tena. Hivi sasa tunakuamini na tuna imani na wewe, lakini ukiendelea kuranda na hizo ramani katika mikoba yako Mheshimiwa, imani hiyo tutakuondolea na tutaanza masuala mazito.

Mhe. Mwenyekiti, Mie naomba katika hospitali ya Mnazi mmoja, Mhe. huku kumeoza, Mnazi mmoja kumeoza, sio siri wala sio dhahiri. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa ukienda Hospitali ya Mnazi Mmoja unaambiwa vipi unakwenda *garage* kutokana na utendaji. Kwa kweli, serikali yetu inajitahidi na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango anajitahidi kuingiza pesa, wakiomba hawajamaliza ile bee, wao wameingiziwa lakini Mhe. Mwenyekiti kwa kweli aa! Sijui niseme kwamba ni madaktari, ama sijui niseme watendaji, kwa kweli huku bado watu hawapo *serious.*

Mhe. Mwenyekiti, juzi nimekwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa macho yangu, nimemkuta mtoto ambae amepelekwa *emergency* katiwa *drip, drip* ile imekamatwa kwa mkono hivi, *plaster* hamna, kweli *plaster* inahitaji kiasi gani na inahitaji bajeti gani.

Mhe. Mwenyekiti, tukitoka hapo kuna chumba pale katika jengo ambalo ni jipya, limejengwa na tulikwenda kulifungua kwa ngoma Mhe Mwenyekiti, jengo lile linanuka ni bovu halifai tujiulize zile pesa za watu zilizoingizwa pale, na zile nguvu za watu za serikali zilizoingizwa pale, zinataka kusimamiwa. Mhe. Mwenyekiti, nimeenda kuna chumba kimoja wanalazwa watoto, chumba kile watoto wanaingizwa *oxygen* na chumba kile pia kuna mashine moja ya *phototherapy* ambayo mtoto anatakiwa kwamba akiingizwa mle akiwa hana nguo, tujiulize chumba kile harufu yake ukiingia tu, ukitoka unatapika, kweli pale mtoto pale kenda kupata afya au pale kenda kupata maradhi.

Mhe. Mwenyekiti, aa! Si kweli hawako tayari, Mheshimiwa hii mashine ya *phototherapy* nimefuatilia nimeikuta mashine inauzwa shilingi 3,400,000/= watoto wanaozaliwa hivi sasa asilimia kubwa sana wanazaliwa na matatizo ya umanjano, ukishazaliwa na tatizo la umanjano, unataka kuingizwa katika mashine ile, Hospitali ya Mnazi Mmoja kuna mashine wanasema mbili lakini niliyoiona ni moja. Watoto wale mashine ile anatakiwa kuingizwa mtoto mmoja, wanachokifanya hospitali ya Mnazi mmoja wanaingizwa watoto watatu. Unaambiwa muingize mtoto weka kanga, muingize mtoto weka kanga, kwa sababu watoto wale wanaingizwa wakiwa hawana nguo na wengine wanazaliwa wana vifua vikuu, wanazaliwa wana harara ya mwili, wengine wanazaliwa afya yao kila mtu anajua afya yake, kitoto kinaingizwa mle hakina nguo, niambie pale anapata afya, anapata maradhi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kweli basi mashine ile hospitali za *private* kama *Global* na kwengine, kuna mashine 7, Hospitali ya Mnazi Mmoja kuna mashine 2, si aibu jamani kweli kitu kama hichi tunashindwa kuomba, basi afadhali tungekuja humu Baraza la Wawakili tukasema tupige *donation* tunaijua hali basi tunge–*donate* tukanunua zile mashine japo 4, lakini mashine 2 kweli tuko-*serious*, kweli tumeomba pesa omba pesa hii tukashindwa aa! Tuseme ukweli moja iwe moja na mbili iwe mbili.

Mhe. Mwenyekiti, watendaji wa Wizara Afya, bado hawako tayari kushikamana na Mhe. Rais wa Zanzibar, kuifanya Wizara ya Afya ni wizara ya mfano, tubadilike, tutaua, kila siku tutakuwa tunaua sisi, kuna vifo ambavyo Mwenyezi Mungu kaviandika haviepukiki, lakini kuna vifo tunavyovisababisha. Wizara ya Afya mnatuua. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tukitoka hapo niende Mheshimiwa, katika hapo hapo suala la afya nimeenda juzi katika kituo cha Fuoni. Mhe. Mwenyekiti, watoto pale wamekwenda kupata chanjo, wananambia kwamba wiki iliyopita walirejeshwa hamna bomba za kupigia shindano, Mhe. Mwenyekiti, dawa tunapata msaada, basi hata bomba tunashindwaa kununua, watoto waliopo pale ni zaidi ya 50, waliopata chanjo kama 20, badala yake chanjo ile baada ya kupigwa unaambiwa hivi, ile pamba ya kufutia damu hamna, unaambiwa kama hivi mtoto afutiwe damu kwa nguo ya mzazi, basi pamba inauzwa kiasi gani, pamba inauzwa tu kiasi gani.

Kwa hivyo, tunaingiza pesa katika pesa katika wizara hii, tujiulize hizi pesa zinazoingiwa zinafanyiwa kitu gani. Tusiwe waongo, tuwe wa kweli jamani, kwenye shida mtu unatakiwa uombe, basi wewe nenda kaombe, jamani wizara yangu haina pesa ya kununua pamba, basi utagaiwa lakini wewe unakaa tu huko. Mhe Rais wa Zanzibar anaona kama vitu viko, kwa sababu vinatolewa pesa, lakini mwisho wa siku vitu vile haviko. Jamani tusimdanganye Mhe

Rais wa Zanzibar tuseme ukweli, na tuwe tayari jamani, tusipokuwa tayari tutauana kila siku. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii nina hasira nayo kutokana na utendaji, hakuna kitu kibaya kama kudharau afya ya mwenzako. Mhe Mwenyekiti, wengine wanapesa wanakwenda *Global,* wale wakulima na wakwezi watakwenda wapi, hawana. Kwa mfano, hivi sasa ukitoka hapa ukienda katika *ward* ya watu wenye maradhi ya kisukari, haki ya Mungu huli siku mbili kwa uchafu, ile harufu utakayokutana nayo mle *"Allahu Akbar"* naamini hutoweza kula, tujiulize basi hasa lile suala la kusafisha linataka pesa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimekwenda hospitali mimi nimekuta kwamba usiku saa 4, *ward* ambayo wanalazwa watoto ambao wako *emergency* hao *ward* inafagiwa usiku wa saa 4, kitoto maskini kimepumzika au mama mzazi kajifungua kachoka, unaambiwa nyanyuka, nyanyuka, nyanyuka, mufagiwe usiku saa 4 asubuhi mnakwenda wapi *disco.* Mhe. Mwenyekiti, tujiulize asubuhi wanakwenda wapi. Kwa nini wanafamye kitu kama kile usiku, mzazi kachoka anataka kupumzika, leo usiku wa saa 4 unamwambia kwamba kurupuka, simama, simama mufagiwe kitu gani. Mhe. Mwenyekiti, kujenga majengo mazuri sio afya, majengo *Alhamdulillahi* tunajengewa, na pesa tayari tunatiliwa, lakini tujiulize hawa ambao wanahusika na madawa na usafi wanafanya kazi zao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi niko tayari tutoke na Mhe. Waziri, moja kwa moja nitatoka kwa gari yangu yake yeye haina mafuta twende tukaangalie Hospitali ya Mnazi Mmoja, kweli hali hali inaridhisha ya usafi, hairidhishi na ile ni hospitali ambayo inategemewa. Mhe. Mwenyekiti, hatuko *serious,* tunauana na Mhe. Rais wa Zanzibar halijui hili, kwa sababu mnamficha, mkipeleka hivi vitabu mnapeleka idadi ndogo ambayo wanaokufa si kweli hii idadi ya wazazi waliokufa na wala mimi sikubaliani nayo hii ni uongo, tena ni uongo.

Mhe. Mwenyekiti, nimekwenda Hospitali ya Chake Chake kuna mama kajifungua kwa operesheni badala ya kujifungua kaambiwa apate huduma ambayo ya utulivu kimekosekana chumba. Kwa kweli, ni jambo la kushangaza mpaka Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali amelazwa Hospitali ya Chake Chake kalazwa ndani ya chumba cha daktari kashindwa kupata *ward* nzuri ya kulazwa tujiulize tunakwenda wapi.

Mhe. Mwenyekiti, kama Pemba tunavyokujua hali yetu tunayoijua mtu unakwenda kumlaza *emergency* anaumwa maradhi mengine yanakuwa ni siri Mhe. Mwenyekiti kifo ni siri, kuna watu wanatakiwa walazwe katika *ward* ya siri tujiulize kama Hospitali ya Chake Chake mtu ana maradhi ya siri anataka kufa unakwenda kumuweka dhahiri nahiri unamuwekea lile dude la kijani wengine tukiliona tu dude la kijani tunasema basi huyu anakufa, kwa sababu hatuna uzoefu, kwa kweli sivyo. Kwa kweli, hapa tukisema kwamba tunakwenda kukarabati bati katika Hospitali ya Chake Chake ni sawa na kuchukua kidonda ambacho kimefanya gaga tukakitia dawa juu yake tunafanya nini, tujiulize tunafanya kitu gani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hii ni wizara nzito na ukipelekwa katika wizara hii ni kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar tayari kakuamini na akikuamini tukiachia waziri kuna watendaji wengine wanaohudumia mahospitali hawa nao pia hawataki kila siku mtu wende kumsukuma, mtoto wa kwenda hataki kigari, leo kila siku wanatakiwa wao kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar aende ziara

za kushitukiza, hivi Mhe. Waziri hana kazi nyingine za kufanya, anazo hebu tufanyeni kazi kwa kutegemea fungu kutoka kwa Mungu tusifanye kazi kwa mazowea. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wa Afya atumbua majipu Wizara ya Afya kuna majipu, hawafai hawa kuna taka katika wizara yake Mhe. Waziri anazifuga, yaani wanamtia tope hawa. Kwa kweli, hivi sasa hatuna imani na Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja ukienda unaambiwa wewe umekwenda *garage* umeyataka, kitu gani tunafanya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hiki kitabu sijakisoma kwa sababu najua humu mna usanii mtupu, muda ni mali, mimi siwezi kusoma kitabu kama hiki kwa sababu hapa utaambiwa sijui tutanunua sijui *DNA* sijui tutanunua nini ukija mwaka mwingine unaambiwa yale yale tunafanya kitu gani. Mhe. Mwenyekiti, siungi mkono hata asilimia zero hapa siungi mkono kubwa ninalowaomba watu wa Wizara ya Afya jamani tubadilike tusiuane. Wakulima na Wakwezi hawana uwezo wa kwenda hospitali za pesa watakwenda huko Hospitali ya Chake Chake na Hospitali ya Mkoani, jamani mbona tunafanya hivi sivyo jamani. Mhe. Mwenyekiti, siungi mkono. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Zulfa Mmaka Omar kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Sarahan Said atafuatiwa na Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf ajiandae.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushuru sana Mhe. Mwenyekiti kwa kupata fursa ya kuchangia angalau machache katika Wizara hii ya Afya. Lakini awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuniamsha nikawa salama usalimini na Ramadhan hii.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein katika jitihada zake kubwa sana za Wizara hii ya Afya ambayo kwa kweli kwa hatua moja au nyingine ametutoa tukiwa mbali sana mpaka kutufikisha hapa pamoja na matatizo yaliyopo, lakini kwa kweli amejitahidi vya kutosha ili na sisi kama wananchi wake basi tumuunge mkono katika jitihada zake za kuimarisha afya za wananchi wa Zanzibar na wengina ambao wanapata huduma hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru waziri kwa kitabu chake hiki alichofafanua jinsi ya kuweza kutoa changamoto zilizomo na kuweza kusema baadhi ya mambo ambayo mengine yanakuwa kama yameshafanyiwa kazi lakini mengine yanahitaji kufanyiwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, niunge mkono wenzangu ambao weshapitia katika kutoa hoja zao moja moja ambazo nyingine zinakuwa zimefanana na za kwangu. Naomba nianze na ukusanyaji wa takwimu, katika takwimu niliyoiona humu ni takwimu ya UKIMWI ambayo kwa Zanzibar bado iko chini ya asilimia moja, lakini sasa hivi tunakufa kwa maradhi yasiyoambukiza lakini mimi katika kusoma humu kwenye kitabu sijaona watu wanakufa kwa asilimia ngapi kwa maradhi ya sukari, maradhi ya figo, maradhi ya shindikizo la damu na mengine mengi humu sijaona takwimu yake tunakufaje, lakini ninavyoona ni kwamba maradhi haya yanatuua zaidi kuliko maradhi ambayo tunayapatia kipaumbele maradhi ya UKIMWI sijui kwa sababu, niliona sana kuna maambukizo lakini vifo vyake vya UKIMWI ni vichache kuliko vifo vingine.

Sasa nimesema sana kuangalia katika takwimu nikaona kwa sababu tunapigia kelele sana mambo ya UKIMWI tumeyasahau haya maradhi mengine ambayo yanatuua kwa kasi sana. Kwa hivyo, ningemuomba waziri kama ana takwimu ya maradhi sukari, maradhi ya moyo, maradhi ya presha ya figo kama ana takwimu atakapo kuja atwambie tunakufa kwa asilimia ngapi sasa hivi maana yake ni kasi kweli kweli na maradhi haya mpaka sasa hivi hayajulikani chanzo chake nini.

Mhe. Mwenyekiti, niliona humu kwamba anazungumzia kuhusu habari ya kutoa elimu, lakini maradhi haya ya sukari na mengineyo zamani yalikuwa yanakuja kama ni uzawa, sasa hivi si uzawa wala si mpaka uwe na tumbo wala si uwe mrefu au mfupi wewe utapata maradhi haya ukiwa mchanga ukiwa mdogo sijui yanatokana na sababu gani lakini mpaka sasa hivi maradhi haya kwa Zanzibar yameshika kasi sana na Kansa lakini hatujui sababu zake ni zipi, kwa sababu ni maradhi yanayotuua kwa kasi. Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kama atakuwa na takwimu na kujua ni sababu gani, basi atuambie siyo kutoa elimu kwa sababu elimu ya hapa ni kama elimu ya UKIMWI ambayo unafanya hiki unafanya hiki lakini sukari wewe ukila usile maradhi haya unayo sasa sijui sababu yake nini na yanatuua kwa kasi sana. Kwa hivyo ningeomba hilo liangaliwe.

Mhe. Mwenyekiti, kuna sababu kubwa ambazo nyengine zinatuathiri zamani ilikuwa mabwana afya walikuwa wanapita kwenye makaro, wanapita kwenye vyoo vya majumba wanapita kwenye mito kuua wadudu wa kichocho au vitu gani, tunapenda sana kudharau tunadharau baadhi ya mambo baadae yakiripuka yanakuwa makubwa sana. Kwa hivyo, maeneo haya ambayo yanazalisha matatizo mengi ambayo baadae yanakuja kuwa ukitoka kisonono unakuja kupata matatizo mengine kwenye mambo ya mikojo na mambo mengine ukubwani, basi ningeomba Mhe. Waziri suala hili la mambo ya ugatuzi basi akatutolea mfano kwamba hawa watu ambao watapita majumbani siyo kwamba ukachukue dawa hawa ni kupita majumbani ukitaka usitaka ukafungua choo chako pamoja na karo ukatiliwa dawa, ningeomba hili kwa sababu matatizo madogo lakini athari zake ni kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nimeona sana takwimu za upasuaji ukiachia Mnazi Mmoja basi hospitali inayofuata ni Hospitali ya Chake Chake, nayo ina upasuaji mkubwa lakini ukiangalia mtu aliyepasuliwa Chake Chake hiyo hospitali yenyewe akatoka salama basi ni ubingwa wa madaktari, kwa sababu vifaa vyake havikidhi haja za mtu ambaye anakwenda kupasuliwa. Lakini pia Hospitali ya Chake Chake naisemea sana kwamba ni hospitali kubwa inayotumiwa na watu wengi sana ukiachia Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hospitali ya Mnazi Mmoja ilikwishawekwa hospitali ya rufaa, mabilioni ya fedha yanapelekwa pale lakini na Hospitali ya Chake Chake ni hospitali ambayo inatibu wagonjwa wengi sana lakini pato lake haliingizwi vile inavyostahiki inafanywa kama hospitali ya wilaya.

Mhe.Mwenyekiti, ningesema sana kutokana na uwezekano wa hali ya wagonjwa wanavyozidi na *population* ya watu wa Zanzaibar, sasa hivi katika kisiwa cha Pemba namuomba Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein amefanya jambo kubwa sana kuijengga Hospitali ya Mkoani katika kiwango kikubwa sana. Mimi niseme tu kwama Hospitali ya Mkoani haifai kuwa hospitali ya mkoa nayo ingepandishwa ikawa hospitali ya rufaa kwa upande wa Pemba kwa sababu ile hospitali iko ya kisasa na Dkt Ali Mohammed Shein ameonesha mfano mkubwa sana.

Vile vile, Hospitali hii ya Chake Chake kutokana na idadi ya watu inayochukua basi ingalipandishwa kuwa ni hospitali ya mkoa na ikapatiwa hadhi yake ya kimkoa. Lakini hospitali hii mwaka jana katika jumla ya mambo niliisemea sana kwamba upauaji wa bati itakuwa ile hospitali hatujaitendea haki, ile hospitali ilikuwa ijengwe ghorofa kutokana na eneo lililopo na tayari fedha zimeshatengwa kipindi kile karibu milioni mia nne na kuendelea tukasema kwamba hii hospitali ijengwe ya ghorofa ili iweze kukidhi haja za maeneo ya pale.

Kwa hivyo, sjui suala hili la ujezi wa ghorofa kwa Hospitali ya Chake Chake limefikia wapi, kwa sababu nilisikia mpaka udongo pamoja na mambo mengine yote tayari lakini sijui limefikia wapi. Kwa hiyo, naomba hospitali hii nayo ikatizamwa kwa jicho kubwa sana ili kuangalia kutokana na hadi na mambo ambayo inachukua.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba pamoja na Wakuu wa Wilaya zake. Hospitali ya Mkoa wa Kusini Pemba umekusanya damu nyingi sana ni ya kupigia mfano kwa miji midogo kama ile lakini ikakusanya damu nyingi wakiwa chini ya uongozi wa Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba lakini pia na Wakuu wa Wilaya walifanya kazi nzuri kukusanya damu. Kwa hivyo, ni damu nyingi sana ilipatikana ingawa muda sina lakini katika ukurasa wa 68 damu iliyopatikana kuna *unit* nyingi sana kwa hiyo niseme tu kwamba wamepata mafanikio makubwa sana, lazima na hali kama hiyo tuweze pia kuitolea mfano kwamba kumbe tukitaka tunaweza kufanya jambo kama hili.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti naomba hizi hospitali au mradi huu maalum wa damu usichoke kuendeleza kuweza kutoa hii iwe kama taaluma fulani ya kuchagia damu kwa kuwaokoa watu wetu ambao wanapata matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Hospitali ya Mnazi Mmoja tuliipitishia hapa kwamba iwe hospitali ya rufaa, hii hospitali itakuwa na vigezo vingi sana sijui imefikia wapi rufaa yetu, kwamba hii imekuwa hospitali ya rufaa vigezo vyake vimefikia wapi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja nikimaanisha kwamba nitazuia fungu, kwa sababu nataka nipate ufafanuzi kwa hivyo naandika kabisa nisije nikaambiwa humo kwenye jina nataka nihakikishe Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja imefikia wapi.

Nikiendelea na mchango wangu, sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la Bima ya Afya, tunajenga taaluma hii ya Bima ya Afya lakini bima hiyo ya afya ipo na hospitali nyingine ambazo zimechanganywa na za serikali, bado katika upande wa serikali hatujajipanga na Bima ya Afya, kwa sababu tunakorogana mule kwa mule aliyekuwa ana bima aliyekuwa hana haijulikani mwenye pesa nani asiyetoa pesa nani. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri watu ambao watahitaji bima ya afya ya serikali, basi na serikali ama ingetenga hospitali au ingetenga maeneo maalum ikawa siyo mbadala wa kushirikiana mle ndani ikawa mmoja anapata huduma ya bima mmoja hapati huduma wakati wote ni wananchi ningeomba sana hili suala likatoa ufafanuzi kwamba bima ama tukafuta kabisa kwamba bima ya afya isiwemo katika hospitali ya serikali ama tutenge hospitali ambazo zitakuwa na bima ya afya na itakuwa ni mjadala wa kuweza kusaidiana.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nataka nizungumze kuhusu tiba asilia, Wizara ya Afya imejipanga vipi, humu ukipita mitaani utasikia kuna dawa za tabibu zimetoka kwenye kuruani kuna dawa

nyingine za hawa wenzetu wanaotia ubani kuna watu wengine dawa za kila aina. Mhe. Mwenyekiti, hizi dawa baada ya dawa kumalizika zinarudi tena kuja hospitali baada ya magonjwa mengine kutokezea sasa dawa za kisuna je wametoa leseni wanawajua hao wanaotibu suna wanajulikana vipimo vyao vinajulikana na ni kweli hayo madawa wanayotumia ya suna wanatumia asali wanatumia kitu gani au wewe unachanganyiwa kwa sababu unaumwa utakula tu maana unaambiwa wewe ukiwa unaumwa utakula chochote.

Sasa Wizara ya Afya ndiyo yenye dhamana ya kututengea sisi kwamba wagonjwa musinunue dawa za suna au kanunueni kwa mtu fulani tumehakikishana nae au zile dawa mbadala nyingine ambazo zinakuwa kama za vijiti nyengine siyo za suna lakini za vijiti vijiti tunazopewa huko mitaani, kunywa maji kunywa vijiti kunywa kitu gani sasa hizi dawa je wizara inafanyaje kuhusu watu hawa wanaendelea na kama wanaendelea wao wana-*organize* vipi. Kwa hivyo, ningeliomba hilo pia wakaweza kutuangalia.

Mhe. Mwenyekiti, pia jengine nilisikia hapa kuwa kuna hospitali za *cottage* moja wapo ikiwa ni Hopspitali ya Vitongoji ni mara ya kwanza Hospitali ya Vitongoji ilishatubeba katika kufanya ukarabati wa hospitali ya chake chake na hivi sasa Hospitali ya Chake Chake ama itajengwa ya ghorofa ama itapauliwa itakuwa ina kasoro, hospitali tutakayotegemea kwa Chake Chake Hospitali ya Vitongoji hii hospitali tayari ina vigezo vya kuweza kubeba Hospitali ya Chake Chake na kama bado umejipanga vipi kuweza kubeba kwa kipindi ambacho itafanyiwa ukarabati hiyo Hospitali ya Chake Chake.

Mhe. Mwenyekiti, kuna madaktari bingwa sana umesema hapa, kuna madaktari wazalendo, kuna madaktari wa kila kitu lakini miaka ya nyuma pamoja na kila sekta kulikuwa na daktari bingwa mmoja kutoka nchi ambazo yale maradhi yapo, hapa juzi tu nimesifiwa sana nikaambiwa hapa kuna Mheshimiwa keshakatwa nyama ya macho mara tatu nyama inarudi mpaka inafunika jicho lakini hivi karibuni amekwenda kufanyiwa na mchina na hao madaktari bingwa wanasema nenda kafanyiwe na mchina, alipofanyiwa na Mchina haikurudi tena kwa sababu wanatia *cover* wanayapanga kwa sisi hao madaktari bingwa hamuwafundishi hiyo kutia kava mpaka irudi kila siku.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti nataka nikwambie kuna haja ya kila sekta pamoja na kwamba tuna madaktari bingwa basi zile nchi ambazo zinatu-*support* basi tuombe madaktari bingwa wawepo hapa kama *adviser* wetu wa kuwasaidia tena wale madaktari wetu ili kupata uwezekano wa kuweza kuangalia hiyo hali. Kwa kweli, kama ninavyosema kwamba mtu yeyote afya ndiyo kitu cha kwanza na bila ya afya mtihani.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, unazo dakika tatu nakuomba umalizie.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Lakini nimeona humu kwamba wamefukuzwa madaktari. Kwa kweli, naku-*support* sana madaktari waliokuwa hawana utu wala hawana imani na nchi hii pamoja na watu wake wewe fukuza wala usiulize na sisi tutakupa *support.* Kwa kweli, ukiachia mshahara daktari na mwalimu anapewa mafungu mawili badala ya fungu lake lile la kulipwa na Mwenyezi Mungu huyu hamuachi anamlipa fadhila kubwa sana, kuna madaktari wengine hawajifahamu kwamba msaada wake haupotei anausubiri kesho akhera

Mwenyezi Mungu akijaalia anakwenda kumlipa pamoja na Mwalimu lakini yeye anaona kama hakupata chochote hapa ndiyo haiwezekani.

Mhe. Mwenyekiti, jengine matatizo mengi sasa hivi yanatokeza hasa kwa mbwa vichaa, zamani ilikuwa ikifikia muda kama mbwa wa porini wamezidi wanauliwa sasa kama mbwa hawa wamekuwa wana maradhi ya vichaa mambo mawili tuangalie, wengine kama wanauzika tufanye mpango wa kuwapelekea wenzetu wanaokula mbwa ili tupunguze lakini wengine wawe wanafungwa na wenyewe hilo lingesaidia sana.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nizungumzie Hospitali ya Mkoani, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein pale amefanya jambo kubwa sana. Tunashindwa kuliweka slogan moja kubwa sana linalopeleka maendeleo ya hospitali katika Hospitali ya Mkoani likawa linazungushwa na Dkt. Shein na ile hospitali ya mkoani ikawa kama kioo kimoja kikubwa sana, hana hata jina pale baada ya Abdallah Mzee Hospitali hakuna kivutio chochote. Nchi za wenzetu Mhe. Rais akifanya jambo kubwa sana pale juu wekeni nembo yake kila anaepita amjue nani yule atamaliza muda wake akimaliza muda wake mpaka mtu anauliza kajenge nani hii basi mtu akipita tu akiuliza yule nani atajibiwa yule alikuwa fulani. Kwa hivyo, ningeomba pale likawepo *slogan* moja kubwa ambalo Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ile ni nembo yake amefanya jambo kubwa sana si la masihara katika mambo yake.

Mhe. Mwenyekiti, basi niangalie katika kutoa hoja zangu lakini naunga mkono hoja na kama kutakuwa na ufafanuzi uliokuwa kidogo haujaniridhisha basi nimeshasema nitazuia fungu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Suleiman Sarahan Said kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohammedali atafuatiwa na Mhe. Nadir Abdullatif na Mhe. Hidaya Ali Makame ajiandae.

Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii sote tukamshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa pumzi ya kuweza kufika katika Baraza lako na wale waliokuwepo nyumbani waliokuwa na hali yao, Mwenyezi Mungu katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani awape afya nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Afya pamoja na watendaji wake wote kwa hotuba hii ambayo wametupa hivi punde pamoja na kamati nzima, bajeti ya Wizara ya Afya ni bajeti ya uhai wa wananchi mimi kwanza nimpongeze waziri aliyetangulia Mhe. Waziri wa Afya Mahamoud Thabid Kombo, nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar vile vile kwa kutuletea waziri wa Afya Mhe. Hamad Rashid ambae ni waziri msikivu kama alivyomtangulia mwenzake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu, Madaktari wote wa visiwa vya Unguja na Pemba, *nurses* na kazi wanazokabiliana nazo katika hili, hatuwezi kukimbia muangaza na ninachosema mimi changamoto tuliyoiona inatukabili sote sisi viongozi wananchi na watendaji. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hapa aliposoma katika *challenge* ambazo

zinakabiliana na Wizara ya Afya kuanzia *page* 121 hadi 126 na mambo mengine ya jumla kwa pamoja na bajeti hii.

Kwanza niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuipa umuhimu sana Wizara ya Afya kupitia Baraza lake la Mapinduzi. Kwa kweli, ni jambo ambalo sote hatuna budi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Uzini kwa kumshukuru yeye akiwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuweza kuona hali halisi ya hii bajeti ya Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nisaidie mambo mawili mpaka matatu kwa ushauri na tatizo naliona lipo lakini tatizo tunaweza tukalitatua kwa pamoja, hakuna tatizo lisiloweza kutatuliwa, katika bajeti hii Mhe. Waziri alitwambia hapa Serikali kupitia Wizara ya Afya imetenga 12.6 *billion* kwa mwaka huu wa 2018 *Alhamdullilahi*. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Waziri alisema ni jambo la kihistoria haijapata kutokea bajeti kama hii ya dawa ya 12.6 *billion*.

Mhe. Mwenyekiti, sina utaalam lakini mimi ni mdau mkubwa sana katika kusaidia Wizara ya Afya kwa miaka thalathini hizi pesa ni nyingi sana na kama tutakuwa waangalifu watendaji katika Wizara ya Afya hizi pesa zitatutosheleza, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutakuwa na *surplus* ya madawa kwa pesa hizi 12.6 *billion*. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti naomba umefika wakati hii nchi yetu sote tuna uchungu na nchi sote tunapenda nchi, hapa tupo kwa niaba ya wawakilishi wanaoiwakilisha Zanzibar katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, kama pesa hivi zitasimamiwa 12.6 zikanunuliwa madawa kwenye viwanda *with quality and price* naamini Zanzibar mwaka huu kwa Wizara ya Afya tutaondoka na matatizo yote kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, kama tutakuwa *very serious* na 12.6 *billion* nataka niwaombe watendaji kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu waliojaaliwa kununua madawa haya wanaohusika tuache kununua madawa kwenye sehemu ambazo sizo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafahamu na mtaalam nimezaliwa Mjimkongwe naelewa inatolewa tenda inapewa kampuni ya Dar-es-Salaam, kwa sababu wakati mwengine wizara inataka mabati elfu wanakuja kwa mfanyakabiashara mfamasia hapa wanachukua kwao, wanamwambia bwana ee tupe bati elfu za vidonge. Kwa hivyo, ninachotaka kusema mimi nashauri kwamba hizi fedha na Serikali ya India kuptia Waziri Mkuu Mzee wetu Mhe. Narendra Modi tunaweza tukazalisha hata mambo mengi katika pesa hizi. Kwa maana hiyo, ninachoomba serikali kupitia Wizara ya Afya wawe wasikivu ili haya malalamiko yaliyotoka naamini yataondoka.

Kwa kweli, najua Mhe. Mwenyekiti kila mmoja anapenda ana uchungu na nchi. Kwa hivyo, naamini pesa hizi kama zitatumika viwandani *with quality and price* pesa hizi ni nyingi sana na historia, kwa hivyo lawama ile ya visiwa vya Unguja na Pemba na vituo itaondokana kama pesa hizi tutakwenda vizuri. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa duniani viwanda vipo kwa nini tuende *third part* au *fourth part* kwa kutaka kitu kighali. Kwa mfano, dawa hii omba India sehemu nyengine England leo wana *subsidise* ukinunua kwenye viwanda India, Ujerumani na sehemu nyengine wakishakuona kama Zanzibar wana *subsidise they give the discount*.

Sasa hiyo utaalam haitaki unataka moja kwa moja wende kwenye mtandao uagize kiwandani serikali ipeleke pesa moja kwa moja kwenye kiwanda, tunao marafiki zetu wengi kama vile

India, England, Ujerumani, China na sehemu nyengine *with quality and price*. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa ni hilo ambalo nimeona nilitolee mchango wa pesa hizi ambazo zinaweza kusaidia na kuondosha malalamiko.

Lakini jambo la pili Mhe. Mwenyekiti, serikali imekuwa inatumia pesa nyingi sana katika kuwasafirisha wagonjwa unajua kila mmoja na mitihani ya Mwenyezi Mungu. Lakini naomba kutoa mawazo pesa tunazotumia Wizara ya Afya kwa kupelekwa wagonjwa nje ni pesa nyingi sana. Sasa kwa ushauri wangu Mwenyekiti, mimi Mwenyezi Mungu aliponiletea mtihani wake na amesema atatuletea kila aina ya mitihani, ugonjwa, maradhi, mali kila kitu lakini mwisho katwambia wapeni habari nzuri wanaosubiri.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana mimi nilipokwenda *Saifee Hospital Mumbai* kuna ndege kumi kwa siku nilikwenda kujua hali yangu ya afya mimi mwenyewe. *Saifee Hospital* wana sehemu wanaita *VIP* nimechajiwa dola mia nne tu, yaani nimetizamwa kuanzia nywele yangu inakwenda vipi, inatembea vipi mpaka mguu kwenye kidole cha gumba *Saifee Hospital Mumbai* ndio waliojua tatizo langu la maradhi yangu ya moyo na nimelipa dola mia nne hiyo ni *VIP*. Sasa tuondokane na sehemu hizi za Chinai sehemu hizi za *deal* lazima tutafute hizi pesa tunazozipata kama sehemu hizo nyengine tutatumia wagonjwa mia. Kuna sehemu nyengine za Mumbai mahospitali ya kisasa pesa hizi hizi tunaweza kuwatibu wagonjwa mia tatu, sasa lazima tuwe waangalifu katika masuala ya pesa, tusikae tu kuna sehemu Chinai unaambiwa dola elfu tano au sehemu nyengine tutizame Mumbai ni sehemu ya kwanza Mhe. Mweyekiti ndio inaongoza kwa madaktari.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi Mohammedraza dola mia nne nime-*charge* kila kitu kuanzia asubuhi unaingia unatoka saa tisa ya mchana, *break fast* unapata mle mle, *lunch* unapata mule mule na wanakupa ripoti yako yote na *DVD*. Kwa hivyo, naiomba Wizara ya Afya tutizame hospitali nyengine hizi zilizokuwa karibu na zilizokuwa na ahuweni ili pesa zile tulizokuwa nazo ambazo ndio za walipa kodi, kwa hivyo kama kuna sehemu tutizameni hizi. Kwa mfano, twendeni *Saifee Hospital* kuna madaktari wengine wanaweza wakawasaidia tukaepusha matumizi ambayo yasiyohusika, pesa hizi hizi badala ya wagonjwa mia tukatumia wagonjwa mia tatu. Mhe. Mwenyekiti, hilo kwa Wizara ya Afya napenda kutoa ushauri huo.

Jambo la tatu Mhe. Mwenyekiti, wenzetu wanataka kutusaidia. Mhe. Mwenyekiti, nataka niwaambie tu Wizara ya Afya naomba kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tuna madaktari wazuri, tuna wataalam wazuri, utendaji mzuri, mwaka huu alikuja daktari bingwa duniani anayeongeza Dkt. Ramakanta Panda wa Amsterdam kwa bahati alipokuja Zanzibar nilimualika mimi alikutana na Mhe. Waziri wa Afya, wakati huo anaitwa Mahamod Thabit Kombo. Mhe. Mwenyekiti, daktari yule alivyoipenda ile jina la Zanzibar tu alivyoipenda aliiambia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Waziri wa Afya tena kuwa na *Press Conference* kwamba anataka madaktari wanne, apelekewe kwenye hospitali yake ambayo ndio inayoongoa kwa dunia ya moyo akawape wataalam kupata majaribio na kufundishwa bure isipokuwa pale wapate tiketi na sehemu.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, tuna neema kubwa sana daktari bingwa Duniani Dkt. Ramakanta Panda kaja Zanzibar na kasema nipeni watu wanne atawafundisha yeye. Sasa naomba tu Mhe. Mwenyekiti, najua Wizara ya Afya ina mambo mengi lakini panapokuja bahati kama hii hapa Wizara ya Afya ilizungumza bajeti ya kupata wataalam, ya kupata mambo gani.

Lakini kuna mambo ambayo yanapatikana lazima tuwe tunayafuatilia na Mhe. Waziri wa Afya namshukuru alimwita tena ilikuwa siku ya Jumapili kalala nyumbani kwake nikenda nikamuomba kaja kafungua wizara akaamka saa tano, hakutosheka hapa akasema Mhe. Mohammedraza tufanye *Press Conference* kazi ya Wizara ya Afya serikali na Dkt. Ramakanta Panda hospitali yake kukaweko na *Press Conference official*. Lakini leo *astaghafirullahi* sijui pengine hata hizo kumbukumbu hazipo. Kwa hivyo, naombe tu watendaji naamini Katibu Mkuu ni mtu msikivu sana na ni mtu ambae mama namuelewa nimefanya naye kazi Bi. Asha kwa hivyo washirikiane na hili ni letu sote.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba Wizara ya Afya katika masuala muhimu tuna vituo vingi vya afya katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi jambo zuri. Kwa hivyo, naiomba Wizara ya Afya tunapokuwa na vituo tumejiandaa kuvijenga na kuvifungua angalau tuhakikishe tuna wataalam, tuna *nurse* au daktari najua hali yetu ya serikali. Lakini tunakwenda kukimbilia vituo madaktari hakuna, wakati mwengine *nurse* hakuna. Kwa hiyo, niwaombe Wizara ya Afya tunapojiandaa kutengeneza kituo au kwenda kufungua tuhakikishe tuna madaktari wa kuweza kusaidia hili.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri kwa serikali kupitia Waziri wa Afya na hili Mhe. Mwenyekiti, naliomba sana leo lazima tuwe na utaratibu wa kutoa wafadhili akina-Raza, wafanyabiashara akina-Raza wafadhili akina-Raza wanapotaka kutoa misaada ya madawa na vifaa lazima waishirikishe Wizara ya Afya, kwa sababu hapa Zanzibar kumekuwa kama genge, kwa mfano ninaweza kutoka Mwakilishi nimepewa madawa yameshamaliza muda wake nakwenda kuwasukumia watu wa Uzini bila ya kujali, bila ya kumjali Mwenyezi Mungu vitu hivi vinafanyika Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, naiomba serikali kupitia Wizara ya Afya iwataje wadau kama Raza katoa vifaa sivyo ambavyo havina *quality* isemwe, sasa hatuwezi leo Mhe. Mwenyekiti wanatoka watu nje wanatuletea vitanda au *used* hujui vitanda vile hapa hatuna soko, tumefanya mapinduzi yetu kwa kujiletea maendeleo bora tule sembe tujiamulie mambo yetu, lakini hatuwezi kukaa Wizara ya Afya ikaa inakamata madawa yaliyokwisha muda wake, inakamata vitu vilivyokwisha muda wake halafu yule mtu anakwambia mimi nilikuwa sijui.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana na hilo nawaambia Wizara ya Afya *Wallahi* mtabeba jukumu kwa Mwenyezi Mungu fimbo ya Mungu haina sauti, kama unahisi wewe umemlinda yule mfanyabiashara au unahisi wewe yule umempendelea kwa sababu mkereketwa kwa sababu ya kada wa Chama cha Mapinduzi *Wallahi* jambo hili litakufika wewe mpaka na watoto wako, haiwezekani madawa yamekwisha watu wanasambaza kwenye sehemu zao wizara haijui, bora tule ugari tule seme ndio hii tuliyokuwa nayo sisi na Mhe. Rais wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohammed Shein hapa. Nchi yetu hii tunajiamulia mambo yetu wenyewe leo tuna raha humu ndani *alhamdullillahi*, lakini ndio nasema siku zote tusikimbie muangaza, huwezi kutafuta mwezi bila ya kutizama nyota tafuta nyota ndio uone mwezi.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana Wizara ya Afya tusikubali kupokea na vituo hivi vilivyokwisha muda wanajua, kuna wengine wanabadilisha *packing* hawa watu wa kupandishwa tu kwenye vyombo vya sheria. Namshukuru Mhe. Rais wetu wa Zanzibar juzi tu katoa hotuba nzuri kwenye mwezi Mtukufu wa Ramadhani ametoa hotuba ya kutunasihi sisi wafanyabiashara, enyi

wafanyabiashara waoneeni huruma wananchi jitahidini musiuze vitu ambavyo sivyo, leo anakuja mtu Wizara ya Afya iko pale mtu analeta mchele umebadilika rangi halafu anasema yeye hajui, hivi vitu viko vingi sana lakini wanaoumia ni wanyonge sisi watendaji humu sote tunakwenda kujitibu nje. Lakini tusimsahau Mwenyezi Mungu haiwezekani mtu kafika nenda kwenye vyombo vya sheria funga kamata kama sheria hazisemi tuleteeni sheria hapa tutengeneze hizo sheria naamini Waheshimiwa Wawakilishi wote hawa wataitekeleza sheria hiyo.

Kwa kweli, haiwezekani mtu mfanyabiashara Raza analeta kitu sicho anafahamika kwa sababu ya mkereketwa unaua umma, haiwezekani Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, naiomba sana Wizara ya Afya inapopokea vifaa itizame tathmini, itizame *quality* sio mtu anakwenda kununua vidonge tu anasema mimi napeleka jimbo la Uzini aala! Hapa kuna Wizara ya Afya, kuna wataalam, kuna wanaohusika dawa gani nenda Wizara ya Afya utapata. Kwa hivyo Wizara ya Afya ni jambo muhimu lakini tusikae tukalindana, maana yake kuna wengine huko nje wafadhili mimi hivi karibuni nilikuwa nje ya nchi nilipewa karibu kontena tano za vifaa vikongwe na magodoro, nikawaambia aaa! Nchi yetu sisi haina janga hilo nilikataa, sasa tusitafute tu watu wanakuja wanaleta mizigo halafu tunatafuta kamera mtu anasambaza kitu ambacho hukijui kimetokea wapi.

Kwa hivyo, naiomba sana serikali itoe tamko Wizara ya Afya na hizi *dispensary* zote zilizokuwepo lazima zifanyiwe tasmini, lazima zitizamwe hatukatai lakini lazima tuwe wakweli jembe ita jembe na pauro ita pauro. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, hivi vifaa vya afya, chakula na madawa lazima tufike pahala tuseme hapa tumefikia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, umebakiwa na dakika mbili.

Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali: Dakika mbili Mhe. Mwenyekiti. Kwa hiyo, basi mimi niitakie kheri Wizara ya Afya na niombe hii bajeti ambayo iliyokuja hizi fedha zilizotengwa ziende kwenye *swiratwamustakim* wananchi wafaidike, sote tufaidike na yale ambayo watu ya kusameheyana basi tusameheyaneni tusongeni mbele, maana ukiyatizama ya nyuma hatufiki.

Kwa hivyo, nimuombe basi Waziri wa Afya ni mtu ambae namuheshimu sana ni mzee wangu baba yangu Mhe. Hamad Rashid pamoja na watendaji wote Makatibu Wakuu. Vile vile, namuomba Mhe. Waziri wa Afya kama kuna posho za madaktari au jambo lolote ambalo hawajalipwa, naiomba sana Wizara ya Afya ibane matumizi yake ilipe mafao ya madaktari kama ipo kwa vituo vyote vya Unguja na Pemba, ionewe huruma katika mwezi huu mtukufu tubane matumizi mengine ili tulipe hizo posho a *over time* za madaktari wote wa Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wanachi wa Jimbo la Uzini na kwa niaba ya Baraza hili nililoletwa kutekeleza ilani ya chama, naiunga mkono Wizara ya Afya kwa asilimia mia moja, ahsanteni. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali kwa mchango wako. Sasa naomba nimuite Mhe. Nadir Abdul-latif Yusuf atafuatiwa na Mhe. Hidaya Ali Makame, na Mhe. Omar Seif Abeid ajiandae.

Mhe. Nadir Abdul-lafif Yssuf: *Bismillahi Rahmani Rahim* Mhe. Menyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Afya Mhe. Hamad Rashid kwa mwaka 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, nitachangia machache ambayo nayafahamu kutokana na kwamba sio mzoefu wa wizara ya mambo ya afya kama nilivyosema wizara iliyopita Wizara ya Kilimo sina uzoefu na Wizara ya Afya vile vile sina uzoefu sana, bali nitazungumzia wananchi wangu pamoja na mambo ambayo nayaona na yale ya kutoa ushauri.

Kwanza nimpongeze pia Waziri aliyoondoka Mhe. Mahamoud Thabit Kombo kwa kuweza kusimamia kituo cha Chaani Kikombeni, kuweza kujengwa upya na kikawa kituo makini na kisafi na cha kisasa na anatarajia sana kwamba madaktari vile vile, watakuwa wakisasa na madaktari wazuri watoweza kutoa huduma nzuri kama kituo chenyewe. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Mwenyekiti, lazima tuwe wawazi Wizara ya Afya kwa muono wangu mimi hata wapewe mawaziri kumi waendeshe wizara ile, kwa muda huu Zanzibar watu watendaji walivyo baadhi yao basi hawatoiweza. Mimi binafsi nipewe mimi na Mawaziri wengine wanisaidie Wizara ya Afya kuiendesha tabu Zanzibar, kwa sababu bado hasa *target* yenyewe inayotakiwa hasa kwenye masuala ya fedha na masuala ya kukamilisha vifaa na mambo mengineyo na madaktari bado *level* ile haijaweza kufikiwa bado kutokana na uchumi wa nchi.

Sasa nimpongeze Mhe. Waziri kwa jitihada zake alizoanza nazo na nguvu yake anaanza nayo, maana yake si kama namsifu mimi tu, na Ramadhani hii lakini hata watu wanasema waziri kaanza kazi vizuri kama alivyoondoka mwenzake na yeye kaanza mara mbili yake, ili kuona kazi inakwenda. Na naweza kumsema kwamaa waziri huyu ambaye ameteuliwa nikiangalia ni chama chengine kabisa katoka ni mpinzani kwa ufupi kutoka kwetu sisi, lakini kazi anayoifanya utafikiria ni mwana-CCM anafanya kazi *kihakililahi* kusema la ukweli na hii nimpe pongezi vile vile, Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) akisimama hapa anajua anaongea nini, anaongea maana na anafanya kazi ya maana. Nampongeza sana hawa ndio viongozi mawaziri hawa wawili ambao ni wapinzani nawapongeza sana kwa kazi wanazozifanya. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Mwenyekiti niende kwenye suala hospitali kwa ujumla, naomba kumpongeza sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa mambo yote ambayo anajitahidi kuweza kutoa fedha, maana yake ukitaka tusitake Mhe. Rais yeye hawezi kwenda kufanya kazi za chini kwa mujibu wa sheria. Yule ni kiongozi wa nchi, serikali, wizara inataka fedha inataka majengo inataka vifaa yeye anaidhinisha anakaa anashauri, anawapatia na hili tunaliona, analifanya kwa asilimia 100 kwenye suala la afya kuwapatia wanachotaka.

Lakini majengo sasa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo yako chini ya serikali yetu ukiangalia mengine mazuri mengine si mazuri, hali kama walivyoeleza Waheshimiwa Wajumbe

wenzangu waliozungumza si kama wanamuonea Mhe. Waziri au wanaonea wizara ni hali halisi baadhi ya sehemu nyingi ipo, ningekuomba sana Mhe. Waziri na *cabinet* yako nzima kwamba muhakikishe kwanza jambo la mwanzo usafi ndani ya maeneo yote ya hospitali za Zanzibar pamoja na huduma nzuri kwa wananchi, kwa sababu anayeenda kutibiwa sasa hivi kwenye hospitali za serikali ni wanyonge ambao hawana uwezo.

Hakuna mtu hata mmoja ambae hana uwezo akatibie *Global* wakati *CT-Scan* sijui laki mbili, sijui laki tatu, leo igharibike Mnazi Mmoja *CT-Scan* siku mbili tu wanaipata pata watu wanyonge taaban, wangine wanafika hata kupata vifo ambavyo pengine havijaandikwa mimi siwezi kuzungumzia kitu kama hicho. Lakni *CT-Scan* anaambiwa kafanye hana uwezo, sasa hii nikasema tuone pia umuhimu wa serikali kupitia Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kwamba machine zile za ghali zinatolewa bure, na ningeomba machine hizi angalau kupitia wizara yako ziwe angalau tatu tatu zisiweko moja wala mbili, kwa sababu mnaowatibu ni wananchi wingi watu wenye uwezo watakwenda *Global* watakwenda *Al-Rahman* na sehemu nyenginezo.

Mhe. Mwenyekiti, pia niwahakikishie kwamba hakuna hospitali hata moja Zanzibar ya *private* ambayo itaweza kufananishwa na hospitali ya Mnazi Mmoja kihuduma kiutaalamu na kwa vifaa. Hizo hospitali zote hata hao madaktari wanaazima kutoka serikalini, madaktari ambao wanatumia hospitali za *private* wanaanzima serikalini, serikalini tuna madaktari wazuri tuna *management* nzuri ya wizara tuna viongozi wazuri, lakini kama hamjawa wakali kuhakisha mna dili na wanaoharibu masuala haya ya utendaji hatutofika.

Lakini wizara yako vile vile, ningeomba sana muajiri watu wa kutosha hasa madaktari ambao hawapo, kuna madaktari *specialists* unakuta Zanzibar nzima Mnazi mmoja unaambiwa wako wawili. Wakati wale wawili wataweza kuhudumia vipi wananchi wote kwa siku hospitali ile utafikiri markiti pale, watu wingi sana haya ni kama mahospitali ya China, India, Nigeria na nchi nyenginezo ukienda hospitali utafikiri uko marikiti ya vitoweo.

Sasa Hospitali ya Mnazi Mmoja wananchi wengi, madaktari kidogo hivi daktari mmoja wawili *specialist* ataweza kuhudumia watu wangapi kwa siku au kwenda kuwauliza yeye mwenyewe anachoka. Hivyo, ni vyema sasa tuajirini *specialists* wawe wengi tizameni *strategy plan* zenu ziko vipi kwamba kila raia mia anatakia daktari mmoja mpate vile *standard* ambazo zinatakiwa kiafya.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana nikazungumza kwa hali tunayokwenda nayo kwa sasa hivi Wizara ya Afya hata tuweke mawaziri wote tukuwekeni wa mbele kwenye Wizara ya Afya hamtoweza kwenda, kwa wizara hii natutalaumiana kila siku tumuombe sana Mhe. Waziri lazima mushauriane kwenye kuzidisha watendaji wawe kamili kwenye ma-*specialist* na wengineo la si hivyo tutakulaumu wewe tunamlaumu Katibu sijui tutamlaumu waziri mwengine, tunamlaumu Makamu wa Rais tutamlaumu serikali kwenye suala hili tutakuwa hatufiki,

madaktari wawe wengi kwa mujibu wa *level* inayotakiwa fedha ziwepo machine ziwepo imeharibika moja nyengine ipo, si inaharibika moja nyengine ipo si inaharibika moja anaambiwa mtu ende *Global*, sasa *Global* ataenda kutibiwa na nani wakati serikali hailipi pale.

Kwa kweli, hii imekuwa kitenga uchumi saa nyengine, wakati wa nyuma huko wanaziharibu makusudi watu wakalipishwe kule hata hatufahamu. Tunaona hii ni hali halisi mtu anaambiwa kule akalipe laki mbili masikini atalipa vipi. Lakini Mhe. Mwenyekiti namuomba sana Mhe. Waziri kwamba ahakikishe kwamba kituo changu cha Chaani Masingini ambacho kipo tunakijenga ili tuweze kukamilisha Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa sababu wananchi waliokuwepo pale ni zaidi ya elfu saba, na kituo kile hakifanyi kazi kimekufa kabisa.

Sasa mimi Mwakilishi wa Jimbo la Chaani niko tayari kushirikiana na Mhe. Waziri nitajua mimi mwenyewe fedha nitazipata wapi kwa ajili ya kuanza kujenga *foundation* hospitali ile mpya ili na Mhe. Waziri aweze kutia nguvu zake kupita Wizara ya Afya au wafadhili ambao utaweza kuwaleta wewe kituo kile tuweze kukimaliza kama mwaka 2020, wananchi wetu waweze kupata huduma ile. Niko tayari kabisa kutoa ushirikiano uwo ili kukamilishe Ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini pia tuwasaidie wananchi wote kwa ujumla ikiwa CCM, ikiwa CUF, ikiwa CHADEMA na vyama vyengine wataumwa waweze kwenda kutibiwa pale kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, suala langu jengine nakata wizara yako ilichukulie hatua ya ziada muweze kuangamiza mbu, nzi na kunguru hivi sasa hivi hakuna sehemu ya Zanzibar utakayoenda kula hata iwe hoteli ya *five star* chumba milioni tatu kwa siku, basi ukenda kula *restaurant* manzi tele kwenye chakula, ukenda Forodhani hali kadhalika, hospitalini halkadhalika tunaomba sana mutafute fedha maalum za kuweza kuangamiza nzi ambazo wanasababisha kipindu pindu maradhi pamoja na kuangamize hawa mmbu kama mlivyoangamiza pamoja na kunguru, ili kuondosha mazingira machafu na maradhi ambayo yanasababishwa na wadudu hawa.

Lakini vile vile, Mhe. Waziri ningekushauri sana kwa sababu kila siku tunapiga kelele mtu tunawazungumzia watu wenye UKIMWI, hawachukuli hivi hawapewi hivi, wizara yako kesho ituletee daktari hapa Mhe. Waziri, Wawakilishi wote wapimwe UKIMWI wote na majibu yote Mhe. Spika, aje atangaze huu ndio mfano, aje atangaze Mhe. Spika, Mwakilishi gani kaathirika Mwakilishi gani hajaathirika aje hapa atangaze. Haya ndio tunataka tuone kwa sababu sisi tunawazungumzia watu kila siku, sijui wanaumwa na hivi, na hivi na hivi na sisi tuje tupimwe humu ndani. Japo kuwa mtu asisemwe ana UKIMWI lakini aseme huyu kidogo anaumwa. Mhe. Waziri tunakuomba sana uwalete madaktari hao ili waheshimiwa wapimwe na wao tuwajue, Mhe. Waziri naambiwa hapa nije nipimwe heke yangu kwa sababu wengine washaanza kuogopa. *(Kicheko/Makofi)*

Jengine Mhe. Mwenyekiti, naomba sana suala la *ambulance* yale ambayo mnayo makubwa ma-*four wheel drives* ya *land cruiser* kwa ushauri wangu zile kwa njia zetu ni nzuri, lakini *standard*

ya *ambulance* hazifai kwa sababu zinapinduka mara moja *stability* yake ni ndogo sana ziko juu sana tungeomba sana kama zile ni za msaada zichukueni, ziingizeni kwenye masuala ya utendaji ya wizara, lakini *ambulance* ninuweni ambayo *stardard* yake hayapinduki ovyo kama wanaotumika nji za wenzetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambao nashauri serikali kwa ujumla kwamba watu wote wawe na rekodi ya watoto yatima wazee wasiojiweza, pamoja na watu wenye ulemavu ndani ya Zanzibar, serikali iweze kukaa na makampuni ya *insurance* ambayo ya afya *health insurance company* wakae nazo kama wataamua kusaidiana au watalipa wao serikali waweze kuwalipia hawa watu kadi za afya, wawe nazo bure kwa sababu watu wenye ulemavu, watoto yatima, wazee wanaumwa kila siku fedha za kwenda kujitibu hawana. Kwa hivyo, tunaomba sana serikali ilifikirie hili, kupitia Ofisi ya Rais na Mwenyewe wa Baraza la Mapinduzi Ikulu, kwamba kama uwezekano upo basi hawa watu wakatiwe waweze kupewa *insurance* yao ya afya, ili wawe wanatibiwa bure.

Lakini vile vile, jengine ambalo nataka nilizungumze Mhe. Waziri tuna *pharmacy* nyingi ndani ya Zanzibar, kuna siku moja mimi nilishangaa sana niliwahi kununua dawa Mhe. Mwenyekiti, ikaandikwa *Made in India*, lakini ile dawa nikaitaka ikawa imeniishia nikenda nayo India kile kichupa kile, nikaenda kwenye *pharmacy* zinaitwa *Apollo Pharmacy India*, wakanambia hii dawa hatuitambui wala haipo. Sasa mimi swali langu najiuliza huku Zanzibar kuna dawa imeitwa *Made in India* ambayo naambiwa ndo inajulikana inatoka India na nimaarufu. Kufika kule India *pharmacy* karibu mbili tatu wananambia hii hatutowi wananambia hii hatutoi India haipo.

Sasa Mhe. Waziri hebu tunaomba sana mkafanye utaratibu hawa wenye *pharmacy* isije kuwa wengine wanabuni hizi dawa au wanafoji kupitia kuweka *trade mark* za watu za nchi kwa kuvutia labda akiona akiweka made in India, *made in USA*, *made UK* labda ataweza kuuza mara moja na kuweza kuumiza watu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo kama nilivyosema mwanzo maongezi yangu mimi ni madogo lakini kama nilivyohimiza kwamba usafi ni muhimu kwenye masuala ya maabara, sehemu za operesheni, sehemu za kutoa meno na sehemu nyengine zote, usafi ni muhimu watendaji wawepo na wao wa kweli kwa sababu kama walivyoeleza humu ndani atakaye simama mtatwakwa tu, kwa sababu watendaji wengine hawana imani inaonekana.

Sasa tunaomba sana muwe wakali mchukuwe hatua za kutosha ili haya mambo yaweze kwenda vizuri, tunaamini sana sio wewe, sio mimi, wala sio mwengine yoyote anataka mtu afariki mtu aumwe au mtu aumie, lakini inasababisha na watu wachache na kama labda kuna tatizo nyinyi wenyewe mnalijua basi fanyeni mulitafutie ufumbuzi wa haraka iwezekanavyo hili suala.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nafikiri nitangojea majibu yangu hasa kituo changu cha afya, ili Mhe. Waziri nije nimpitishie bajeti yake kwa asilimia yote mia sasa hivi nampa tisini na tano tu. Nazuiya kifungu kidogo cha kupata jibu ambalo vipi tutashirikiana naye kwenye kituo changu cha Chaani Masingini na mambo mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti baada ya hayo kama nilivyosema nai- *support* asilimia 95 na nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe,. Nadir Abdul-latif Yussuf. Sasa nimwite Mhe. Hidaya Ali Makame atafuatiwa na Mhe. Omar Seir Abeid na Mhe. Mohammed Said Mohammed ajiandae.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuchangia machache ya Hotuba hii, ya Mhe. Waziri Hotuba ya Wizara ya Afya. Mhe. Mwenyekiti, nikawa kama ni Mjumbe wa Kamati nimenyanyuka na kuiunga mkono hotuba hii, kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri wa Afya mpya ambaye ameteuliwa karibuni tu, na muda mchache tu ambao kaingia tayari tumeshaanza kuona yale matunda mazuri, na matokeo mazuri na matokeo mazuri juu ya wizara hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba kuna msemo unasema "Ukimuona mtu mzima analia mbele ya watu ujuwe kuna jambo". Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya ndio wizara ambayo jicho kubwa na binaadamu au uhalisia mzima wabinaadamu upo hapa Wizara ya Afya, kwa sababu bila ya afya huwezi kufanya kati chochote, bila ya afya huwezi kufanya lolote na hata sisi tuliokuwepo ndani ya Baraza lako hili tukufu kama tusingekuwa na afya imara, au tusingekuwa na uzima basi sidhani kama kuna mjumbe yoyote hapa angesimama na kuweza kuongea lolote au angesimama na kuweza kuchangia lolote. Kwa hivyo, tujuwe kwamba afya ndio kila kitu katika maisha ya binaadamu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mengi sana tumeyaodhesha kwenye ripoti yetu ya kamati, lakini tu ningependa kumwambia Mhe. Waziri kwa vile ni mpya ndani ya wizara hii, kaja karibuni tu basi ningemuomba sana akazipitia sana sana sana, ripoti zetu zote za Kamati ya Ustawi wa Jamii zinazohusiana na Wizara ya Afya, akaweza kuziona zile changamoto ambazo tumeziorodhesha mle, lakini pia akaweza kuyaona yale yote ambayo tuliyatolea maelekezo lakini tukayaomba kutendewa kazi, kutekelezwa juu ya wizara yake hii, ayaone na ayafanyie kazi. Kwa kweli, wizara hii ni kubwa wizara hii ni kila kitu, lakini nipende kumwambia Mhe. Waziri kwamba ndani ya ripoti hizo hakuna kitu ambacho atafuatilia akaweza kukikosa mle na akaweza kukosa muelekeo, kwani ndani ya kamati yetu hakuna tulichokiacha hata kimoja.

Mhe. Mwenyekiti, tumepita kila sehemu inayohusika na Wizara ya Afya, tumepita kituo baada ya kituo Unguja na Pemba, hatukupata uwezo wa kwenda nchi jengine kwenda kuangalia na kusoma, lakini hizo hizo zilizokuwemo humu ndani ya nchi yetu, hakuna sehemu ambayo hatukupita na tukaona changamoto na tukaweza kuziorodhesha kwenye wizara husika.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri watendaji wake ndio wasaidizi wake, wote akaye nao vizuri, akae nao makini ili waweze kusaidiana katika kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Mhe. Mwenyekiti, Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi imetoa tamko kwamba "elimu bure na afya" kwa hiyo wananchi wetu wanajivunia sana haya matamko na ndio maana wakawa wana-*complain* kubwa wanapokwenda mahospitali wakakosa huduma hichi kinawavunja moyo.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana yeye ni mzalendo, mzaliwa, ndio kila kitu ndani ya nchi hii, tunamuomba usimamie wizara hii kwa jicho lako la huruma na kwa moyo wako wote wa utendaji, basi tunamuomba nguvu zako zote zimalizie ndani ya wizara hii, ili wizara hii iweze kuwa na maendeleo mazuri lakini iweze kupunguza wimbi kubwa la changamoto zilizokuwemo ndani ya wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, nitaizungumzia kidogo Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hospitali ya Mnazi Mmoja ni Hospitali ya Rufaa ambayo ndani ya nchi hii tunaitegemea Wapemba, Waunguja na kwengine kokote.

Mhe. Mwenyekiti, tulipopitisha ule Mswada kuitaka Hospitali hii kuwa ni Hospitali ya Rufaa wengi kuli-*complain* tukaona kwamba hii hospitali bado haijakidhi vile viwango vya kuwa Hospitali ya Rufaa kwa sababu kila mtu anaitegemea ile hospitali na kila mgonjwa anaitegemea ile hospitali na kila mgonjwa anaingia kwa aina yake pale kwa ajili ya kupata matibabu.

Kwa hiyo, kuna vitu vingi ambavyo bado havijakuwa kama ni kitu ambacho kitasababisha ile Hospitali iwe Hospitali ya Rufaa, lakini kwa macho ya wakubwa na kwa macho ya wengi na kwa macho ya muekano ikaonekana kwamba ile Hospitali kweli ni hospitali ya Rufaa na kweli kwa sababu inafanyakazi na inatoa huduma.

Lakini huduma zinatoka pale Mhe. Mwenyekiti, bado changamoto kwa wananchi. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri akalisimamia hili neno Rufaa ndani ya Hospitali ile. Neno Rufaa ni neno kubwa sana ndani ya Hospitali ile tulipe hadhi lile neno Rufaa ili ile hospitali ionekane kweli ya Rufaa.

Mhe. Mwenyekiti, hospitali ile ndio tegemeo la ngonjwa wa aina yoyote ambaye atashindikana maradhi yake kutibiwa ndani ya Hospitali za Vijiji na dani ya Hospitali za Wilaya na atakapokwenda pale atakuwa ana uhakika wa kwamba huku ninakokwenda nitakwenda kupata matibabu na nitaweza kupona kama bado Mwenyezi Mungu hajanihitaji . Lakini inakuwa ni tafauti kwa baadhi ya wagonjwa na kwa baadhi ya wakati.

Pale hospitali Mhe. Mwenyekiti, ili kuimarika zaidi basi ile miundo mbinu yote inayosababisha ile hospitali iitwe Rufaa inahitajika kuweko, pale vifaa vya huduma ya kupima, ya kutibu na kufanya kile ile ambalo linahusika na vifaa viwepo na visiwe chakavu na visiwe hafifua kwa sababu ndani ya Hospitali ya Rufaa hakutakiwi kuwe na kipimo kimoja ambacho kinahudumia wagonjwa 40, 50, 100 kwa siku moja.

Lakini, ndani ya hospitali yetu ile tunaona changamoto nyingi sana zinaikabili kuhusiana na suala la vipimo, iweje mgonjwa katoka Makunduchi au Nungwi kapita hospitali ngapi huko mpaka kafika pale anafika pale anataka huduma za *CT-Scan*, anataka huduma za *X-Ray* anataka nyengine anaambiwa hapa hazipatikani nenda pahala fulani. Kwa nini yule dokta akajua kwamba huko anakomwambia aende zipo zile huduma wakati yeye ni msimamizi na muhusika mkubwa wa ile hospitali ambayo inatakiwa zile huduma ziwepo kwanini kule akajua kuwa zipo na pale ziwe hazipo.

Mhe. Mwenyekiti, nikwambie sana Mhe. Waziri hili suala linahitaji kufatiliwa na linahitaji usimamizi wa hali ya juu, bila ya kufanya hivyo huu usanii unaoambiwa kwamba upo utaendelea kuwepo. Na huu usanii wakati kila mtu tayari anauzungumza basi upo, upo kweli, sio kama ndani ya hospitali ile ikose vifaa hivi, hiyo si kweli. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri awe msimamizi wa suala hili.

Lakini pia ile hospitali ina Wajumbe wa Bodi ambao hao wameteuliwa *special* kwa ajili ya usimamizi na kusaidiana na ile hospitali. Namuomba Mhe. Waziri kwa hichi kipindi ambacho umebakia kuwa nacho akawajua na akawatambua hawa Wajumbe wa Bodi, akawa nao bega kwa bega na akafanya kazi nao kwa karibu, hawa wanaweza kukusaidia kwa asilimia mia 100. Wale nao wameteuliwa pale kuwa ni wasaidizi wa ile hospitali kuweza kurekebisha yale madogo madogo yasiyotakiwa kufanyika na wizara wao wayafanye. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri na hawa Wajumbe wa Bodi wanaoisimamia Hospitali ya Mnazi Mmoja na wao uwe nao karibu ili uweze kufanya nao kazi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda kwenye suala la usimamizi wa kazi. Wakati tulipokuwa tunafanya ziara zetu za kamati tuliona baadhi ya changamoto kwamba huu usimamizi ndio unaozuri hii wizara. Usimamizi ndio kila kitu, kwa kweli haiwezekani kama huku kuna kitengo fulani ambacho kinasaidia ile hospitali ikawa mawasiliano ni hafifu na pale hospitali husika.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyofahamu tuna Kitengo cha Damu Salama ambacho kitengo hichi kina mashirikiano makubwa na Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kitengo hichi kinahifadhi damu na pale hospitali wanakwenda wagonjwa ambao wanahitaji damu. Kwa mfano, unakwenda pale hospitali baadhi ya siku unakuta kwamba ndani ya ile hospitali eti hakuna damu ya kuweza kumsaidia mgonjwa na mgonjwa wenyewe *time* nyengine pengine ana *emergence case*. Haiwezekani, wakati huku kwenye kitengo unaambiwa damu zipo mpaka hazina kazi ya kufanyiwa, lakini wenye hospitali kule wanakwambia wao damu hakuna.

Mhe. Mwenyekiti, hivi vitu ambavyo vinafanyika haviingii akilini, usimamizi na utaratibu ndio kila kitu. Mimi ninachofahamu kwamba ndani ya nyumba anapokuwepo baba na mama na wanawe, baba ndiye anayekuwa msimamizi, lakini na mama ndiye mshughulikiaji mkuu wa

usimamizi wa baba. Mhe. Waziri una timu kubwa ambayo inaweza kukusaidia wewe kila kitu, una Mhe. Naibu Waziri una Makatibu Wakuu, una wasaidizi wa Makatibu Wakuu, lakini pia una Wajumbe ambao wanaisimamia Hospitali ya Mnazi Mmoja kama Hospitali mbali ya wizara, watumie hawa kwa kuzifanya hizi kazi.

Mhe. Mwenyekiti, malalamiko ni mengi. Mhe. Waziri nakuomba sana uyasikilizi haya malalamiko ya wananchi juu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, niaibu sana sana. Kwa kuzingatia hili tunamuona sana Mhe. Rais wa Zanzibar anavyofanya kazi juu ya kusimamia maendeleo ya wananchi wake juu ya kupata huduma bora ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja na ndio maana kila siku anaendelea kufungua vituo au maeneo kwa ajili kwamba wale wananchi wapate huduma zilizobora, lakini ufatiliaji na utendaji ndio unaokwamisha hizi huduma. Mhe. Waziri ningekuomba sana usimamie juu ya hili na uwe makini juu ya hili.

Mhe. Mwenyekiti, ndani ya hotuba yako hii kwenye vifungu kuna maeneo mengi yametenga vifungu, lakini pia ndani ya kitabu chako hichi, ukurasa wa mwisho huku wa 74 kuna matumizi ya Hospitali ya Mnazi Mmoja na kila kitu kimewekwa na fungu lake hapa. Kuna huduma za uchunguzi zimewekewa fungu lake, kuna huduma za matibabu zimewekewa fungu lake, lakini kuna huduma za uongozi na utawala. Kwa hiyo, haya mafungu yaliyotengwa ndiyo yanatakiwa kufanya kazi mle ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Lakini hapa katika mafungu yote haya uliyoyaorodhesha tunataka yasimamie na yafanye ile kazi ambayo yamewekewa hapa sio yawekwe hapa kwa kuoneshwa tu, yafanye kazi ile inayotakiwa haswa.

Mhe. Mwenyekiti, nina hakika lawama zitakwisha, ninahakika na haya malalamiko kwa wananchi wetu yatapungua kwa asilimia kubwa. Namuomba sana Mhe. Waziri sana Mhe. Waziri hichi kitabu amekielezea vizuri sana na mafungu yote humu ameyaonesha, lakini ufafanuzi ndiyo unaohitajika ili kila mtu afahamu kweli hichi kitabu kimeongea kweli lakini na utekelezaji. Mhe. Waziri atakapotekeleza haya yaliyokuwemo ndani ya kitabu hichi nina hakika kero za Wizara ya Afya zitapungua.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa sitaki kuongea mengi kwa vile ni Mjumbe wa hii Kamati. Kwa hivyo, niseme tu Mhe. Waziri labda atakapokuja hapa kuna fungu hapa limewekwa la ujenzi wa Hospitali ya Binguni, naomba aje atupe ufafanuzi Waheshimiwa Wajumbe lakini na hata wananchi waliokuwepo huko nje wajue ndani ya mwaka huu hii Hospitali ya Binguni kwa hili fungu lililopangwa hapa utekelezaji wake utakuwaje na je, utafikia kwenye hatua gani na vipi hospitali hii itaanza kujengwa baada tu ya kupitishwa bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo macheche niseme na mimi naiyunga mkono hotuba hii kwa asilimia 100. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, nakushukuru Mhe. Hidaya Ali Makame, kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Omar Seif Abeid atafuatiwa na Mhe. Mohammed Said Mohammed na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu ajiandae.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Afya. Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa Rehma na kumtakia Rehema na Amani Mtume wetu Muhammad

(*S.A.W*), ikiwa leo tuko katika Ramadhani ya 19 ya Mwezi huu, namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie sote afya njema, tumalize Ramadhani hii kwa salama na wale ambao ni wagonjwa Mwenyezi Mungu awape afya na walio katika hospitali pia na wao Mwenyezi Mungu awahuishe ili waweze kurudi nyumbani waweze kuungana na familia zao katika kusherehekea sikukuu ambayo iko karibu kutufikia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sina budi kuchukua fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa juhudi zake kubwa wanazozifanya kuliongoza taifa letu. Mimi kila siku nitakuwa sikutenda haki nikikosa kumshukuru kwa yale aliyoyafanya katika taifa hili. Tumuombee na yeye kwa Mwenyezi Mungu amuongezee afya, hekma, busara ili aweze kutuongoza na tufikie pale pahala tulipopakusudia kama Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi inavyoelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, naanza utangulizi huu kwa sababu gani. Nasema haya kwa sababu kabla ya Mapinduzi katika jimbo langu la Konde kulikuwa na kituo kimoja tu cha afya kinachoitwa Kituo cha Afya cha Konde, wananchi wote kutoka Makangale, Msuka, Mkiawang'ombe, Kiuyu Kipangani na kwengineko wote walikuwa wanakuja kukutanika pale Konde wanasubiri huduma katika kituo kile. Kwa kweli, kilikuwa ni kijituo kimoja kidogo hata mvua ikinyesha watu walikuwa wanajibanza upenuni kusubiri kuingia kumuona daktari.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya Mapinduzi yetu tukaanza ku-*improve* kidogo kidogo katika huduma za afya na leo hii ninavyosema Jimbo langu la Konge lina vituo vya Afya saba. Nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar tena kwa utendaji wake. Tukisema kweli Mhe. Rais ni Rais wa mfano. Pamoja na yeye mimi nachukua fursa hii tena kuupongeza uongozi wa wizara, lazima tukubali ya jana siyo ya leo. Mimi siwezi kusema kama kitabu hakina kitu, mimi nasema kitabu kipo vizuri, kimepangika kinachohitaji ni maboresho na hakuna mkamilifu mwanadamu, kila mwanadamu ana makosa yake, mimi Omar nina makosa yangu, mwengine ana makosa yake na kila mmoja ana makosa yake. Uzuri wa binaadamu ni kukosea na akakubali kukosolewa, ndipo tutakapofika kwenye pahala pazuri tukafikia lengo tulilolikusudia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hiki naomba kwanza kabla ya kwenda kwenye michango mengine nitakwenda kwenye ukusa baada ya ukurasa. Lakini nilitaka Mhe. Waziri atakapokuja anambie kuhusiana na makusanyo tuliyoyaweka kwamba tuliwapangia hawa katika kipindi kile kilichopita kutukusanyia pesa hasa Mnazi Mmoja, ukusanyaji wa mapato ukawa umeshuka umefikia asilimia 40.4 tuliwapa jukumu la kukusanya shilingi milioni 931 na shilingi 22,000 lakini wakaweza kutukusanyia shilingi 375,910,687 sijui kulikuwa na kikwazo gani.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu *NHIF* walipokuja hapa walitwambia katika maeneo ambayo wanalipa pesa nyingi moja ni Hospitali ya Mnazi Mmoja, lakini hatujui kuna nini. Naangalia naona labda kuna kitu kinataka kifanyiwe marekebisho ili kuweza kufikia lile lengo la makusanyo.

Mhe. Mwenyekiti, tukiingia upande mwengine ukurasa huo huo wa 5 nilikuwa naona mafanikio ya wizara ambayo yamepatikana na wakawataja watendaji ambao ndio wanaoiyongoza wizara hii, wanayoiendesha, tukawakuta kuna wafamasia 3, ukurasa wa 5 unasema

> "Mafaniko yaliyopatikana wakiwemo madaktari 46, wauguzi 170, Wafamasia 3 na fundi sanifu wa maabara 34."

Kwa kweli, nashauri sana kwamba nafasi za wafamasia ni muhimu na iko haja ya kuziongeza. Kwa upande wa Pemba tulikuwa tunalilia wafamasia, sasa nasikia tumepelekewa mfamasia sijui mmoja au wawili, kwa ujumla wake wafamasia 3 kutokana na uhalisia wenyewe ni kidogo. Kwa hivyo, naomba sana kwamba suala la wafamasia liongezwe, hawa ndio wapishi wa hiyo tiba ambayo tunaitegemea.

Mhe. Mwenyekiti, pia kama alivyosema mwenzangu Mhe. Suleiman Sarahan Said kwamba kuna takwimu ya watu wa UKIMWI, lakini hatuoni takwimu ya maradhi ya sukari, wagonjwa wa moyo na maradhi ambayo siyo ya kuambukiza ambayo kwa sasa yanaathiri kwa kiwango kikubwa maisha ya wananchi wetu. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana watu wa wizara wakati wanapotuandikia ripoti kama hii watupe takwimu, kwa sababu wanapotupa takwimu kama hivi ni jambo ambalo linatusaidia sisi kuweza kushauri na kuelekeza, kwani kila kitu au maendeleo ya jambo lolote linapatikana baada ya kujua uhalisia wa mahitaji yako, na kama hujui uhalisia wa mahitaji yako huwezi kupata mafanikio kama unavyoyategemea.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tukienda katika ukurasa namba 10 kumezungumzia hapa ugonjwa la homa ya ini, nalo ni ugonjwa hatari. Lakini pia naomba nifahamu kwa faida ya wananchi wetu, wizara jinsi gani imejipanga kupambana na hii homa ya ini. Hapa naona pameandikwa kwamba, naomba kunukuu:

> "Wizara inandelea kutekeleza mkakati wa kufanya ufatiliaji wa jamaa na jirani wa wagonjwa wa Kifua Kikuu ili kuweza kuibua wagonjwa wapya. Jumla ya watu hao 942 ambao ni jamaa wa wagonjwa walifuatiliwa".

Lakini hapo chini kwenye nambari 30 wakasema kwamba.

> "Hadi kufikia Machi 2018 jumla ya wagonjwa 196 kwa huwo ugonjwa wa homa ya ini waligundulika"

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kuzungumzia homa hii ni moja katika maradhi hatari na sijui wataalamu wamejipanga vipi kutoa elimu au kutoa tahadhari juu ya homa hii ya ini kama inavyofanywa kwenye tahadhari ya homa nyengine hasa kwa wananchi wetu vijijini ambao mambo haya wanahitaji kupata taaluma ya kila wakati. Kutokana na hali hiyo, naomba sana kutolewa elimu juu ya magonjwa haya kama ya homa za ini na mambo mengineyo ambayo ni homa hatari, ili jamii iweze kuelewa na itiliwe mkazo kwa wananchi wetu wote.

Mhe. Mwenyekiti, tukenda kwenye ukurasa wa 12 tunaambiwa kuna suali la mama wajawazito. Mhe. Waziri aipokuwa akisoma katika kitabu chake alisema katika mwaka 2016/17 wajawazito 61,981 sawa na asilimia 91 ya lengo walihudhuria katika *clinic* na hivyo wengi wa mama hao angalau walifika *clinic* na mama watoto angalau mara moja kabla ya kujifungua. Hata hivyo wengi wa mama hao hufika *clinic* wakiwa wanakaribia kujifungua.

Mhe. Mwenyekiti, nimetaka nijue idadi ya akinamama wajawazito ambao wamejifungulia majumbani. Katika takwimu tumeiyona idadi ya watoto waliozaliwa katika kiambatanisho nambari 4 ukurasa wa 64 na idadi ya hospitali walizojifungulia. Tujiulize je, nyinyi mmepata takwimu kwa watu waliojifunguliwa hospitalini. Kuna utaratibu gani wa kupata takwimu kwa wale watu wanaojifungulia majumbani. Ni vyema na ni busara zaidi mkaanza au mkawa na mpango madhubuti wa kuwatambua wale akina mama wote ambao wanajifungulia majumbani.

Mhe. Mwenyekiti, hawa tutawatambua vipi. Tutawatambua kwa watu wetu waliokuwepo katika vituo vya afya kurudi chini, kurudi katika ngazi za shehia na ngazi za nyumba kumi, wakashirikiana na wale wakunga wa asili kuweza kupata takwimu halisi ya mama wajawazito wanaojifungulia majumbani. Katika takwimu hii pia tuliyoiyona hawakutuonesha kwamba ni watoto wangapi ambao wamefariki.

Kwa mfano, ukichukulia hesabu ya mama wajawazito waliolazwa utasema Hospitali ya Chake Chake waliolazwa walikuwa ni 3314, waliojifungua kwa njia ya kawaida 2984, waliofanyiwa upasuajiri ni 244, lakini ukitoa hesabu hiyo utakuta kuna upungufu wa 16. Je, sasa hawa tujiulize wamekwenda wapi, wamekufa. Sasa kama wamekufa kwa nini msituorodheshee. Kwa hivyo, ni vizuri ni vizuri mkaorodhesha, ili tukapata kujua ni idadi gani halisi ya watoto waliokufa baada ya kujifungua na watoto wangapi waliokufa kabla ya kujifungua kama mlivyoeleza hapa wazazi waliofariki hapa mmeeleza wazazi waliofariki, lakini hamkueleza ni watoto wangapi ambao wamekufa baada ya kujifungua au kabla ya wale mama zao waliojifungua.

Lakini, ukiangalia na takwimu hii utakuta kuna mapungufu hata ukijumlisha hiyo 3,314 ukiijumlisha 244 inakuja 3,228 tofauti mimi naiona tofauti hapa ipo kwa sababu inawezekana kwamba wako wanawake au mama wajawazito waliokwenda kuripoti hospitalini lakini mkawapa namba nyengine kukawa na *confusion* ya takwimu. Kwa mfano, mtu akitoka Konde anakwenda Wete akianzia kituo cha afya cha Konde anapewa namba ile anasajiliwa upya na akenda Wete anasajiliwa tena.

Hivyo, utaratibu huu naomba tuubadilishe na tuwe na usajili mmoja tu mama mjamzito mnapomlaza kama katoka Konde atoke na namba yake kule kule Konde akenda kule iwe ya Wete pale au ya Chake Chake iwe ni muendelezo tu, ili kuweza kupata namba halisi ya mama wajawazito ambao wameripoti, jambo hili litatusaidia kupanga mipango yetu mizuri tutaaweza kujua watoto wangapi wamezaliwa, wangapi wamefariki, wangapi wanamatatizo, wengine wamezaliwa bila ya matatizo na mambo kama haya.

Lakini tukienda kwa ujumla…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nakukumbusha bado dakika tatu.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Tulizungumzia tatizo la uzazi wa mpango, lakini tumeona kwamba watoto waliozaliwa hapa kwa msimu mzima kwa muda wa miezi 9 tukenda kwenye jaduweli hili tunawaona kama watoto waliozaliwa ni 27, 275, je hapa tujiulize akinamama hawajafanya Uzazi wa Mpango, kwa sababu takwimu hapa inaonesha ni akinamama 27 tu au chini ya 27,275 waliojifungua wangine wamezaa wawili wengine watatu inamaana hata iyo 27 wanawake hawafiki ina maana hapa wanafuata mpango tatizo lililopo hapa ni takwimu.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri, pamoja na mambo mengine ni kusimamia takwimu katika wizara hii, na sio wizara hii tu inaonekana takwimu ni tatizo kwa ajili maendeleo ya popote takwimu ni kitu muhimu namuomba sana kwamba tuwasihi watendaji wetu wafanye kazi zao kwa uwadilifu na wawe wanaweza kujituma kwa kuweka angalau hizi kumbukumbu. Kwa kweli, wenzangu wamesema mengi mimi nasema kitabu ni kizuri siwezi kusema kitabu kibaya, kitabu ni kizuri kwa sababu kina muelekeo kina mambo mengine mazuri unaona lakini nawaomba wayasimamie haya.

Mhe. Mwenyekiti, hii ina maana Idara ya Utumishi watu wake hawawajibiki vizuri Mkurugenzi kama yupo ananisikia Idara ya Utumishi hawaweki kumbukumbu zao vizuri. Kwa hivyo, tunaomba wanaohusika watekeleze wajibu wao, ili kuweza kufikia malengo, kwani hatuwezi kufikia malengo kama hatuna kumbukumbu ya mambo yetu, leo tukiichambua kumbukumbu hii ya kitabu hiki utakuta kuna mambo kidogo.

Hivyo, baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti sitaki niseme sana, isipokuwa nasema naunga mkono hutuba hii na Mwenyezi Mungu awajaalie awape nguvu wakaitekeleze ili Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na yeye afurahi kuona kwamba yale aliyoyanzisha yanaendelezwa. Baada ya haya Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Konde nasema naunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti, Ahante nakushukuru Mhe. Omar Seif Abeid kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Mohammed Said Mohammed, atafutiwa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa ajiandae.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, lakini nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambao anaifanya kwenye wizara hii, hakika muangaza unaonekana (*Makofi*).

Vile vile, nimshukuru sana na nimpongeze Mhe. Mahmoud Thabit Kombo aliyewaachia kijiti hichi alijitahidi kufanya kazi kwa bidii sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nisome Ilani ya Chama cha Wananchi CUF na baadae nataka nisome Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika utekelezaji wa afya. Mhe. Mwenyekiti, naomba uniridhie sana nianze kuzungumza kwenye Ilani ya Chama cha Wananchi CUF naomba kunukuu.

Ilani ya Chama cha Wananchi CUF inasema hivi:

> "Afya ya mama na mzazi CUF inashukuru jitihida zilichukuliwa na wafadhili mbali mbali ikiwemo mradi wa Banki ya Maendeleo ya Afrika *ADB* kwa kusaidia huduma za tiba na kinga kwa akina mama waja wazito kuelekea kunako uzazi salama. Hata hivyo, sekta ya ndani ya nchi bado haijaona umuhimu wa uwekezaji wa kutosha katika masuala haya na mzigo huu umekuwa mkubwa kwa hospitali na *clinic* nyingi kuweza kuzimudu msongomano wa kina wa mama wazazi katika wodi ya wazazi ya hospitalini ni hali ya kutisha.

> Sasa Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoongozwa na CUF ndio ilani inasema, inaendelea kutoa huduma za uhakika kwa tiba na kinga za wazazi ikiwemo uwekezaji katika miundombinu na vitendea kazi kwa huduma, ajira bora kwa Wauguzi na Wakunga, dawa na zana mbali mbali za afya kwa mama mzazi, itazidisha juhudi za mashirikiano na wafadhili wa Mashirika ya Maendeleo kuendelea kuisaidia Zanzibar katika kufanikisha azma ya muda mrefu ya uzazi salama".

Mhe. Mwenyekiti, nataka sasa niisome Ilani ya Chama cha Mapinduzi, naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Ilani ya Chama cha Mapinduzi inasema hivi:

> "Utekelezaji wa Sera ya Afya, Sera ya Afya ya mwaka 1999 imefanyiwa mapitio na sera mpya ya mwaka 2011 imeandaliwa na kuanza kutumika. Aidha, Sheria ya Afya ya Jamii na Sheria ya Mkemia Mkuu wa Serikali imepitishwa chini ya sheria hii, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeamrishwa na kupewa nguvu za kisheria".

Mhe. Mwenyekiti, nataka kwenda sasa kwa mama watoto, huduma za mama watoto na uzazi salama, jumla ya vituo 84 vimetoa huduma za ziada zikiwemo kuzalisha maabara na huduma za meno, huduma ya afya ya uzazi kwa njia ya kawaida au upasuaji na afya ya mama mtoto hutolewa bila ya malipo katika hospitali zote na vituo vya afya.

Vituo vyote hivyo vinafaidika na upatikanaji wa dawa chini ya mpango maalum Zanzibar *Intergret Logiest System* na juhudi za kuwapatia watoto chanjo zinaendelea kutengeneza ili kupunguza idadi ya vifo vya watoto ambavyo asilimia 99.75 ya watoto wote wenye umri chini ya miaka 15 wamepatiwa chanjo hizo, chanjo za *BCG* imefikia asilimia 148, polio asilimia 95, dondo koo, kifa duro, pepopunda na uti wa mgongo asilimia 101 na shurua asilimia 77.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kujenga hoja ndio maana nikasoma ilani za vyama vyote viwili hivi, Ilani ya Chama cha Mapinduzi imeweka sawa na wale ambao walihisi ilani hii haipo au haiweki sawa, ilani hii ni nzuri sana, Mhe. Hamad Rashid endelea kuitekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Wizara ya Afya kwenye kitabu chao, nataka nichukue fursa hii kuwapongeza sana, kwa kuwa wametekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi karibu asilimia 80 hongereni sana na ndio Chama pekee kitachoweza kutufikisha pale tunapokwenda. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutaja mafanikio hayo mbali mbali mimi sasa nataka kuenda kwenye ukurasa wa 5 wa kitabu hichi na naomba tu kidogo mafanikio wizara kwa mwaka wa fedha 2017 -2018, moja katika haya anasema kupanuka kwa huduma za matibabu ikiwemo huduma za usafisha wa figo na matibabu ya saratani niwapongeze sana kwa kazi kubwa ambayo wanafanya na hakuna wasi wasi kwenye kile kitengo cha figo na kila mtu anaona sasa tunavyoweza kufanya *dialysis* ikiwa na utaalamu mkubwa sana, ombi langu kwa wizara kuweka wafanyakazi wengi wenye wataaluma ili basi kufikia lengo lile ambayo serikali inazitaka.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 15 wa kitabu hiki, huduma za kupambana na maradhi yasioambukiza *ANCD*. Mhe. Mwenyekiti, nimekuwa mdau mkubwa sana wa *ANCD* ni

maradhi yasiyokuwa ya kuambukiza ikiwa hapa Barazani au nje ya Baraza, niwapongeze sana wenye Kitengo cha *ANCD* kwa kufanya kazi lakini elimu ya Afya inahitajika sana ikiwa mitaani, ikiwa makazini, ikiwa kila pahala ningewaomba sana waweze kutoa elimu ya afya, ili basi wananchi ingawa wana mwamko mwingi wa kufanya mazoezi lakini pia na mwamko wa vyakula tuweze kutumia vyakula vile salama.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 17, kupamba na kichocho na minyoo na matende niendelee kuwapongeza sana kwa kazi kubwa ambayo wanaweza kuifanya lakini bado tunahitaji kufanya utafiti wa kudumu, ili kuona yale maeneo kama Makunduchi na kwengine wale mbu wa matende wameondoka kabisa lakini sehemu za Mahonda kuna kichocho kingi tuweze kuondoa kichocho kiwe angalau kinaweza kitufikisha katika hali nzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende tena katika huduma za msingi za afya ya akili niendelee kuipongeze sana serikali lakini hapa nataka Mhe. Waziri anisikilize vizuri changamoto katika sisi ni mgonjwa mtarajiwa wa afya ya akili kila mmoja wetu na wale tunawaweka kule ni binaadamu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri sana kwa heshima kubwa na taadhima atembelee akawaone wale watu wanakaa pahala salama, kwa sababu tusiwaweke kule kama wafungwa wale sio wafungwa wale ni wagonjwa tu, hivyo namuomba Mhe. Waziri atembee, akaione ile hospitali je sehemu wanayowekwa ni sehemu salama tuwaonee huruma sana.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na ukurasa wa 24, huduma za msingi za afya lakini tayari nimeingia uko, lakini Mhe. Mwenyekiti, ukurasa 31, Kitengo cha Huduma za Damu Salama niseme tu nao niwapongeze sana kwa kazi kubwa, lakini nichukue fursa hii kulipongeza Baraza laki Tukufu kwa kuchangia damu nzuri na nyingi na tukapita kiwango kumbe tukitaka tunaweza na ndio mfano mzuri wa viongozi hawa kwa jamii yote. *(Makofi)*

Vile vile, tuipongeze sana taasisi ya G1nayo imejitolea sana chini Mwenyekiti wake Abdalla Maulid Diwani imefanya kazi kubwa, lakini vile vile safari ya CCM ya 2020 nayo imefanya kazi kubwa, lakini na Mkoa wa Mjini imefanya kazi kubwa katika kuchangia damu salama kwa wananchi wote. *(Makofi)*

Lakini niende kwenye ukurasa wa 34, mradi wa kupandisha hadhi vijiji na Wakuu wa Wilaya na Mikoa, Mhe. Mwenyekiti naunga mkono sana hii. Lakini kuna tatizo moja anasema hapa wapo wafanyakazi wa kukidhi haja katika wilaya sitaki kuaminiana na kitabu cha Mhe. Waziri sitakuwa muumini kwa suala hili suala hili sio la msingi kwamba ninayo Mhe. Mwenyekiti ripoti hapa ya Kamati Teule ya kuchunguza Udhaifu wa Upatikanaji wa Huduma za Afya katika Hospitali Kuu za Unguja na Pemba na mimi nilikuwa Mjumbe, na nimepita mote lakini bado tatizo la wafanyakazi liko kubwa.

Kwa kweli, tunao uwezo wa kuweza kuzipandisha hadhi hospitali zile lakini bado tuweze kuweka wafanyakazi wenye taaluma kwa sababu unakumta *orderly* yeye anaweza kufunga kidonda anapiga sindano anafanya kila kazi. Kwa hivyo, bado tunaupungufu na hili ni tatizo la *central government* yenyewe, lazima tuweke mtazamo wetu katika wafanyakazi wa huduma ya afya, hatuwezi kuweza kuilaumu wizara kwa nini wizara haiajiri, lakini serikali kuu kwa nini haijiri na watu wenye wataaluma wapo wakafanye kazi kule kwa wagonjwa lakini imani inategemea. Mhe. Waziri namuomba kitu kimoja baada ya kuajiri hawa wapewe mafunzo

maalum kwanza ya *hospitality*, ili basi wawe wakarimu wasiweze kutoa zile lugha chafu kwa wagonjwa, kwa sababu ukimpa lugha nzuri mgonjwa moja wapo basi ninaamini wanasoma *psychology* ya kutosha lakini bado tunahitaji kukumbushana binaadamu tukumbushane kwa sababu tunasahau.

Ukurasa wa 38, Mhe. Mwenyekiti, najaribu niende mbio kwa sababu hata hichi kitabu kikubwa sijakigusa, anasema *program* ndogo ya uongozo na utawala. Sasa hapa nataka niseme tu Mhe. Mwenyekiti, nina nia na makatibu mnisikilize vizuri, nina nia ya kuchukuwa mshahara wa Mhe. Waziri, kama hatojibu mambo yangu.

Kwa kweli, nafahamu kulikuwa kuna nyumba nyingi za wizara na sehemu ambazo zilikuwemo zilikuwa nyumba za Vuga, Kilimani, Kikwajuni, Kwamchina, Michenzani na kwengine, sasa nyumba hizi nataka kuzijua kwa sababu kuna watu wamerithishana, madakatari wetu wanakaa pahali sipo na nyumba za Gamba kulikuwa na madaktari wanakaa nataka kuzijua ziko wapi hapa nitachukua mshahara wa Mhe. Waziri na ukamatia kwanza mpaka atakaponijibu vitu hivi viko wapi na aniambie wale waliorithishana na akina nani.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 43, Hospitali ya Mnazi ya Mmoja, Mheshimiwa nichukue fursa hii kuipongeza sana Hospitali ya Mnazi Mmoja sana kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya lakini napo kwenye faida kuna na mapungufu yake.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye hospitali ile imezidiwa sana na watu *population* ni kubwa tofati ya miaka iliyopita, nilipoona kwenye kitabu hichi cha Mhe. Waziri kuwa anaelekea Binguni kujenga Hopitali kubwa nataka nichukue fursa hii bila ya kimeme kumpongeza sana kwa sababu *population* imekuwa kubwa sana lazima tuhamie huko kwengine lakini mashaka yangu yananipa Binguni lakini mashaka ninayo ya Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Hospitali ya Mnazi Mmoja tumejenga *maternity* nzuri inavutia ina vifaa vingi lakini bado iko katika hali mbaya, siku moja Mhe. Waziri nimempigia nimekwenda na nimempigia simu atakuwa shahidi, kuna hali mbaya wagonjwa wanalala mpaka chini. Lakini sio hilo tu juzi hapa tuliunda Kamati Teule Mhe. Mwenyekiti ya kuchukunguza majengo ya serikali na ninasema tu katika majengo ya afya na lile jengo la Dodoma la *maternity* linahitaji kuchunguzwa bado linavuja lina ubovu wa aina nyingi. Vile vile, hata lile jengo la *neurosurgery* bado lina matatizo mengi makubwa maji yanaingia ndani tunampa mkandasi mmoja huyo huyo kuna harufu kuna harufu ya rushwa katika bodi ile ya ukandasi. Mheshimiwa umekwenda hapa lazima upatizama kwa jicho kubwa sana pana harufu ya rushwa inaweza kutokea hapa.

Mhe. Mwenyekiti, nielekee kwenye ukurasa wa 56, wa kitabu hichi, nitajaribu kuenda mbio sana Mhe. Mwenyekiti nivumilie sana, kwa sababu nina mambo mengi hata sijaweza kuyachukua mengine ukurasa wa 16, kitabu cha Mhe. Waziri kinaonesha pesa zilizotengwa kwa vifaa tiba mimi nataka kusema ni vidogo pesa za vifaa tiba ni kidogo zilizotengwa hapa lakini vile vile tujitahidi labda kuweza kumuongezea na mimi nina nia ya kulichukua fungu moja la maendeleo nikalielekeza kwenye vifaa tiba.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu cha Mhe. Waziri, katika kiambatanisho cha 4, kina *column* ya 2, haionesha inasema nini, waliojifungua kawaida kwa njia ya upasuaji na *column* ya

mwisho inaonesha waliofariki kwa kweli hazihamiki, takwimu hizi hazifahamiki. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atueleze alikusudia nini kwenye takwimu hizi hazifahamiki hata kidogo, na ndio maana nadhani wenzangu wakasema kitabu hichi hakina maana, lakini kitabu hichi kina maana isipokuwa kuna sehemu kimekosewa sana. Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri aje atutafsirie *column* zake hizi hata hesabu hizi hazioani, tungekuomba sana ufanye kitu kama hicho ili tuone jumla ya wajawazito waliolala wangapi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ningeomba sana Mhe. Waziri achukue kitabu kikubwa au watu wake wachukue kitabu kikubwa naanza sasa kutoa vitu. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa kwenye ukurasa nataka kuangalia kuwa iende kwanza nitowe changamoto zilizopo katika Hospitali ya Abdalla Mzee, kuna changamoto za mashine, kuna changamoto ya umeme mdogo unapelekea kuharibikia vifaa na kile kufaa za *X-Ray* kilichoharibika pale je Mhe. Waziri atakapokuja hapa anambie kimeshatengenezwa tayari cha *X-Ray* na kuna changamoto nyingi na pesa za *OC* kupelekwa kwa wakati hazipelekwi pia nalo hilo ni changamoto nyingi sana lakini hospitali ile ni nzuri sana, ukosefu wa makaazi wa madaktari pia ina matatizo, tunaomba tu basi tuweze kuwekewa sawa tuweze kujua kitu hiki kimenda zake.

Mhe. Mwenyekiti, Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Afya Huduma za Utayarishaji wa Mipango na Bajeti kiashiria cha matumizi ya serikali aya ya makadirio kimewekwa asilimia kumi na tano makadirio. Kwenye ukurusa wa HO 12 naomba tuende hapo naomba tuende HO 12 mheshimiwa kama umefika nataka kuuliza kitu kidogo sana hapo kwenye ukurasa huo, anasema umeweka mwaka 2016 ni asilimia 1.5 je kwa mwaka wa wajawazito wanagunduliwa na upungufu wa damu 2016 uemeweka ni asilimia 1.5 je kwa mwaka 2017 ni asilimia ngapi hakuna mama wajawazito walioripotiwa kuwa wana upungufu wa damu kwa mwaka huo, na wala hakuna *target* yoyote ambayo imeelezwa hapo.

Sasa niende kwenye ukurasa ya PHO 101 kiashirie chenyewe kinasema Lishe ya Watoto kwenye kiashiria cha lishe anasema asilimia ya watoto chini ya umri wa miezi sita walionyonya maziwa ya mama pekee nataka kujua hapo je wamepata takwimu za kupimia kiashiria hiki kwa vipi, kiashiria hiki kimepimwa vipi wamewauliza, wametoa *questionnaire* na je kuna ukweli wowote hapa na wanawajibu ukweli mimi sifahamu namuomba Mhe. Waziri unisaidie sana. Lakini tuende kwenye kitabu hiki cha HO 12 hapa kina kiashiria chengine asilimia ya matumizi ya fedha za serikali kwa Wizara ya Afya makadirio waliyoweka ni asilimia 15 kwa mwaka 2018/2019 ukurasa ya HO hayaendi sambamba na cha SMZ 24, ukiangalia SMZ 24 huko unaweza kupata ukizipiga hesabu unapata asilimia nane tu.

Sasa nilikuwa nataka kujua anapokuja Mhe. Waziri ukurasa huu wa SMZ 24 kunaashiria ukipiga hesabu unaona asilimia nane lakini kwenye ukurasa huu ambao wewe umeuweka ukurasa wa fungu HO 12 hili umepata asilimia kumi na tano ningeomba kiashiria hiki Mhe. Waziri uniwekee, lakini vyengine nilikuwa nataka nitowe ufafanuzi na niseme Mhe. Mwenyekiti fungu la Mnazi Mmoja Hospital nina nia ya kulizuwia lisiende popote nilichukuwe mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa na HO 127 hapa naomba ufafanuzi wa kifungu cha PH0101 Kinga ya Elimu ya Afya na kifungu kidogo cha Huduma za Kuimarisha Kinga za Jamii mwaka 2017/2018 zilitengewe bilioni 2,212,828,000 lakini mwaka huu kimetengewa milioni

286,190,000 mwaka huu kimepangiwa milioni 68,176,000 nilikuwa nataka kujua tu mbona zimeshuka sana hatumairishi hii kinga tena ya jamii au iko vipi.

Vile vile, akini niende tena kwenye kifungu kidogo kwenye ukurasa huo huo HH010110 Huduma ya Kuimarisha Afya ya Mazingira ya Jamii mwaka jana zilitengwa bilioni 7,720,357,000 mara hii imetengwa bilioni 2,650,000,000 nilikuwa nataka kujua lakini vile vile nilikuwa nataka kujua Huduma za Kuimarisha Afya Wilayani pesa zimepungua lakini mara hii mara ile tulipangiwa milioni 300,000,000 mara hii tumepangiwa biloni 1,713,034,000. Lakini Huduma za Ufuatiliaji Maradhi ya Kuambukiza hii mwaka jana tulipangiwa bilioni 9,250,347,000 mara hii imepangwa bilioni 5,000,000,000 sasa nataka kujua kwanini pesa zipunguwe kiasi hiki jee hatufuatilii tena maradhi ya kuambukiza au imekuaje.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho ni Huduma ya Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto mara hii tumepangiwa milioni 279,990,000 lakini safari hii kimezidi zaidi kimepangiwa bilioni 2,916,000,000 nilikuwa nataka ufafanuzi na ili niseze kuvichukua vifungu hivi lakini kifungu chengine kwenye PHO 102 Huduma za Tiba na Huduma za Matibabu safari hii kina pesa nyingi sana kina milioni 33,806,000 wakati ule kilikuwa na milioni 15,360,000 kwanini pesa zimezidi wingi zaidi, pesa hivi unazipeleka wapi tulikuwa tunataka kujua, vile vile kuna kifungu kidogo chza HH 01020106 Huduma za Uchunguzi wa Dawa na Vipodozi mwaka haikupangiwa kitu lakini mwaka huu imepangiwa milioni 566,700,000 nilikuwa nataka kujua tu kwanini zimepangiwa na wakati ule kulikuwa hakuna.

Lakini Huduma za Uchunguzi wa *Sample* za *FBA* imepangiwa milioni 120,000,000 mwaka jana lakini mwaka huu imepangiwa bilioni 1,135,000,000 mheshimiwa na hiki nakaribia kukichukua kifungu hiki kama nimebakia dakika kidogo nambie...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, dakika zako za kawaida zimekwisha lakini nimekuongeza dakika tano kwa hiyo hizo tano bado una dakika mbili.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa imani yako sizimalizi hizo...

Mhe. Mwenyekiti: Ndio umebakiwa na dakika mbili Mhe. Mjumbe.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nataka kuja kwenye mapato katika Hospitali ya Mnazi Mmoja mapato 2017/2018 yalikuwa ni milioni 931,022,000 lakini safari hii yamechuka kiasi kikubwa tumepata milioni 7,012,417 nilikuwa nataka kujua kwa nini tumechuka hivyo, lakini vile vile nakuja tena kwenye kifungu cha H2 Mnazimmoja Hospitali ukurasa na H 210.

Mhe. Mwenyekiti, Huduma za Uchunguzi na Utibabu mwaka jana tulikipangiwa milioni 295,754,000 lakini safari hii tumepangiwa milioni 704,063,000 kwa nini tumepangiwa pesa hizo na zimezidi kiasi kikubwa sana, lakini vile vile Huduma za Uchunguzi na Kutowa Huduma za Uchunguzi kwa wagonjwa wote mwaka jana tulipangiwa milioni 5,000,000 safari hii tumepangiwa milioni 273,000,000 nilikuwa nataka kujua lakini kubwa nilikuwa nataka kujua

Uendeshaji na Uratibu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ambazo hapa pana bilioni 10,084,000,000 mwaka jana hiyo na mwaka huu kuna bilioni 14,097,000,000 nilikuwa nataka tujuwe tu ni nini.

Mhe. Mwenyekiti, vifungu hivyo ndivyo ambavyo nina nia ya kuweza kuvichukua na nikushukuru sana kwa kuniongeza dakika mbili na ninasema naunga mkono hoja hii kwa asilimia tisini, na asilimia kumi mpaka nipate majibu au nichukuwe mafungu hayo nilosema.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Mohamed Said Mohamed kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Hussein Ibrahim Makungu atafuatiwa na Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kufika hapa katika mchana huu wa Baraza lako Tukufu hili kuchangia bajati hii muhimu sana ya Wizara ya Afya.

Lakini kwanza nimpongeza sana Mhe. Waziri kwa kazi yake nzuri japo kaanza muda mfupi kazi lakini tumeona matumaini yake na lengo lake na nia ya nzuri kwa Wizara hii ya Afya, lakini niwapongeze sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati wote mwenyekiti na wajumbe wake kwa ripoti yao nzuri na kazi zao nzuri nashukuru sana nawapongeza Vile vile, niwashukuru sana watendaji wa Wizara ya Afya kwa kazi yao kubwa kama unavyojua wizara hii ni kuokoa maisha ya wananchi au sisi kutuokoa kwa hivyo niwapongeze kwa juhudi zao kubwa kwa sababu kazi yao wanataka ufanye kwa umakini mkubwa uliokuwa nao na nashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianzie katika ukurasa wa kwanza huu katika bajeti ya Mhe. Waziri wetu wa Afya katika ukurasa huu wa nne lakini katika bajeti yake hii katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 Wizara ya Afya katika fungu H01 iliidhinishwa jumla ya shilingi bilioni 72,000,000,000 Mhe. Mwenyekiti nisema fedha hizi zile serikali iliyoidhinisha kwa bajeti hii ni fedha nyingi sana haijawahi kutokea Mhe. Mwenyekiti, lakini serikali yetu na juhudu zake kubwa pamoja na waziri wetu na viongozi wetu wameona umuhimu mkubwa wa wizara hii.

Kwa kweli, niko kwenye Baraza hili huu mwaka wa saba au wanane lakini bajeti hii haijawahi kutokezea Mhe. Mwenyekiti kwa umuhimu wa Wizara ya Afya wa kuja kutushughulikia wananchi wetu wapate kupata huduma iliyokuwa nzuri na afya bora, ili maisha yapate kwenda mbele wapate kufumbua maisha mazuri kwa watoto wetu, wazee wetu na vijana kwa ujumla. Mhe. Mwenyekiti, nipongeze sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kazi waliyoiona hii muhimu kwa nia yake njema na Mwenyezi Mungu atusaidie atuwezeshe bajeti hii iende vizuri kwa mwaka huu tuone mafanikio mwakani tukija hapa, lakini mimi naamini kwa wananchi wetu mara hii watafaida kwa Wizara hii ya Afya.

Lakini Mhe. Mwenyekiti hizi fedha ni nyingi sana kama nilivyosema bilioni karibu 72,000,000,000 haijawahi kutokezea kwenye bajeti yoyote ya Baraza la Wawakilishi na bajeti hii ni ya mwanzo ni kubwa kwa umuhimu wake. Lakini Mhe. Mwenyekiti nisema hizi fedha ni nyingi na watendaji hizi fedha wanakwenda kuzitumia kwa mambo mbali kuna mambo mazuri watazitumia na mengine ya ubadhirifu au yatakuwa ya udanganyifu sio lengo lililokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, niko kwenye Kamati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kamati ya *Public Account Committee PAC* kuhusu hesabu za serikali. Kwa kweli, baadhi ya fedha zinatumika vibaya, yaani mpaka unasikitika unasema hizi fedha. Kwa hivyo, naomba sana tutapofanya *auditing* ya serikali basi fedha hizi ziangaliwe vizuri hata hao watakaotumia watumie kwa malengo yalikusudiwa, hata hii Kamati yetu ya *PAC* ya Zanzibar watakaochaguliwa basi wawe wakali sana katika suala la hili la kutumia fedha hizi za Wizara ya Afya. Kwa hiyo, naomba nimepata uzoefu mkubwa huko Tanzania Bara kwenye kamati hii muda mfupi nimefanya kazi lakini nimeona changamoto zake na wajumbe walivyokuwa wakali wa Kamati ya *PAC* na mimi mmoja mjumbe wa Kamati ya *APC Public Account Committee*, jambo muhimu sana katika kamati hii kuchunguza hizi fedha za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kwamba sura ya Zanzibar au Wizara ya Afya ni Hospitali ya Mnazi Mmoja ikifanya uzuri Hospitali ya Mnazi Mmoja zinazofaa Zanzibar nzima basi yeye kafanya vizuri hilo halina shaka. Sasa namuomba Mhe. Waziri afanye ziara ya kushtukiza au ghalfa usiku, mchana, asubuhi akiamua yeye akatembelee hospital na hata mimi akitaka nitamsaidia Mhe. Waziri nitakuwa mpambe wake kumsaidia kwenda kutembelea kwa sababu hili jambo la kujitolea na kusaida, wakati mwengine ukienda Hospitali ya Mnazi Mmoja watendaji wetu wako *slow* utakuta mtu kwanza kaletwa mgonjwa, lakini daktari au wahusika wanafanya shughuli zao nyengine au wanakula kwanza mgonjwa anaumwa anaweza kufa na wala hakuna mshughulikiaji. Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri afanye haraka haraka apite kwa kushtukiza tu wala taarifa wasiwe nazo hao wenzetu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, ambayo ni hospitali ya rufaa hii.

Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Waziri na hata mimi nitamsaidia akitaka nitakuwa tayari wakati wowote isipokuwa yeye aniambie nitakuwa mpambe wake nitampeleka tutakwenda kuangalia hizi changamoto tupate kuona kuna nini. Kwa kweli, wakati mwengine watendaji wetu hawafanyi kazi na fedha nyingi tushatoa za serikali za mambo ya *OC*, mambo ya utendaji za kawaida pesa zishatolewa na serikali. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana bajeti hii iende tukija mwakani hapa tuwe na mfano na wananchi wakubali kwamba Chama cha Mapinduzi kwa kupitia Ilani yetu hii tunafanya kazi kwa nia nzuri na Mhe. Rais wa Zanzibar kachagua watendaji ambao wanafanya kazi vizuri kwa nia safi bila ya kujali muda wao wala maslahi yao.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu Hospitali yangu ya Bububu na KMKM ile ya Mtoni hospitali kwanza inafanya vizuri sana Hospitali ya KMKM Mhe. Mwenyekiti nashukuru wale vikosi wanafanya kazi bila ya kujali usiku, mchana lakini akienda pale mgonjwa anapata unafuu mimi nawashukuru sana Mwenyezi Mungu awazidishie na pale jengo jengine linajengwa la Wazazi na Watoto Mwenyezi Mungu atuwezeshe jengo lile limalizike na madaktari waje kufanya kazi vizuri, na nawapongeza wananchi wangu wote wa Jimbo la Mtoni wanakwenda pale na wengine wanakuja kutoka maeneo tofauti. *(Makofi)*

Vile vile, Hospitali ya Jeshi Bububu inafanya vizuri sana inasaidia sana wananchi kule Kihinani pale jeshini inafanya vizuri sana nawashukuru nawapaongeza sana jeshi kwa kujitolea na kusaidia kama kumuona daktari rahisi, dawa zenyewe rahisi wanakuwa na saa nyengine bure unapewa kwa hiyo nawashukuru.

Lakini, Mhe. Waziri kuna ahadi moja hapa ilikuwa dawa wapewe wale ndugu zetu wapewe dawa *free* za hizi Mnazi Mmoja, sasa sijui kama wanapewa hizi dawa KMKM Hospitali na kule Hospitali ya Bububu Jeshini. Sasa naomba unieleze kama wanapesa sawa kama hawapewi basi wawe wanapewa fungu wasaidiwe kwa sababu wanafanya kazi kubwa sana kituo kile cha KMKM, matokeo yangu naomba sana muelekezo wako Mhe. Waziri kwanza kwa ufupi unisaidie pia dawa wapewe kwa sababu wanasaidia sana niseme hivyo wanasaidia sana.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee katika ukurasa huu wa tano Hospitali ya Mnazi Mmoja naipongeza kwanza ilijitahidi kukusanya mapato, ilipangiwa kukusanya mapato karibu milioni 221,000,000 ni fedha nyingi sana, lakini katika mwaka huu wameweza kukusanya katika milioni 144,000,000 Zanzibar kwa mapato ya Wizara ya Afya, hili jambo zuri na bado tunaweza kukusanya mapato zaidi.

Kwa kweli, kama alivyosema Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali haya matibabu kutibiwa ni fedha nyingi sana na wananchi wengine hawawezi kulipa. Lakini hapo utapolipa ni fedha nyingi sana unapata, hakuna kitu ghali duniani Mhe. Mwenyekiti kama dawa unaweza ukakuta dawa kidogo kidonge kimoja ukaambiwa shilingi elfu tano, shilingi elfu kumi kimoja tu hasa hebu nambie pesa hizi nyingi kama hizi zinakwenda wapi saa nyengine na dawa hapo Hospitali ya Mnazi Mmoja zengine zinauzwa au unakwenda kununua au unalipa matibabu mengine kwa hiyo bado hizi pesa naomba sana tukusanye.

Mhe. Mwenyekiti, wamekusanya hizi kwa milioni 148,000,000 lakini tukusanye milioni 200,000,000 hatujafika lakini naomba sana tujitahidi kuzizingatia hizi pesa na kuzifuatia kiundani tuwe makini sana tuweze zisipotee kwa sababu hapa najua Mhe. Mwenyekiti kuna upotevu wa pesa, pesa zinaibiwa nyingi karibu pengine asilimia themanini zishaibiwa hizi pesa kwa hiyo tuwe makini katika ukusanyaji wa mapato katika Hospitali yetu hii ya Mnazi Mmoja ya Rufaa.

Sasa naomba nizungumzie mafanikio wa Wizara hii ya Afya. Mhe. Mwenyekiti, naipongeza sana wizara 2017/2018 mwaka jana mpaka mwaka huu tu kama wenzetu nampongeza Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kafanya kazi nzuri kajitahidi sana kwa hivyo na mimi nimpongeza sana ndugu yangu kwa sababu Mhe. Rais wa Zanzibar anajua kabadilisha lakini anajua kampeleka sehemu nyengine kufanya kazi na huku pia kamleta Jemedari mkubwa zaidi Mhe. Hamad Rashid kwa kazi yake hii ya Wizara ya Afya.

Lakini niseme kipaumbele cha kwanza wizara imefanikiwa kununua hii mashine ya *MRI* na sasa hivi *MRI* inafanya kazi, hii mashine ni pesa nyingi sana inafika dola milioni 1,800,000$ na hii mashine mheshimiwa ninachoomba tuizingatie kwa wafanyakazi wazuri. Mhe. Mwenyekiti, unaweza kwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja mashine hii ya fedha nyingi tu tumenunua serikali Mhe. Rais wa Zanzibar katafuta pesa tumenunua Ujerumani *Philips* hii mashine, unakwenda pale unakuta inatoa ripoti lakini unambiwa haitowi kwenye karatasi daktari aje asome pale pale kwenye kompyuta.

Mhe. Mwenyekiti, haya mambo ni aibu kununua *printer* ule wino wa *printer* ku-*print* hii ikuwa haiwezekani mgonjwa anaumwa anataka kupigwa *MIR* itazamwe kaumia wapi lakini unambiwa ku-*print* haiwezi. Sasa ni aibu hayo mambo madogo madogo mheshimiwa inashindikana jambo

hili la kununua pengine unakuta hata laki mbili au tatu haifiki *printer* na ukienda unambiwa hamna. Kwa hivyo, naomba sana mashine hii ni muhimu na ya fedha nyingi sana serikali imetumia hapa, hivyo ni vyema tuizingatie kwa kufanya kazi wananchi wetu waone matunda ya mapinduzi ya nchi yao kwa ajili ya hii mashine iweze kuwasaidia mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 31 pia serikali niipongeze sana hii mashine *DAN machine* tulipiga kelele sana Baraza lililopita tangu miaka mitatu nyuma minne mashine hii ilikuwa hamna mpaka leo na hapa serikali tayari imesaini mkataba huu wa manunuzi wa mashine hii ya *DNA*. Lakini bado nasema tumechelewa sana hii mashine ni muhinmu sana na najua serikali ina nia nzuri kununua na itanunua sio kama nasema haiwezi itanunua kwa sababu tayari ishaleta mambo mazuri hapa kusaini mkataba huu.

Kwa kweli, mashine hii Mhe. Mwenyekiti itatusaidia katika udhalilishaji jambo moja kubwa sana nchi yetu udhalilishaji hatumjui nani kafanya kitu hiki wewe mashine hii itatusaidia pale pale kutowa majibu mtu anohusika na mambo haya watoto wetu wanaumia huko mitaani bado, lakini ushahidi haupatikani. Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba mashine itakaponunuliwa wananchi wamepewe taaluma wapewe ufahamu mzuri elimu nzuri atakayefanya mambo haya mashine ipo itamtambua hiyo mashine muhimu kwa dunia katika nyanja tofauti yakiwemo kujua mtoto huyu wako, siwako hii mashine itatambua udhalilishaji utatambua, mambo mengi.

Kwa hivyo, nashukuru serikali kwa jitihada zao kubwa na Mhe. Rais wetu wa Zanzibar anajitahidi sana anajitahidi sana kwa mashine hii kuifatilia mpaka mimi nilipokwenda Ikulu kuzungumza naye katika kamati yetu ya Waheshimiwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa alizungumzia suala hili la udhalilishaiji, kwa hiyo mimi namshukuru na nia hiyo anayo najua hii mashine utakuja na itafanya kazi katika shughuli iliyokusudiwa kuwafichua wale ambao watakuwa na tabia hii ya udhalilishaji mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nende kwenye ukurasa wa 20 katika ufuatiliaji wa maji safi na salama kuondosha haya maradhi Mhe. Waziri nakushukuru wizara yako umeandika hapa katika huduma ya mazingira kufatilia maji safi na salama, kujua mazingira yote yalivyo katika wananchi wetu kupata haya mambo ya maradhi ya mripuko hasa vile vile. Lakini, Mhe. Mwenyekiti naipongeze na niseme ukweli bila kwa ubabaifu kwa mwaka huu mvua zilizokuja lakini tukiangalia maradhi haya mimi sijayasikia kutokezea kama miaka ya nyuma iliyipita. Kwa hivyo, najua serikali imepiga hatua kubwa sana kwa kufanikiwa kuzuwia haya maradhi kwanza ya mripuka kipindupindu kwa Wizara ya Afya kufuatilia usafi katika majimbo au maeneo yetu kidogo tumeweza vizuri na hata angalia maji safari hii hayakujaa katika maeneo mengi sana. Kwa hivyo, bado tufatilie mwakani tujipange mambo haya yasitokezee.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia suala hili la usafi pia tukiangalia vyakula ndugu zetu wamejitahidi wanauza vyakula vikiwa safi, wananchi wetu hawapati maradhi kwani Zanzibar ukitizama mheshimiwa wanakuja watalii kutoka sehemu mbali mbali wa ndani ya nchi na nje ya nchi. Sasa kama vyakula vyote vikiwa vibaya watalii wale watakula nini au maji yetu yakiwa machafu watalii wataumwa au mara nyengine hawaji tena kwenye kisiwa cha Zanzibar.

Pia kuna watalii kutoka Tanzania Bara wapo wanakuja sasa hivi ukienda Forodhani wakati wa jioni wanajaa tele wanakula pale. Chakula hujui kama kisafi au kichafu unajua wamesema

kwamba nzi wamekuwa wengi, lakini bado tunahitaji jitihada ya kupunguza mambo haya ili hiki kisiwa kionekane kama kipo kwenye usalama kuanzia chakula, maji na mambo yote mtu anakuja hapa anajua haumwi wala hapati tatizo lolote, hayo mambo yatatusaidia kupata pato la taifa kwa ajili ya wageni wetu hawa wanaokuja.

Kwa hiyo, naomba Wizara ya Fedha na Mipango bado ishughulikie usafi wa vyakula vyetu hawa wananchi wanaouza wapewe elimu, wasifungiwe ila wapewe elimu zaidi wajue wanaweka vyakula vyao usafi mgeni akija atumie vizuri, kisafi kimoto wapewe elimu iendelee mheshimiwa kwa sababu wanakuja watu hatuwajui wanatoka wapi, Tanzania nzima wanakuja hapa Zanzibar kutembea, hasa kipindi hiki cha sikukuu wanakuja watu wengi. Kwa hiyo, tuwape elimu wananchi wetu wapate faida kwa sababu hii nayo ni moja ya faida ya wananchi wetu kupata mapato yao au ajira zao kupitia vyakula. Kwa hivyo, tuwape elimu wafaidike na nchi yao na mapinduzi yetu ya 1964 kuona wao wanakuwa na maisha mazuri na ajira zao zinakuwa nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye malengo ya wizara kwenye ukurasa wa 26, niipongeze sana wizara kwa juhudi mbali mbali humu wamesema vifaa ikiwemo mashine ya *DNA* malengo yao wizara mwaka huu wameweka kununua hii mashine ya *DNA*. Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza najua kwa mwaka huu Mhe. Waziri mashine utanunua kwa *speed* yako kubwa uliyokuwa nayo utanunua hii mashine. Tukija mwakani hapa mashine itakuwa ipo na inafanya kazi kwa malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia nishukuru kujenga nyumba za madaktari katika hospitali za Abdalla Mzee. Jambo hilo pia nilipongeze sana serikali niseme kama bajeti iliyopita madaktari wetu wana hali ngumu hasa ukitizama nyumba wanayokaa ni shida, nilisema bajeti iliyopita hapa. Mhe. Mwenyekiti, usafiri daktari wetu hana ikitokea *emergency case*, ishawahi kutokezea daktari yupo anakaa jimboni kwangu Bububu tu pale, lakini kufika hospitali hana usafiri apande daladala. Mhe. Mwenyekiti, huyo daktari anakuja kumuokoa mwananchi anataka kufa yeye apande daladala inakuwa tunaharibu hata yale mandhari yetu au tunaharibu maisha ya yule mtu.

Kwa hivyo, naomba hao madaktari wapate usafiri mheshimiwa kama vespa au gari ndogo japo wakopeshwe walipe kidogo kidogo kupitia Benki yetu ya *PBZ*. Wakopeshwe vigari vidogo waende Japan Wizara ya Fedha iagize gari 50 *Vitz* au vespa ili wakopeshwe hawa ndugu zetu ili waje kuokoa maisha yetu. Sasa hapa serikali imeandaa kujenga hizi nyumba za madaktari kule Abdalla Mzee naipongeza serikali hili jambo ni zuri.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia haitoshi kuna madaktari wetu wengine hawana nyumba, hawana usafiri wakopeshwe pesa kupitia *PBZ* kuna mikopo nyumba za *ZSSF* hizo hapo chungu nzima zinajengwa, maghorofa yapo hapo basi wakopeshwe hao madaktari na walimu kwanza walipe hata miaka kumi mbele, na wao watakuwa hawawezi kuondoka kwenye nchi hii kwa sababu wana mkopo na maisha yao mazuri wataendelea kutumikia serikali hii na Wizara ya Afya kwa ujumla. Kwa hiyo, naomba sana iwaangalie hawa madaktari wetu Mhe. Waziri waangalie hali zao ni ngumu tukifanya utafiti ukitizama maisha yao ni magumu na wanatuokoa sisi.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kama Dkt. Ali Amour nimpongeze sana hata mimi kanitibu nilipokuwa mdogo. Kwa kweli, huyu ni daktari mzalendo kabisa tangu miaka hiyo yupo na hana nia ya kuondoka Zanzibar. Lakini madaktari wengi hawa vijana sasa hivi wanasomeshwa nje

wakitoka China, wakitoka kusoma huko wakija hapa na vyeti vyao wanafanya kazi mwaka mmoja halafu wanakwenda Tanzania Bara kwa ajili ya mshahara wanaolipwa. Mhe. Mwenyekiti, lakini ukitizama wengi wameshaondoka serikali inasomesha wakimaliza wanaondoka, lakini nimpongeze Dkt. Ali Amour yeye ni mzalendo miaka yote yupo hapa na yuko Hospitali ya Mnazi Mmoja ni daktari wa watoto. Nampongeza sana na Mwenyezi Mungu amzidishie imani na atamlipa kesho siku ya kiama kwa juhudi zake kubwa huyu Dkt. Ali Amour na jitihada zake kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze Dkt. Jamal yupo hapa *Al-Rahman* anafanya kazi nzuri, anatusaidia sote nimpongeze kwa juhudi na uzalendo wake. Ukitizama mshahara wake sio mkubwa lakini hawezi kuondoka kwenda nchi nyengine au kwenda Tanzania Bara kufanya kazi kwa sababu ya uzalendo niwapongeze. Mhe. Mwenyekiti, wengine wapo lakini nimewataja hawa wawili kwa juhudi zao kubwa wanajitahidi sana, hivyo serikali iwaangalie hawa Dkt. Jamal aangaliwe sana, Dkt. Ali Amour aangaliwe sana maslahi yake na serikali imuongezee kama tunzo fulani kwa kufanya kazi kwa uzalendo hapa Zanzibar. Kwa hiyo, naomba sana madaktari wengine wote nimesema waangaliwe pia mheshimiwa kwani wana kazi kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 16 haraka haraka hapa kwenye kitabu chetu kimesema kwamba karibu watu 2,106 walichunguzwa asilimia 75 wanasumbuliwa na maradhi ya kisukari, wanasumbuliwa na maradhi ya shindikizo la damu. Mhe. Mwenyekiti, hili tatizo ni kubwa sasa hivi na ukitizama matatizo kama haya waziri ameandika hapa watu wengi wanasumbuliwa kila ukifuatilia watu wengi wakipimwa sasa hivi utakuta wana maradhi ya sukari au presha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kama mimi ni Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kutoka Baraza la Wawakilishi tulipata semina moja kule Bungeni alikua *professor* mmoja anaitwa Barnaby anatoka MOI Hospital ya pale Muhimbili. Huyu ni daktari wa Rais Mstaafu wa awamu iliyopita Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete huyu ni daktari wake. Huyu ni *professor* yaani huyu jamaa anaelewa maradhi haya mawili kiundani kabisa. Tulipata semina hiyo wabunge wote mimi nashukuru ilitusaidia sana, lakini naomba Mhe. Mwenyekiti kama itakuwa semina hii ifanyike kabla ya Baraza kumaliza hili la bajeti mimi huyu *professor* nitazungumza nae na nitamleta hapa kwa gharama zangu aje kutupa semina sisi wawakilishi sote japo ukumbi wa juu ili aje kutuelimisha Waheshimiwa Wajumbe kuhusiana na masuala haya ya presha na sukari.

Mhe. Mwenyekiti, ni jambo la muhimu sana kupata elimu haya maradhi sio kama yana kinga, hayana chochote lakini ukipata elimu ya maradhi haya itatusaidia sote. Kwa hiyo, naomba nataka nijitolee huyu *professor* nitazungumza naye na nitamleta kwa gharama zangu bila ya mchango aje hapa siku moja atufanyie semina wawakilishi sote tukae na tupate elimu ya maradhi haya, kwani maradhi haya ni hatari.

Kwa hiyo, naomba sana jambo la muhimu sana waziri ulisema katika kitabu chako kuhamasisha wananchi wetu wafanye mazoezi ni jambo muhimu sana, bila ya mazoezi hakuna tiba yoyote au hakuna dawa itakayokusaidia Mhe. Mwenyekiti kwa sababu mazoezi wanasema kila binadamu ni muhimu kufanya mazoezi, hakuna binadamu aliyekamilika bila ya mazoezi hiyo elimu sisi hatuna. Kwa hiyo, huyu akija atatufahamishe nini umuhimu wa mazoezi kukimbia maradhi haya

ya kisukari na presha. Kwa hiyo, naomba sana mheshimiwa tuliangalie na ikiwa tayari mimi nitafanya mawasiliano nae huyu *professor* aje hapa atupe semina.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 27 wa kitabu chetu, Mhe. Waziri ametwambia jumla ya wagonjwa 271 waliosafirishwa nje ya Tanzania kwenye matibabu, kati ya watoto 30 wamepata maradhi ya moyo wamepekwa Israil wengine India. Mhe. Mwenyekiti, serikali inatumia fedha nyingi sana kwenye suala hili na ukitizama hapa waziri ametuandikia gharama yake bei gani lakini naamini mimi ni mamilioni ya fedha itakuwa tunadaiwa.

Kwa hiyo, naomba tujihamasishe kama Mhe. Rais wetu alivyojitahidi na viongozi wetu Makamu wa Pili pamoja na waziri wetu kununua hizi mashine tuwatafute wataalamu wetu wenyewe ili waweze kutusaidia. Mhe. Mwenyekiti, kuna wagonjwa wengine wanapelekwa India na hawana sifa ya kupelekwa India, kwa sababu ukitizama kwanza huko India matibabu ni *very expensive* naweza kusema, ni dola 5000 kwenda mbele.

Mhe. Mwenyekiti, nishakwenda India mara tatu kumpeleka mzee wangu hakuna dola 400 au 500 unakwenda na *ten thousand dollars* zinakwisha kule hakuna mchezo. Mhe. Mahamoud Thabit Kombo unafahamu unaniangalia, unafahamu hakuna rahisi, hakuna dola 400 kama alivyosema Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali amezungumza lakini hiyo ni *checkup*. Lakini kuna mambo yakihusika pale dola 10,000 itakatika na waziri anajua gharama ni kubwa na serikali yetu itakuwa inabeba mzigo kupelekwa watu karibu 700 au 200 nje kila mwaka au kila muda mwisho tutafilisika kwani kodi yetu hii anayoikusanya waziri itaishia kupeleka watu nje na watafaidika watu wa nje.

Mhe. Mwenyekiti, kule India ukiuliza wanakuja wagonjwa kutoka nchi mbali mbali, mimi nishakwenda kule Chennai nishakwenda mimi, nishakwenda Bombay wanafanya kama utalii wao kwa wagonjwa, kama kipato chao cha utalii. Wanajua ndege inakuja na wagonjwa wanakuja sasa na sisi tuna uwezo na tuna ma-*professor* wazuri kutoka hapa Tanzania Bara wanaweza wakaja hapa na mashine ya *MRI* na wataalamu wakatibu kupitia *e-health* mambo ya *electronic* ya ugonjwa unapata kuzungumza na daktari aliyekuwa nje na kukupa dawa za magonjwa yale. Inaweza ukawa upo hapa lakini unazungumza Marekani na mtu tufunge mtambo kama huo wa *e-health* wenzetu wanafanya hivyo itasaidia kupunguza hii gharama ya kupeleka watu nje.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu unaweza kutoka hapa ukienda nje unaumwa, lakini dawa unayopewa hapa haikutibu ukifika nje unatibiwa na unapona, kwa sababu gani wana utaalamu zaidi. Sasa tukifunga mitambo kama hii ya kusaidia na serikali ina nia hiyo imeanza sasa hivi *e-tax* itaanza kufunga, *e-education* haya mambo yatasaidia kupunguza gharama hii ya kupeleka wagonjwa wetu nje kwa asilimia kubwa. Kwa hiyo, Mhe. Waziri naomba sana tuangalie kutibu watu wetu hapa hapa tufunge hizi mashine wataalamu tuwe nao wazuri, tusaidiane nao tutatibu naamini kama tutafanikiwa wananchi wetu wengi ni masikini na hawana uwezo wa kwenda nje, tukifanya hapa hii Wizara ya Afya itatusaidia kuweza kuwaokoa.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nimalizie kwenye ukurasa wa 30 matokeo ya ukaguzi ya kupelekea kuyafunga maeneo karibu manne. Mhe. Mwenyekiti, jambo la mwanzo hili suala la chakula wajumbe wamesema kwamba kuna mchele umekamatwa hapa karibu tani 569. Sasa hili jambo ni la aibu hivi vyakula wanakula binadamu sio mtu mwengine. Leo kama vyakula vinaingia

kwenye nchi na vinakamatwa au vinakuwa havifai binadamu kula hivyo tunahatarisha maisha ya wananchi wetu. Kwa hiyo, naomba sana suala hili Mhe. Waziri uliangalie vizuri sana tusifanye masihara kwenye mambo ya chakula, mambo ya dawa, mambo ya vipodozi. Wengi ukiangalia kwenye mitandao utakuta dada zetu wanaharibika nyuso, wanaharibika kila kitu kwa sababu wanatumia madawa sio, *lotion* sizo hawajui. Wao wananunua wanaambiwa utakuwa mweupe kidogo wanatia matokeo yake baada ya miezi sita mtu anakuwa anabadilika. Kwa hiyo, tuwe makini kwenye hivi vipodozi tuviangalie madawa yetu yanauzwa hapa wamesema pia wajumbe kuna dawa zinaandika made in Marekani kumbe sizo dawa ukienda India hazipo, hiyo kweli ipo. Kwa hiyo, tuangalie kwenye madawa haya huko kwenye *pharmacy* zetu wanauza.

Mhe. Mwenyekiti, tuangalie dawa ziwe sahihi na zifanyiwe *checkup* ziangalie angalau kuwe na watu *inspectors* wawe wanapitia kama watu wa kodi *ZRB* au watu wa umeme wa TUKUZA wanafanya uchunguzi kila baada ya muda wanapita. Kwa hivyo, na hawa wapiti waziangalie dawa na bei zake ndizo sahihi, wakati mwengine unaweza ukauza dawa hawa watu wa *pharmacy* wanatia bei wanazotaka wao, dawa ya kuuza mia tano inauzwa elfu mbili, kuwe na watu maalum wapitie kila *pharmacy* iwe inapitiwa na inaangaliwa *expiry date* ya dawa, inaangaliwa dawa ndio ziko sawa viwango nchi inayotoka ifatiliwe kiundani, Mhe. Mwenyekiti tunao uwezo huo wa kufanya na kuangalia uzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tumeona kama kiwanda kimoja kinatoka Uturuki kuleta dawa vyengine vyote havifai. Lakini ukiangali hapa kuna dawa nyingi na kuna viwanda vya India, Pakistan kuna sehemu mbali mbali Nigeria, Senegal wanaleta dawa hapa sasa tuangalie hizi dawa ndizo za binadamu. Mtu unaweza kula dawa lakini huponi, dawa ni nzuri lakini ile dawa haina viwango. Kwa hiyo, Mhe. Waziri umeandika katika kitabu chako ufatilie na naamini unao watu makini na wawe wakali na wazalendo wa nchi hii wasibahatishe kwenye suala la dawa, chakula na vipodozi tufanye kazi za uhakika tusiwe tujali pesa tukawauzia wananchi wetu ambao ni masikini wakaja kuumia kwa jambo dogo kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana na mimi naunga mkono bajeti hii na naomba sana tumpe waziri nafasi akafanye kazi kwa bajeti yake nzuri sana hii haijawahi kutokezea katika Baraza letu tukufu bajeti kubwa kama hii, haijawahi kutokezea. Kwa hivyo, naomba tumpe nafasi akafanye kazi Mhe. Waziri mwakani hapa mzee wangu, baba yangu nakuheshimu sana najua itakuja ripoti nzuri na manufaa tutayaona kwa wananchi wetu hasa Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja kwa kazi nzuri na tutaweza kufaidika katika nchi yetu. Nakupongeza sana na nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti kunipa nafasi hii naunga mkono asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Hussein Ibrahim Makungu kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Afya kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2018-2019.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kusimama hapa nikiwa mchangiaji wa mwisho kwa leo hii katika hotuba hii niweze kuchangia vizuri na nifahamike na mchango wangu ukafanyiwe kazi.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutuwasilishia hotuba yake hii kwa ufasaha na kusema kweli yale yote yaliyokuwa yameandikwa humu ni mazuri naamini yatatekelezwa. Pia niipongeze kamati kwa kutoa mashirikiano katika wizara hii kuweza kufanya kazi zao vizuri. Mhe. Mwenyekiti, vile vile nimpongeze Mhe Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanazozifanya katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikianza mchango wangu nianze kuunga mkono hatua zilizochukuliwa kaulimbiu ya wizara "Matibabu Bure ni Haki kwa Kila Mwananchi". Mhe. Mwenyekiti, hapa niipongeze wizara kwa kutekeleza Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kaulimbiu hii niseme kwamba kuhusu suala la mama na mtoto hili tayari tulikuwa tushapewa taarifa kwamba kina mama na watoto watatibiwa bure, lakini bado Mhe. Waziri nataka niwambie katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja sehemu ya mama wanapokwenda kujifungua bado kuna watu wanachangishwa.

Mhe. Mwenyekiti, mzazi anapokwenda hospitali anaambiwa achangie kama atapima damu kujuulikana damu yake ikoje anaambiwa achangie au akitaka kupima sukari anaambiwa achangie hata mtoto mchanga ambaye amezaliwa akitaka kuangaliwa sukari anatakiwa achangie. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri suala hili aliangalie lipo na linafanyika pamoja na kaulimbiu ya kusema kwamba kila mwananchi anatakiwa apatiwe matibabu bure lakini hili suala lipo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa ni kwamba kuna tatizo la pale mgonjwa pale anapozidiwa kama anahitaji damu, pale linapotokea tatizo hili la damu mgonjwa anaambiwa akatafutiwe damu lakini hatibiwi mpaka damu ile irejeshwe. Sasa naomba kwa makusudi kama patatokezea mgonjwa anahitajika damu basi atibiwe halafu watafutwe watu wake wairejeshe ili kuokoa mwananchi yule.

Kwa kweli, tatizo hili lipo wagonjwa wetu wanapokuwa na tatizo la damu wanaambiwa kwamba hawatibiwi kama anahitajika damu basi ikatafutwe damu ndio atibiwe. Sasa namuomba Mhe. Waziri kwa makusudi ulifanyie kazi hili ili iwaonee huruma wananchi wetu mgonjwa anapopata tatizo hili la kutakiwa damu basi atibiwe kwanza halafu masuala ya damu yatatafutwa baadae. Pia uwekwe mkakati waseme mgonjwa hatolei mpaka ile damu irejeshwe, ni bora wafanye hivyo kuliko kumuacha mgonjwa anaumia lakini mpaka ipatikane damu ndio atibiwe hapa tutakuwa hatutendi haki itakuwa tunamuumiza yule mgonjwa. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri kwa makusudi suala hili lifanyiwe kazi kama mgonjwa atatokezea anahitajika damu kama anatakiwa chupa tatu basi aingizwe chupa tatu halafu ufanywe utaratibu, sio aachwe mpaka iletwe damu ndio atibiwe, hili itakuwa sio suala la kiungwana.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kuhusu programu ya Huduma za Tiba. Mhe. Mwenyekiti, mimi niende katika Bodi ya Wakala wa Chakula na Dawa. Kwa kweli, naipongeza bodi tayari ipo imechaguliwa lakini ninachotaka kusema kwamba bodi hii inafanya kazi zake vipi nataka nipate

maelezo Mhe. Waziri wakati atakapokuja, pia niungane na waheshimiwa wenzangu kuhusu masuala haya ya chakula na dawa zinazoingia zishapitwa na wakati.

Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli waheshimiwa wengi wameanza kulisema hili suala na kuhusu chakula kinachoingizwa kinapita wapi pale bandarini wakati watu hawa wa afya wapo pale bandarini na dawa zilizokuwa zimepitwa na wakati zinapitaje katika maduka mpaka zinafika wakati watu wetu hawa wapo na wanafanya kazi zao na bodi nimeipongeza pia ipo. Kwa hiyo, mimi atapokuja Mhe. Waziri anambie unatumika utaratibu gani wa kupitisha vitu bandarini. Pia namuomba wakati wa majumuisho atupe ufafanuzi wa kina unaotumika katika ukaguzi wa vyakula katika bandari zetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu nije katika Mradi wa Kupandisha Hadhi Hospitali za Vijiji kuwa Wilaya na Wilaya kuwa Mkoa. Mhe. Mwenyekiti, naipongeze serikali kwa makusudi kufanya suala hili zuri, lakini naomba pamoja na kazi hii nzuri wanayotaka kuifanya ya mradi huu wa kupandisha hospitali zetu za vijiji kama walivyotwambia katika kitabu chao hiki, basi wanapotaka kufanya kazi hiyo wawe makini hasa kuhusu majengo kwa ukarabati.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukarabati kama walivyotwambia katika kitabu kuwa Hospitali ya Makunduchi inatarajiwa kuwa ya ghorofa. Naomba lisimamiwe vizuri suala hili tusije tukapata malalamiko au changamoto kama majengo mengine ya wizara yanapokuwa hayana kiwango.

Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli hapa tuna malalamiko mengi kuhusu majengo ya serikali yanakuwa hayana kiwango. Kwa hivyo, naiomba wizara pamoja na kazi hii wahakikishe wanasimamia ili tena tusirejee kupata majengo yaliyokuwa hayana kiwango.

Pia nikiendelea hapo hapo kuhusu hospitali hizi za vijiji zinazotaka kupandishwa kuwa wilaya, katika maeneo ambayo yako mbali mfano mgonjwa kaumwa usiku anataka kwenda hospitali akienda katika Kituo cha Afya cha Fuoni kama kashikwa na homa anaambiwa hapa sisi hatupokei mgonjwa wa homa tunapokea wazazi tu aende Hospitali ya Mnazi Mmoja. Usiku huo mtu hana gari pale katika kituo keshafika lakini anaambiwa hatupokei mgonjwa wa homa tunapokea wazazi. Namuomba Mhe. Waziri waangalie basi warejeshe utaratibu wa kuwepo madaktari katika vituo vidogo wawasaidie wananchi, usiku atoke anakotoka mpaka afike Hospitali ya Mnazi Mmoja hili ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika Programu ya Uendeshaji wa Uratibu wa Wizara ya Afya. Nataka niipongeze wizara kwa juhudi wanazozichukua kuhusu kukamilisha mchakato na uanzishaji wa bima ya afya. Hili ni suala zuri na wizara nyingi tayari zinalalamika kuhusu bima ya afya. Kwa kweli, suala hili tulikuwa tunalipigia kelele, lakini naona sasa limeshafika hatua nzuri na naamini litatekelezwa na wizara zetu, wafanyakazi wetu wataweza kupata bima ya afya.

Pia nilikuwa nataka nizungumze kuhusu ajira za wafanyakazi wapya katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kupitia programu hii kusimamia suala hili kwa kina kuajiri wafanyakazi wenye uzeofu na elimu katika fani hizo. Mhe. Mwenyekiti, nimesema hili tuondokane na matatizo madogo madogo au changamoto na malalamiko katika hospitali zetu hizi, kwa sababu tayari kuna mifano hai imejitokeza, mgonjwa akienda hospitali

linaweza kutokezea tatizo. Kwa mfano, kijana aliyeletwa hapa Barazani tuliyemuona baada ya kufungwa mpira katika mkono wake na kutokezea matatizo ya kukatwa mkono. Sasa namuomba Mhe. Waziri masuala haya ayafuatilie ahakikishe wafanyakazi anaowaajiri wawe na elimu, wawe na uzoefu ndio awaajiri. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu nije katika utafiti. Katika programu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, Mhe. Waziri namuomba wakati atakapokuja kufanya majumuisho atupatie ufafanuzi wa kina juu ya tafiti hizo zinazofanywa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Pia nataka kujua baada ya tafiti hizo kufanyika huwa kunachukuliwa hatua gani kwa baadhi ya changamoto zilizogundulika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea niipongeze serikali kwa hatua inayotaka kuchukua ya kuhusu mashine ya *DNA*. Kusema kweli naipongeza sana serikali kwa sababu malalamiko mengi na kilio chetu kikubwa kuhusu suala hili naamini litamalizika. Kilio chetu hiki ni kikubwa kwa sababu tukipata mashine hii ya *DNA* naamini matatizo mengi yatatuondokea.

Mhe. Mwenyekiti, kipindi kilichopita waheshimiwa wengi walikuwa wanapiga kelele kuhusu suala hili, lakini tunashukuru serikali imeliona na tayari wamelifanyia kazi, naamini matatizo na changamoto nyingi zitamalizika.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Magharibi naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe, muda wetu uliobaki ni kama dakika kumi, lakini kabla ya kuakhirisha kikao hiki basi nilikuwa naomba kwanza niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe, lakini nichukue nafasi hii kuwapongeza wajumbe wote waliochangia katika wizara hii na wizara nyengine tafauti.

Waheshimiwa Wajumbe, ukumbusho wangu nilitaka niwakumbushe kwamba sisi Baraza tunaliendesha kwa mujibu wa Kanuni zetu na niwapongeze na kuwashukuru baadhi ya Kanuni nyingi mnazielewa na mnazijua, niwapongeze sana. Lakini nataka niwakumbushe katika Kanuni ya 95(1) Aina za Mjadala. Waheshimiwa Wajumbe "Mjadala kwenye Baraza utakuwa ni wa jumla na mjadala kwenye Kamati ya Matumizi utahusu vifungu mahsusi".

Waheshimiwa Wajumbe, nimeona niwakumbushe hili kwa sababu naona malalamiko yamekuwa mengi kuhusiana na kuchangia kwetu. Lakini katika kifungu cha 98(4) tumetakiwa sisi wajumbe kifungu hicho "Masharti ya Hoja ya Kupunguza Fungu". Waheshimiwa kifungu hiki ni hoja ya kupunguza fungu lolote kwa mujibu wa fasili ya 7(c) - (g) ya kanuni hii itakubaliwa, isipokuwa tu kama mambo yafuatayo a, b, c, mpaka haya yakitimizwa.

Waheshimiwa Wajumbe, nimeona niwakumbushe hili katika kifungu hiki cha 98(4) "Mjumbe yeyote atakayeeleza nia ya kupunguza fungu wakati wa mjadala, anaweza kuomba ufafanuzi au maelezo zaidi katika kifungu husika wakati kitakapofikiwa na Kamati ya Matumizi".

Waheshimiwa Wajumbe, pia katika kifungu hicho cha 7(a, b, na c) "Hoja ya kupunguza fungu lolote katika Makadirio ya Matumizi ya mwaka itatolewa wakati kifungu kinachohusika cha fungu hilo kitakapokuwa kinajadiliwa na Kamati kwa namna ifuatavyo: (a) Kwa kutoa shilingi moja ikiwa ni ishara ya kutoafiki matumizi ya kifungu maalum; (b) Kwa kupunguza kiasi fulani cha fedha ikiwa ni ishara ya kutoridhika na jambo maalum ambalo Mjumbe alilitolea taarifa wakati wa mjadala kwenye Baraza. Isipokuwa taarifa itatolewa kabla ya Kamati ya Matumizi kukaa na Majadiliano yatahusu tu jambo maalum lililotolewa taarifa".

Waheshimiwa wajumbe (c) inasema: "Mjumbe atayetaka kutoa hoja ya kupunguza fungu lolote, ataeleza nia yake hiyo wakati anachangia Makadirio ya Wizara inayohusika na Matumizi hayo".

Waheshimiwa Wajumbe, nilitaka niwakumbushe kwa sababu tumegundua baadhi yao wanakuwa wanachangia lakini hawatoi ile nia na mwisho wa siku tukikaa hapa katika Kamati ya Matumizi Waheshimiwa wale huwa wanahoji na wanaona kama kiti kinawaonea. Waheshimiwa Wajumbe, nilikuwa nawakumbusha hili tuzisome hizi kanuni kwa sababu kiti hakina nia ya kuwazuia wajumbe katika michango yao, lakini tufuate zile taratibu ambazo tumejiwekea sisi wenyewe, tukizifuata taratibu zile basi nina imani sote tutakwenda vizuri na kila mtu haki yake ataipata kwa vile stahiki zinavyokuwa, ndio maana nikasema niwakumbushe. Ni mahodari sana Waheshimiwa Wajumbe kwa hizi kanuni na mnazipitia, lakini na nyengine tuone tunazipitia ili twende sambamba tusione kama kiti kinaonea. Kiti hakimuonei mjumbe yeyote ndani ya Baraza hili, tunapoona kuwa kanuni zimekiukwa basi kiti kitaelekeza kwa mujibu wa hizi kanuni tunazozielewa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, wengine walikuwa wanasema, isijekuwa hapa nasema kabisa. Mimi nimeshukuru wajumbe wengi waliochangia leo waliotoa nia katika kuzuia mafungu wamesema, basi wasubiri kesho ikiwa hawajafanyiwa hivyo wana haki ya kulalamika. Kwa hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe tuzisome kanuni, tuzipitie kwa umakini na tuone tunaendesha Baraza letu hili bila ya kulaumu kiti au kulaumiana sisi wenyewe kwa wenyewe.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo naomba niwashukuru sana kwa utulivu wenu na michango yenu, lakini pia naomba nimpongeze Mhe. Waziri wa Afya kwa uwasilishaji pamoja na watendaji wake wote wa Wizara ya Afya. Pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati na aliyesoma hotuba ya kamati kwa niaba ya mwenyekiti, nawapongeza sana na ninawashukuru kwa utulivu wenu. Naomba niakhirishe kikao hiki mpaka kesho tarehe 05/06/2018 saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

(Saa 8:52 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka
tarehe 05/06/2018 saa 3:00 asubuhi)